

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 25 Juni, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kama ilivyo ada swali la kwanza kwa leo linaelekezwa Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na linaulizwa na Mheshimiwa Clement Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi.

Na. 94

**Ombi la Kufuta Hati Miliki ya Mashamba – Kilosa**

**MHE. CLEMENT B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mashamba makubwa yaliyoko katika Majimbo ya Mikumi na Kilosa yametekelizwa na wamiliki kwa miaka minge sasa; na kwa kuwa, wanavijiji waliokuwa vibarua, enzi hizo, wamezaliana na kuongezeka sana na hivyo kukosa maeneo ya kulima hali inayosababisha wahitaji maeneo hayo ili wajishughulishe na kilimo na hivyo kupunguza umaskini na kujiletea maisha bora:-

Je, Serikali imefikia hatua gani kuhusu ombi la Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa lililowasilishwa Ofisi ya Waziri Mkuu la kuzifuta hati miliki za mashamba hayo ambayo orodha yake iliambatanishwa katika barua hiyo?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clement Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro unayo mashamba makubwa yaliyomilikishwa kisheria lakini hayaendelezwi kama ilivyotarajiwa. Hali hii imekuwa ni kikwazo katika kufanikisha malengo na juhudzi za Serikali za kuinua uchumi na kuongeza pato la Taifa kutokana na shughuli zilizotarajiwa kufanywa katika mashamba hayo; kuongezeka kwa kipato cha wananchi kutokana na ajira inayoweza kupatikana katika mashamba hayo. Aidha, kutokana na kukosa haki ya kuyatumia mashamba hayo maeneo hayo yamekuwa ni chanzo cha kuibuka kwa migogoro mingi ya ardhi pale baadhi ya wananchi ama wameyatumbia au kuyavamia kwa lengo la kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilikwishatoa maelekezo kwa Uongozi wa Mkoa wa Morogoro kuandaa orodha ya mashamba yasiyoendelezwa ili kuiwezesha Serikali kufuta Hati Miliki za mashamba hayo. Mkoa umetekeleza maelekezo hayo baada ya Halmashauri kukamilisha taratibu muhimu za kisheria zinazohitajika kufanywa. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imepokea taarifa ya Mkoa yenye mapendekezo ya:-

- Kufuta miliki za mashamba 138 na ambayo yana ukubwa wa hekta zaidi ya 187,600.
- Ugawaji upya wa mashamba kwa wanaoyahitaji.

Katika taarifa hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imependekeza kufutwa kwa miliki za mashamba 39 yenye ukubwa wa hekari 34,350. Kwa kuwa wamiliki wa mashamba makubwa hawako Morogoro tu Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI, imeziagiza Halmashauri zote nchini kuwasilisha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi taarifa kuhusu mashamba yanayohodhiwa bila kuendelezwa ili hatua za kufuta miliki zao zichukuliwe. Maagizo hayo yamo kwenye barua Kumb. Na. CHA. 203/307/01/43 ya tarehe 28 Februari, 2008 na yalitumwa kwa Makatibu Tawala wa Mikoa yote nchini. Kwa kuzingatia taratibu za kisheria zinazohitajika kufanywa, Halmashauri zinaendelea na utekelezaji wa maagizo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ofisi yangu inatekeleza maelekezo haya ya Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali muhimu ikiwa ni pamoja na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Wizara ya Fedha na Uchumi, Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma na Kituo cha Uwekezaji. Utaratibu huu wa kushirikisha wadau hao una lengo la kuiepusha Serikali kwenye gharama kubwa za fidia na utatuza wa migogoro baada ya Hati Miliki za mashamba hayo kufutwa na pia kurahisisha na kuweka utaratibu mzuri na wa haki wa kugawa maeneo ya mashamba haya kwa wanaoyahitaji. Hivyo, napenda kumshauri Mheshimiwa Mbunge kuwa na subira wakati Serikali ikiendelea kulifanya kazi suala hili. Baada ya kukamilika kwa kazi hiyo Waheshimiwa Wabunge watafahamishwa matokeo ya kazi hiyo.

**MHE. CLEMENT B. LYAMBA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake yenye kutia matumaini kwa wananchi na wanavijiji katika maeneo husika hasa katika Kata za Masanze, Kilangali, Mabwelebwele,

Tindiga, Malui, Zombwe na Ulaya. Pamoja na majibu hayo naomba Mheshimiwa Waziri aweze kutoa *time frame* anayodhani ni muafaka ambapo anafikiri hatua hizo alizozieleza zitakuwa zimekamilika, kwa sababu wanavijiji wana shauku kubwa sana ya kuweza kuanza shughuli hizo za kujiinua kiuchumi kwa kilimo.

Swali la pili, ni kwamba je, Serikali inaweza kutoa ahadi ya kutoa mwongozo katika ugawaji wa mashamba hayo wapewe vipaumbele wanavijiji wadogo wadogo, wakulima wanaozunguka mashamba hayo kabla ya kuwafikiria wafanyakazi na wafanyakashara wengine wengi wanaweza pia kutoa maoni kama hayo?

Ahsante Mheshimiwa Spika.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, katika swali hili la kwanza anataka kujua kwamba tunaweza tukachukua muda gani katika zoezi hili, ili liweze kuharakishwa na wananchi waweze kupata hiyo huduma ambayo wanataka kuipata kwa maana ya kupatiwa mashamba.

Nimeeleza mchakato mzima ambao unahitajika hapa kwa ajili ya kazi hii na hapa tunazungumza mambo makubwa. Unazungumza juu ya kwamba unam-*involve* Rais wa nchi katika maana ya kufuta hatimiliki.

Ninaamini kwamba zoezi hili sisi tutajitahidi kama Wizara kuhakikisha kwamba tunafanya haraka iwezekanavyo ili liweze kukamilika. Siamini kwamba ninaweza nikatamka hapa kwamba litachukua muda gani likaelezwa. Lakini naeleza tu nia ya Wizara katika maana ni kwamba tutahakikisha tunafanya haraka iwezekanavyo ili zoezi hili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kwanza ninaweza kutoa maelekezo hapa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ili wakulima wadogo wadogo waweze kuangaliwa kwa karibu zaidi. Hii mimi sidhani kama nina tatizo nalo kwa sababu nchi hii ni nchi ya wakulima na wafanyakazi na humu ndani mna wafanyakazi na wakulima wa nchi hii. Kama kuna haja ya kuona kwamba tunafanya hivyo katika Ilani ya Uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi tunatamka wazi wazi kwamba watapewa fursa za mwanzo mwanzo kwa maana ya kutumia ushirika. Kwa hiyo, naamini kwamba zoezi hili likikamilika hapa Serikali itahakikisha kwamba tunawasaidia wakulima wadogo wadogo ili waweze kupata mashamba haya kwa ajili ya kuweza kujikimu. Tusipofanya hivyo maana yake ni kwamba hawa wataendelea kuwa ni vibarua katika nchi yetu kitu ambacho ni kinyume kabisa na siasa yetu ya Ujamaa na Kujitegemea. (*Makofi*)

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, baada ya majibu mazuri ya Naibu Waziri ningependa kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali inayo mashamba makubwa sana katika Wilaya ya Kilombero ambazo ni sehemu za huko huko alikouliza Mbunge. Kuna shamba la Rwipa, Kotako, Rwipa ilikuwa tutengeneze sukari tukishirikiana na Wa-Cuba. Kotako ilikuwa tutengeneze shamba kubwa tukishirikiana na watu wa Korea, halafu Chita ni shamba ambalo kubwa sana walipewa JKT lakini

hawakuweza mpaka sasa hawaja-*develop* hata robo. Je, katika ardhi hizi ambazo ni kubwa sana Serikali inasema nini nazo zigawiwe kama jibu la kwanza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro umeshajipanga vizuri sana tena mchakato wao umeshakamilika wa mashamba yote ya Mkoa wa Morogoro likiwepo shamba la Rwipa, Chita na mashamba mengineo. Mgawanyo wa mashamba hayo kwa upande wa Morogoro tayari wameshaweka mapendekezo kwamba ni ekari ngapi wapewe wanavijiji, ekari ngapi wapewe wawekezaji. Kwa hiyo, mchakato wa Mkoa wa Morogoro kwa ujumla umeshakamilika na mashamba hayo yatagawanya kulingana na vipaumbele nya Mkoa vilivyoona. (*Makofi*)

Pia niongezee kwamba Mkoa wa Morogoro tayari zoezi hili limeshakamilika. Kwa hiyo, wao wako mbele kwamba imeshafika Wizarani, Wizarani tumeshakaa pamoja na kukaa tayari tumeshaweka mapendekezo ya nini kifanyike ili yaende kwa Mheshimiwa Rais. Nitoe rai kwa mikoa mingine ambayo tumeiandikia yenyenye mashamba kama hayo wahakikishe kwamba mchakato uanzie kwenye Wilaya uingie kwenye RCCs ili mashamba makubwa ambayo wamepewa wawekezaji na hawajayatumia waweze kutuletea mapendekezo ili tuyapeleke mbele ili Rais aweze kutengua hatimiliki za hao wanaomiliki mashamba makubwa ambayo mpaka sasa hivi hayajafanyiwa kazi. Kwa mfano Mkoa wa Tanga una mashamba mengi ambayo yamechukuliwa na wawekezaji lakini mpaka sasa hivi hayajafanyiwa chochote. Kwa hiyo niwaombe Waheshimiwa Wabunge mshirikiane na Halmashauri husika ili kuhakikisha kwamba mchakato huu unafanyika haraka kama ulivyofanyika kwa Mkoa wa Morogoro. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Bado tuko Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Swali sasa linaulizwa na Mheshimiwa Felix Kijiko, Mbunge wa Muhammwe.

Na. 95

### **Kituo cha Afya Kifura Kupatiwa Gari**

**MHE. FELIX N. KIJIKO** aliuliza:-

Kwa kuwa, vituo nya afya vilivyoko Kibondo vilikuwa vikipata msaada wa magari toka Mashirika ya kuhudumia Wakimbizi hasa IRC; na kwa kuwa, Mashirika hayo sasa yamefunga shughuli zao na kwamba, kituo cha afya cha Kifura bado hakina gari la kuhudumia wagonjwa licha ya kuahidiwa kupewa gari siku nyingi:-

Je, Serikali itakisaidiaje kituo hiki cha afya kupata gari ili kupunguza tatizo la vifo hasa nya akina mama wajawazito ambao hufariki kutokana na kushindwa kufika hospitalini kwa wakati?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhamwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kifura kiko umbali wa kilometra 32 toka Kibondo Mjini na kinatoa huduma kwa wakati wapatao 56,803 kutoka katika zahanati sita za Nyaruyoba, Busunzu, Kichanaga, Kigaga, Kasaka na Kigendeka. Pamoja na idadi kubwa ya watu wanaokitegemea kituo hiki, kituo kimekuwa kikikabiliwa na tatizo la usafiri wa wagonjwa baada ya gari ambayo ilikuwa ikitumiwa na kituo hicho kuacha kufanya kazi kutokana na ubovu tarehe 3/09/2007. Hata hivyo kituo hiki kilikuwa kikisaidiwa na zahanati ya Mkugwa iliyokuwa ikiendeshwa na Shirika la Wakimbizi.

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo yapo magari 4 kwa ajili ya shughuli za Idara ya Afya ambapo “*Ambulance*” moja ipo katika hospitali ya Wilaya na gari nyingine tatu ziko katika Vituo vya Afya vya Mabamba, Kakonko, na Nyanzige. Huduma za mawasiliano katika Kituo cha Afya cha Kifura zimeboreshwa; kituo kina mawasiliano ya simu na *Radio Call* ambazo zimevezesha kuwa na mawasiliano kati ya Kituo na Hospitali ya Wilaya pale huduma za usafiri zinapohitajika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali iko katika mkakati wa kuwarejesha Wakimbizi kwao, Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo imeomba magari yaliyokuwa yakitumiwa na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR) yakabidhiwe kwa uongozi Halmashauri ambapo idara ya Afya inategemea kukabidhiwa magari 3 (*Ambulance*) kwa ajili ya usafiri wa wagonjwa na gari nyingine aina ya “*Pickup*” 2 na lori moja la tani saba zitatumika kwa shughuli za Halmashauri. Kwa sasa Halmashauri iko katika hatua za majadiliano kati yao na Shirika hili na ni matumaini yetu kuwa magari haya yatatatua tatizo lililoko katika Kituo cha Afya cha Kifura. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuzisisitiza Halmashauri kuweka kipaumbele na kutenga fedha katika bajeti zake kwa ajili ya ununuzi wa magari ya kusafirisha wagonjwa.

**MHE. FELIX N. KIJKO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ambayo Naibu Waziri ameyatoa. Lakini kimsingi hapa tukiangalia tunategemea misaada zaidi ya kujitegemea sisi wenyewe. Anachokizungumza Mheshimiwa Naibu Waziri ni kwamba sasa wananchi wa Kibondo wategemee msaada wa magari ya Wakimbizi baada ya Wakimbizi kuondoka na bado ni ombi. Sasa je hatuoni kwamba Serikali inatakiwa kubeba mzigo wa kuwahudumia wananchi wa Wilaya ya Kibondo ambao sasa hivi vituo vyote karibuni havina magari na kituo kimoja chenye gari kwamba hilo gari ni bovu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, huu msisitizo tulioewe hapa wa kuomba msaada unatokana na asili ya swali lenyewe lilivyoulizwa hapa. Kilichoulizwa hapa kilielezwa je tunakisaidiaje kituo hiki kwa maana ya kwamba sasa wale waliokuwa wanapewa huduma ile wanaondoka pale. Kwa hiyo, kusema hivi sina maana kwamba tunatia msisitizo mkubwa kutegemea zaidi wahisani kutoka nje. Ninachosema tu ni kwamba yako magari pale ambayo sasa yanabaki na wale wanaondoka na kwa msingi

huo tunafikiri sisi kama Serikali na kama Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tunaweza tukasaidia katika mchakato mzima wa kuomba magari yale yabakie pale kwa ajili ya huduma inayozungumzwa hapa.

Lakini la pili tumejibu hapa kwamba Halmashauri yenyewe inatakiwa ihakikishe inaweka kipaumbele katika suala zima la Bajeti ili kuona kwamba kituo hiki kinasaidiwa. Mimi nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge ambaye ametambua kwamba kuna *problem* pale na ambaye hata na Mkuu wa Kigoma yuko hapa tunamwomba na kwa kweli tunaelekeza kwamba waende wakasaidiane ili kuhakikisha kwamba haya magari yanapatikana na kipaumbele kiweze kutolewa katika Kituo hiki cha Kifura.

Na. 96

**Ahadi ya Kuupatia Mji wa Tunduma  
Maji ya Kutosha**

**MHE. GODFREY W. ZAMBI (K.n.y. MHE. DR. LUKA J. SIYAME)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa, mwezi Oktoba 2007 Serikali iliahidi kupitia kwa aliyekuwa Waziri Mkuu wakati huo kuwa, wananchi wa mji wa Tunduma watapatiwa huduma ya maji haraka iwezekanavyo ili kukidhi upungufu wa maji Wilayani Mbozi:-

Je, utekelezaji wa ahadi hiyo umefikia hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dr. Luka Siyame, Mbunge wa Mbozi Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la maji katika Mji wa Tunduma ambapo asilimia 35 tu ya wakazi wa Mji huo ndio wanaopata huduma ya maji safi na salama. Serikali imeanza utekelezaji wa mpango wa kupunguza tatizo la uhaba wa maji katika Mji huo ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake. Lengo ni kuwa wanaoishi Mijini na wa Vijiji wapate huduma ya maji safi na salama katika maeneo na mwendo mfupi kutoka katika makazi yao.

Mheshimiwa Spika, mwezi Machi 2008, Wizara ya Maji na Umwagiliaji kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) ilitenga shilingi 121,045,524/= kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji katika mji wa Tunduma. Fedha hizo zilitumwa kwenye Mamlaka ya Maji ya Mji wa Tunduma kwa ajili ya kazi zifuatazo:-

- Kuchimba visima virefu vipya viwili;
- Kusafisha visima viwili vinavyofanya kazi;
- Kununua na kufunga “*submersible pump*” mbili kwenye visima vipya viwili na “*surface pump*” moja na mota kwenye “*booster station*”.
- Kununua bomba mpya zitakazoboresha mtandao wa maji.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa kazi hizo uko kwenye hatua mbalimbali kama ifuatavyo:-

- Visima virefu viwili, kimoja chenyе kina cha mita 80 na uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 20 kwa saa, na kingine chenyе kina cha mita 100 chenyе uwezo wa kuzalisha maji za ujazo 10 kwa saa tayari vimechimbwa;
- Visima viwili vilivyochimbwa zamani vimesafishwa ili kuongeza wingi wa maji;
- Zabuni za kuleta pampu mbili na mota zimekwishatolewa na vifaa hivyo vinatarajiwa kupatikana mwezi Julai 2008.
- Dira za maji 39 zimenunuliwa;
- Mchakato wa Zabuni ya kuleta mabomba yatakayoongeza mtandao wa maji inaendelea na mabomba yanatarajiwa kufika mwezi Julai, 2008.

Mheshimiwa Spika, kazi zote zilizopangwa zitakamilika mwezi Oktoba, 2008. Baada ya kazi hizi kukamilika huduma ya maji katika Mji wa Tunduma itaboreka kutoka asilimia 35 hadi asilimia 50. Katika mwaka 2008/09 Serikali itaendelea kuchunguza vyanzo vingine vipya vya maji kwa ajili ya Mji huo.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swalı moja tu la nyongeza. Aidha, nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Spika, Tunduma ni Mji ambao uko mpakani na ni mji ambao unakuwa kwa kasi kubwa sana. Lakini pia Tunduma ni Mji ambao umekuwa na matatizo sugu sana ya maji. Sasa pamoja na jitihada hizo za Serikali kulikuwa pia na ahadi ya

Mheshimiwa Rais kwamba Tunduma itapatiwa maji ifikapo mwaka 2010 na wananchi wa pale hawatakuwa na matatizo. Sasa je, Mheshimiwa Waziri anawaambia nini wana Tunduma kwamba hiyo asilimia 90 ambayo tumelewa maji yafike mijini itakuwa imefika itakapofika mwaka 2010?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, Tunduma ni mji mdogo ambao uko mpakani pale tunaelewa. Kweli ni ahadi ya Serikali kwamba ifikapo mwaka 2010 asilimia 90 ya wananchi angalau wanaokaa mijini wawe wamepata maji safi na salama ya kunywa.

Mheshimiwa Spika, ahadi hiyo nataka kusema bado iko pale pale. Kupanga ni kuchagua unawenza ukapanga asilimia 90 usifikishe kabisa. Kwa hiyo, sitaki kusema kwamba itakapofika mwaka 2010 basi tisini tunafika tunahesabu moja, mbili, tisini tayari tumepata. Inawezekana tukawa themanini na nane, inawezekana ikazidi hata tisini. Lakini ninachotaka kumhakikishia Mbunge kwamba ahadi hiyo ipo na ndiyo maana tumetoa fedha hizo kwa ajili ya kuendelea kupunguza makali ya maji.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo naomba nimkumbushe Mheshimiwa Zambi kwamba programu yetu ya kuendeleza sekta ya maji bado inao mpango wa kuendeleza miradi yote iliyopangwa chini ya *World Bank* mchakato uliopo bado unaendelea ili tuweze kupata fedha za kuendeleza miradi hiyo ya maji.

Matatizo makubwa tulionao sasa hivi ni kwamba Halmashauri zenyewe za Wilaya na za miji nazo katika kuandaa michakato kwa ajili ya kuandaa miradi hii ya *World Bank* bado wako nyuma kidogo na kazi tutaifanya sasa sisi Wizara ni kuhakikisha tunawapelekea wataalamu hasa Wahandisi kwa sababu michakato mingi wanayoileta inakuwa haikidhi mahitaji na hatimaye tunachelewa kuendeleza mipango hiyo. (*Makofi*)

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusu miradi hii ya maji, lakini kwa mji wa Tunduma na miji mingine kama Mwimbi na Matai ambayo iko mpakani na nchi ya Zambia inakuwa si picha nzuri sana inapoonekana upande wa pili wenzetu wanafanya mipango mizuri lakini sisi mipango yetu inasua hasa mradi wa *World Bank*. Ni mradi ambao unaonekana umeshindwa karibu nchi nzima. Je, Serikali inasema nini kuhusu hilo, kwa nini tusitumie fedha zetu za ndani ili kuinusuru miji ya Tunduma, Mwimbi, Matai, Nkasi ili iweze ikapata maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema mradi wa *World Bank* haujafeli. Matatizo yaliyopo hivi sasa ni kwamba sisi wenyewe bado hatujakidhi mahitaji yale na kukidhi ni kufuata yale masharti ambayo walitupa ili mkopo uweze ukatoka kama ulivyopangwa.

Tatizo ambalo nalionna mpaka sasa hivi ni kwamba Halmashauri zetu za Miji, za Wilaya bado tukizipelekea makaratsasi yale kwamba andaeni hivi utayarishaji bado ni dhaifu kwa sababu kwa mfano mpaka sasa ni Halmashauri za Wilaya na za Miji 63 tu ndizo zimekidhi tumezipelekea maombi ya *no objection World Bank*. Zingine tumezirudishia kurekebisha makabrasha yao halafu tena tuombe upya.

Kwa hivyo kama nilivyosema ni kwamba Serikali inafanya bidii kutumia fedha zetu za ndani hata Waziri wa Fedha alieleza hili lakini tuna kazi kubwa kidogo katika hili nataka niseme kwamba hatua kubwa ambayo inafanywa na Wizara ya Maji katika hili kwanza ni kuhakikisha kwamba tunapeleka wataalamu kusaidia Halmashauri za Wilaya kwa sababu ni kweli kabisa kwamba kuna udhaifu katika Halamashauri za Wilaya kuandaa mipango hii ili wenzetu nao wa *World Bank* waweze kuikubali.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, inaelekeea fedha nydingi zinazotoka nje zinatushinda kwa sababu ya kutimiza masharti fulani. Moja katika tatizo ambalo tunalipata ni uwezo wa kule ngazi ya chini ambao wanatakiwa kutimiza yale masharti kufanya. Kwa kuwa Serikali Kuu wanaelewa hili tatizo wanashindwa nini Serikali Kuu kuandaa kikundi cha wataalam wenye uwezo na uzoefu mkubwa wakaifanya hii kazi kwa ufanisi ili fedha ziweze kutumika katika hii miradi ya maendeleo badala ya kuwasukumia lawama hawa Halmashauri ambao uwezo wao ni mdogo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nimeeleza katika jibu la nyongeza hapa kwamba tunajua kabisa udhaifu uliopo katika Halmashauri za Wilaya na hata katika mipango ya Serikali Wizara zote zinazopeleka fedha katika utaratibu huu wa *D by D* Wilayani ukizichunguza sana utakuta kuna kipengele kinasema *Capacity Building*, uwezeshaji wa wale wataalamu walioko katika Halmashauri. Kama nilivyosema sisi Wizara ya Maji na Umwagiliaji baada ya kugundua kwamba kuna udhaifu mkubwa huo nimesema kabisa kwamba tunachokifanya kwanza ni kushirikiana na TAMISEMI kupeleka wataalamu wazoefu na hasa Wahandisi ili wasaidie kuandaa maandalizi. Kwa hiyo, nikubaliane na Mheshimiwa Rashid Mohamed .

Na. 97

### **Miradi ya Maji Vijijini**

**MHE. PASCAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mradi wa maji wa mtaro wa Ntomoko Wilayani Kondoa uliteuliwa na kuingizwa katika mradi wa maji na safi wa mazingira vijijini unaotekelizwa kwa fedha za Benki ya Dunia tangu mwaka wa Fedha 2005/2006; na kwa kuwa mradi huu haujaanza kutekelezwa hadi sasa:-

- (a) Je, ni kwa nini mpaka sasa mradi huo haujaanza kutekelezwa?

(b) Je, mradi huo sasa utaanza kutekelezwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Pascal Constantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 Halmashauri zote nchini ikiwemo ya Kondoa zilichagua vijiji 10 ambavyo vingeingizwa kwenye Programu ili viweze kupatiwa maji safi na salama.

Halmashauri ya Kondoa ilichagua kujenga miradi katika vijiji vingine vya Alema Kuu, Gonga, Olboti, Machiga, Kandala, Soera, Madisa Isongolo na Choka pamoja na ukarabati wa mradi wa Ntomoko. Utekelezaji wa programu Kitaifa unahitaji fedha nyingi. (*Makofi*)

Hivyo basi tangu mwaka 2005 hadi 2007 Serikali imekuwa ikishauriana na wafadhilli kuhusu Programu hii. Kutokana na mchakato huu kuchukua muda mrefu, utekelezaji wa programu kwa kila Halmashauri umechelewa kuanza tofauti na ilivyotarajiwa. (*Makofi*)

(b) Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kuwatafuta Washauri wa kuhamasisha jamii, usanifu na usimamizi wa miradi unaendelea katika Halmashauri zote nchini. Kazi hii inatarajiwa kukamilika mwezi Septemba, 2008 ambapo Wataalam Washauri wataanza kazi ya usanifu wa miradi.

Mradi wa Ntomoko unatarajiwa kuanza kutekelezwa mara baada ya kumalizika kwa usanifu wa ujenzi wa mradi huo ambaa utatekelezwa pamoja na ujenzi wa miradi nilioitaja awali.

**MHE. PASCAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Mradi wa Ntomoko ni wa

ukarabati na kwa kuwa umeharibika sana sasa hivi na hautoi huduma kabisa kwa vijiji vipatavyo kama 18 hawana maji kabisa. Je, Serikali itachukua hatua gani ya kuwanusu hao wananchi wa vijiji 18 ambao sasa wanapata adha kubwa ya maji?

Swali la pili; kwa kuwa hata mradi wa awamu ya kwanza wa Benki ya Dunia haujatekelezwa, kwa mfano katika Jimbo la Kondoa Kusini, Vijiji vya Kidoka, Umekwa, Chase na Hamia ambayo imefunguwa mashine na pampu lakini mashine hizo hazifanyi hizo kabisa je, Serikali ama Wizara itachukua hatua gani kwa mkandarasi ambaye hakutekeleza wajibu wake?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua zinazochukuliwa kama nilivyosema katika majibu mengine ni kwamba; hatua ni kuhakikisha kwamba tunaandaa hatua zote zinazotakiwa ili mradi wa Ntomoko nao uweze kutekelezwa nao chini ya programu hii. Lakini pamoja na hayo hatua za dharura ambazo tumekuwa tukizichukua kutokana na kucheleva kuanza na mradi huu ilikuwa ni pamoja na kutoa fedha za *quick wing* kwa ajili ya kuangalia kwamba miradi midogo midogo ambayo inaweza kurekebishwa haraka na kutoa matarajio itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kondoa kwa bahati mbaya mwaka 2006/2007 haikuweza kufuzu vigezo vilivyotakiwa kwa ajili ya kupata fedha za *quick wing* kwa hivyo mwaka huo haikupata. Lakini kwa mwaka huu bahati nzuri Kondoa napenda kuipongeza kwamba katika Wilaya 63 zilizofuzu yenye nayo imo. Kwa hivyo imeshaombewa *no objection*. Lakini niseme kwamba kwa kuwa bado hatujapokea fedha za quick wing kwa mwaka unaofuata niseme kwamba tutaendelea kuiangalia Kondoa na fedha zile zitakapotoka mara moja tutahakikisha kwamba tunazipeleka Kondoa kwa sababu tatizo hilo la Kondoa linafahamika.

Lakini kuhusu mashine ambazo hazifanyi kazi hilo ni jukumu letu mimi naomba kwamba suala hili Mheshimiwa Degera atufikishie tena kwa sababu ameshatuletea lakini Halmashauri ya Wilaya nayo ilikuwa haijatuambia kama kuna tatizo kubwa ambalo linataka Wizara kuingilia. Kwa hivyo namwahidi kwamba kwa kuwa nipo hapa Dodoma *Weekend* moja nitakwenda niangalie hali ilivyo na Serikali lazima itachukua hatua.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina swal moja la nyongeza, matatizo ya maji yaliyoko Wilaya ya Kondoa ni sawa na matatizo yaliyopo mji wa Kibondo na Kigoma Mjini. Kwa kuwa Mkoa wa Kigoma umejaliwa kuwa na vyanzo vingi vya maji ikiwemo Ziwa, Mito na vyanzo vingine vidogo vidogo vya maji. Lakini pamoja na vyanzo hivyo Mji wa Kibondo na Kigoma Mjini tatizo la maji limekuwa ni tatizo sugu. Je, Serikali inawaambia nini wananchi wa Mji wa Kibondo na Mji wa Kigoma kutokana na matatizo ya maji wanayoyapata na kutumia muda mwangi wa kutafuta maji badala ya kutumia muda kwa kufanya shughuli za kuinua uchumi wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, mimi ya Kigoma, Kibondo na matatizo ya maji mimi binafsi pia inanigusa nikiwa ni mdau na ninaelewa matatizo hayo na nimeshatembelea miji yote hiyo. Nimekagua hali ya maji

Kibondo, Kasulu na Kigoma. Tatizo moja ambalo ninaomba Waheshimiwa Wabunge tusaidiane na linagusa miji hiyo ni kwamba Serikali imekuwa inajitahidi kabisa kupeleka fedha za *quick wing* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba angalau huduma hiyo inawafikia wananchi katika miji hiyo hata kama sio asilimia mia moja.

Lakini jambo ambalo limekuwa likitokea ni kwamba wakati mwingine fedha hizo zimekuwa zikitumika tofauti na tulivyokusudia. Kwa hiyo ninachoomba ni kwamba Waheshimiwa Wabunge mnajua kabisa kwamba fedha zinapelekwa na kama nilivyoahidi huko nyuma ni kwamba kila tutakapopeleka fedha hata kama ni za *quick wing* lazima na nyie mjue. Mjui kusudi muweze kufuatilia maana tunapofika kuuliza kitu ambacho kimeshaharibika sasa inakuwa tena siyo kutibu inakuwa ni *post-mortem* tu sasa. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba tumeandaa watalaam wa kwenda kukagua nini kinafanyika katika miji hiyo kwa sababu tumepeleka fedha lakini hazifanani na kazi iliyokwishafanyika.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ukitiliza majibu yote ya Mheshimiwa Naibu Waziri tatizo linaonekana bado tunaongea na wafadhili. Mimi namwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie. Kwa nini sasa tusiamue fedha zile ambazo tulikuwa tunatumia kwenye mradi wa *Lake Victoria* zianze kutumika kupeleka maji kwenye Wilaya ya nchi hii kuliko kusubiri *donors* ambapo hatuna hakika maji tutapata lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mradi wa Kahama Shinyanga umekamilika pamoja na kwamba maji hayajaanza *ku-flow*. Serikali ilitumia takribani bilioni 250 katika mradi huu. Lakini haina maana kwamba wakati tunafanya mradi wa Kahama Shinyanga basi matatizo yote yamekwisha. Bado matatizo kama tulivyotoa kipaumbele kwenye mradi huu yapo vilevile kwa miradi mingine.

Kwa hiyo, tunapokea ushauri wa Mheshimiwa Serukamba kwamba Serikali iendelee kuelekeza fedha zake katika miradi mikubwa ya maendeleo hapa nchini. Kwa hiyo, ushauri huu tunaupokea lakini vilevile tuendelee na utaratibu wa kuomba hizo fedha za Benki ya Dunia na kama fedha hizo zitaleta matatizo basi bila shaka ushauri huu utatusaidia pia kwa sababu bado hakuna anayetuzuua kuangalia tufanye nini.

Na. 98

#### **Kuzingua Minara ya Simu za TTCL Tunduru**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Shirika la Simu la TTCL limejenga minara isiyopungua minne Wilayani Tunduru; na kwa kuwa minara hiyo imeshakamilika kwa zaidi ya mwaka sasa

lakini bado haijazinduliwa; na kwa kuwa Wilaya ya Tunduru inakabiliwa na matatizo makubwa ya mawasiliano ya *FAX, E-MAIL* na Simu:-

(a)Je, ni sababu zipi za msingi zilizofanya *TTCL* isizindue matumizi ya minara hiyo ikizingatiwa kuwa mamilioni ya pesa za Serikali yalitumika kujenga minara hiyo?

(b) Je, ni lini *TTCL* itazindua matumizi ya minara hiyo ili kumaliza tatizo la mawasiliano kwa wananchi wa Wilaya ya Tunduru?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ninapomwita Naibu Waziri Dr. Maua Daftari, naomba tumpe makofi mengi ya kumpa moyo kwa sababu ya mtihani aliopitia. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue dakika moja nichukue fursa hii kuwashukuru Ndugu zangu wapendwa wote walioshiriki katika mazishi na hitma ya Marehemu mume wangu wakiwemo viongozi wote wakuu, wastaaifu na wake zao. Nimefarijika sana kwa wote waliopata nafasi ya kunifariji kwa simu na kwa kuniona. Mola awape kheri zake na naishukuru sana familia yangu kwa kunisaidia na kuendelea kunifariji hadi leo. Namwomba Mwenyezi Mungu aijalie rehema roho ya Marehemu mume wangu malazi mema peponi amin.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo kwa niada ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mbunge wa Tunduru, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba kuna minara ya kampuni ya *TTCL* iliyoko Tunduru ambayo bado haijazinduliwa. Minara hiyo ilijengwa ili kufanikisha mawasiliano ya simu za mikononi za *TTCL* katika Wilaya hiyo. Hata hivyo, ili minara hiyo itumike inatakiwa kuwepo na mtambo wa *Transmission* ambao utakamilisha upatikanaji wa huduma. Kutowana na ukosefu wa fedha mtambo huo wa *transmission* bado haujajengwa. Ujenzi wa *transmission* unatarajiwaa kufanywa mwakani endapo *TTCL* itafanikiwa kupata mkopo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge msalieni mtume jamani! Hata hamumhurumi? Nitamruhusu Mheshimiwa Mtutura basi tu, inatosha. (*Makofi*)

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kwa kuwa *TTCL* ni Shirika la Umma; na kwa kuwa Tunduru iko mpakani mwa nchi yetu na Msumbiji ambapo inahitaji mawasiliano ya uhakika. Je, Serikali imejipanga vipi kuisaidia *TTCL* ili iweze kupata mkopo na kutatua tatizo la Tunduru?

Swali la pili. Swali hili ninahakika kabisa litahitaji maandalizi. Kwa hiyo, nitamwomba Mheshimiwa Waziri anipe kwa maandishi. Je, ni *transmission* ngapi zinahitajika katika kumaliza tatizo hili katika uzinduzi wa mitambo hii na kila *transmission* inagharimu shilingi ngapi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mtutura kwamba tayari majadiliano yanaendelea kati ya *TTCL* na Serikali kuona namna ya kuwapa Benki *guarantee* ili waweze kupata mkopo na kuweza kuendeleza huduma zao za mawasiliano ya simu tu na si kwa Tunduru tu lakini kwa nchi nzima.

Pili, napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba ili kuboresha mawasiliano Tunduru, *TTCL* kwanza ilipanga kuondoa mpango ule wa *analogue* na kuweka mtambo wa *digital* hivyo ilihitaji kujenga minara Namtumbo, Mchomoro, Milonde na Kilimasela ambayo tayari imekamilika isipokuwa ya Kilimasela tu *transmission* hiyo bado haijafanyika.

Ili kutengeneza *transmission link* ya gharama yake moja ni Dola milioni 1.6 lakini hizo nyingine anazohitaji yeche kama alivyosema Mheshimiwa nitahitaji kuchukua ili niweze kumpa *data* ipasavyo ni ngapi zitahitajika.

Lakini wakimaliza minara hii minne ikakamilika napena nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Tuduru itapata mawasiliano ya *TTCL* kwa kutumia teknolojia ya *CDM*.

Na. 99

### **Hitaji la Huduma ya Simu Mbina**

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO (K.n.y. MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa ni muda mrefu sasa tangu Shirika la *Celtel* limewekeana mikataba na kijiji cha Darpori Wilayani Mbina na mpaka sasa hakuna juhudzi za kupeleka mawasiliano ya simu maeneo haya:-

- (a) Je, ni lini Shirika hilo litaanza ujenzi wa minara ya simu maeneo hayo?
- (b) Kwa kuwa ni miaka miwili sasa tangu kampuni ya Tigo imejenga mnara eneo la Lituhi – Mbina bila kuanzisha mawasiliano. Je, ni lini huduma hiyo itaanza?

## **NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Capt. John Komba, Mbunge wa Mbinga Magharibi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Celtel* inaendelea kufanya tafiti za masoko katika maeneo mbalimbali Wilayani Mbinga. Kampuni hiyo itafikisha huduma za mawasiliano katika Kijiji cha Darpori Wilayani humo pamoja na maeneo ya jirani ifikapo Machi 2009. Aidha ni kweli kampuni ya Tigo tayari imekwishajenga mnara katika eneo la Lituhi, ingawa bado haujaanza kutumika. Mnara huo utaanza kutumika rasmi kuanzia Julai 2008.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudzi za Kampuni za *Celtel* na *Tigo*, kampuni ya *Vodacom* ina mpango wa kuanza ujenzi wa mnara wa mawasiliano katika kijiji cha Darpori, mtambo huu utawezesha kupatikana kwa mawasiliano katika kijiji cha Darpori na maeneo yote yaliyo jirani. Aidha kampuni hiyo iko katika hatua za awali za mchakato mzima wa kujenga mtambo wa mawasiliano katika eneo la Lituhi na matarajio ni kwamba mawasiliano yatapatikana mara tu baada ya mtambo huo kukamilika.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, napenda sana kuishukuru Serikali kwa juhudzi kubwa inayofanya kuhakikisha kwamba Wilaya ya Mbinga inapata mawasiliano kinyume na ilivyokuwa hapo awali. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kuwa msikivu kila pale ambapo tulimfuata au tumemwandikia na kuchukua hatua zinazopaswa. Swal moja la nyongeza, baada ya kufanya kazi hii nzuri ni lini sasa hizi kampuni pia zitafikiria kufanya mawasiliano yawe mazuri zaidi katika Kata za Litumbandyosi na Kata ya Ukata?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Napenda nikiri kwamba Kata alizozitaja sielewi kama zipo katika Jimbo lake au lipo katika Jimbo la Mbinga, jiografia kidogo imenipita. Lakini napenda nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge kwamba juhudzi zinafanywa na makampuni ya simu kufikisha mawasiliano katika maeneo yote nchini na nina hakika Waheshimiwa Wabunge watakubaliana nami kwamba kampuni za simu zimekuwa mkombozi mkubwa katika masuala mazima ya mawasiliano katika maeneo yetu.

Siku zote ninakuwa tayari kuwasaidia Waheshimiwa Wabunge katika masuala yao ya mawasiliano ya simu na nina ahidi kuendelea kuwapa msaada huo wakati wowote.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Maua Daftari, Mwenyezi Mungu azidi kukupa subira na nguvu za kuhimili yote. Tunahamia Wizara ya Nishati na madini swal linaulizwa na Mheshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo.

**Tanzania Inavyonufaika na Makampuni ya Gesi Asilia.**

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN NGWILIZI** aliuliza:-

Je, Tanzania inanufaika vipi kimapato kutohana na kuruhudu kampuni za *Songas* na *Artmas* kuchimba na kuuza gesi asilia ya Songo Songo na *Mnazi Bay*.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali al meshimiwa Brig. Gen. Hassan Ngwilizi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gesi asilia ya Songo Songo ilianza kuzalishwa mwezi Julai, 2004 na *Mnazi Bay* mwezi Desemba 2006. Mradi wa *Songas* wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ya Songo Songo pamoja na mradi wa *Mnazi Bay* unaondeshwa na *Artumas* ni kati ya miradi iliyobuniwa kitaifa kwa lengo la kuendeleza vyanzo vya gesi ya Songo Songo na *Mnazi Bay*.

Mheshimiwa Spika, kuanzia mwezi Julai mwaka 2004 nchi yetu ilianza kutumia gesi asilia inayozalishwa kisiwani Songo Songo Mkoani Lindi katika mitambo minne ya kuzalishia umeme na viwanda kumi na tisa. Gesi asilia ya *Mnazi Bay* Mkoani Mtwara inatumika kuzalisha umeme unaotumika katika Mikoa ya Lindi na Mtwara.

Faida iliyopatikana kutohana na kugunduliwa kwa rasilimali hii katika nchi yetu ni pamoja na kuongeza rasilimali ya nishati kwa ajili ya matumizi katika uchumi wetu hasa wakati huu ambapo gharama za mafuta ya petroli katika soko la dunia inazidi kupanda. (*Makofsi*)

Kwa mfano matumizi ya gesi asilia katika viwanda 19 jijini Dar es Salaam zimeokoa gharama kubwa za matumizi ya mafuta ambayo huagizwa nje ya nchi, zimepunguza gharama za uzalishaji wa umeme, zimeongeza ajira kwenye miradi hiyo na miradi hii imeshiriki katika kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, kampuni ya Artumas inazalisha Megawati 5 za umeme kwa ajili ya matumizi ya Mtwara na Lindi matarajio ni kuzalisha zaidi ya Megawati 6 baada ya kukamilika kwa mikataba ya mradi na ujenzi wa miundombinu ya kusafirishia umeme. Kampuni ya Songas imekamilisha mradi wa umeme kisiwani Songo Songo ambapo nyumba 110 zimeunganishiwa umeme. Kwa upande wa ajira kampuni ya *Artumas* ina waajiriwa wa kudumu zaidi ya 60 na waajiriwa wa muda ni zaidi ya 100. *Songas* wameajiri wafanyakazi wa kudumu 70, kati ya hao 65 ni Watanzania na kazi za muda wameajiriwa wafanyakazi 100.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa huduma za jamii *Songas* imetekeleza miradi ya maji safi na upanuzi wa Zahanati kisiwani Songo Songo. Vilevile visima vya maji 42 vimechimbwa katika vijiji vilivyo katika eneo la mradi Wilayani Kilwa, Rufiji na Mkuranga. Ujenzi wa miundombinu ya barabara, umeme na maji umefanyika Salasala na Kinyerezi mkoani Dar es Salaam.

Kampuni ya *Songas* pia imechangia katika ujenzi wa Shule za Sekondari za Tambani na Kinjumbi na shule za msingi Njopeka, Kilimani, Chamazi na Tungi. Kampuni ya *Artumas* imechangia ujenzi wa hosteli na madarasa katika shule ya sekondari Msimbati na shule moja ya sekondari katika Mkoa wa Lindi. Aidha Kampuni imeanzisha mradi wa shamba la mfano kwa wakulima wa kijiji cha Mchepa.

Mheshimiwa Spika, teknolojia mpya ya uzalishaji na usafirishaji wa gesi asilia imeingizwa nchini, ambapo kampuni za gesi zimetoa mafunzo kazini kwa watumishi wake kwenye nyanja za usafishaji gesi asilia (*Natural gas Processing*) na uzalishaji umeme.

Vilevile Watanzania wamepata uzoefu na utaalam katika fani mbalimbali kama vile za fedha, uendeshaji, utawala na biashara. *Songas* wametenga kiasi cha fedha katika Bajeti yao kwa ajili ya kusomesha wafanyakazi zaidi katika kuendeleza fani zao. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, tathimini za kitaalamu zilizofanywa kwa kuzingatia vigezo vya faida kiuchumi na kijamii zilizotokana na matumizi ya Gesi Asilia zinaonyesha kwamba hadi kufikia Desemba 2007 Taifa limeokoa Dola za Marekani milioni 994.1 ambazo zingetumika kuagiza mafuta kwa ajili ya mitambo hiyo. Kati ya kiasi hicho Dola za Marekani 992 zilizotokana na mradi wa Songo Songo na kiasi kilichobaki cha Dola za Marekani 201 zilizotokana na mradi wa Mnazi Bay. Kwa mradi wa Songo Songo mapato yaliyopatikana kwa kipindi cha Julai 2004 hadi Desemba 2007 ni Dola za Marekani milioni 30.3 ambazo zimewasilishwa mfuko mkuu wa Hazina.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri. Nashukuru kwa takwimu alizotupa kwamba taifa limeweza kuokoa dola za kimarekani milioni 994.1. Mimi nilikuwa nafikiria kwamba huenda hizi zinge-reflect katika kupungua kwa bei ya umeme. Lakini hata hivyo naomba kuuliza maswalia mawili madogo ya nyongeza. Kwa vile bei ya mafuta inazidi kupanda katika soko la dunia na sasa hivi upo utaalam wa kugeuza gesi hii kuwea kutumika katika magari na mitambo. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuwa na mitambo hiyo ili Tanzania iweze kutumia gesi ilionayo kwa ajili ya kuendeshea magari na mitambo?

Swali la pili, kwa vile bei ya gesi hazikupanda na wakati tunatiliana na mikataba kampuni za *Songas* na *Artumas* bei ilikuwa ni chini. Je, ongezeko la bei ya gesi Tanzania inanufaika nalo vipi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba bei za mafuta zinazidi kupanda na ninaomba niseme kwamba tayari Wizara ya Nishati na Madini imeanza kuwasiliana na wawekezaji mbalimbali kuangalia matumizi ya gesi jinsi yatakavyoweza kutumika katika magari lakini pia kutumika majumbani.

Huu ni uwekezaji mkubwa unataka utaalam mkubwa na mpaka sasa hivi upembuzi yakinifu umeshafanywa kutoka kwa wataalam wa China na ni lengo la Wizara kwamba tutaa ngalia yale maeneo makubwa na maeneo *specific* kama vile Hospitali, usafiri wa umma katika matumizi ya gesi hii kwa muda halafu baadaye matumizi haya yatakwenda mpaka kuingia majumbani kwa watu hasa katika mfumo wa mbadala wa mafuta ya petroli lakini pia kama mbadala wa kuni majumbani.

Na. 101

### **Mashamba ya Wananchi yenyne Madini**

#### **MHE. TEDDY LOUISE KASELA-BANTU aliuliza:-**

Kwa kuwa ardhi hiyo ambayo ni mashamba na matongo ya wazawa na kwa kuwa sehemu kubwa ya Tanzania mfano Kanda ya Ziwa, Tabora ikiwemo Bukene kuna madini kama almasi na dhahabu. Je, Serikali inawasaidiaje wananchi waliokumbwa/au kukutwa na hali ambayo kuna madini kwenye mashamba na makazi yao na hivyo, kuhamishwa kwa madhumuni ya kupisha mgodi:-

- (a) Kwa kuwa mikataba hutiwa saini na Serikali bila wananchi kuelewa kinachoendelea, ili kuwasaidia wananchi wetu. Je, Serikali inafanyaje hasa wakati wa mwanzo pale haijafikia hali ya kuwa mgodi kama ilivyo sasa pale Itanana na Mahene Jimbo la Bukene?
- (b) Je, Serikali haioni ni haki kuweka kipengele kidogo kwamba anayekutwa hapo alipwe angalau asilimia moja au mbili ya mapato yanayopatikana ili wananchi wanaokaa kwenye maeneo hayo wapate maendeleo na maisha bora au kuwezesha il wajikwamue ki-uchumi?

#### **NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Louise Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Madini hupatikana ardhini katika maeneo mbalimbali yakiwemo mashamba na makazi ya watu. Kulingana na sheria ya madini ya mwaka 1998 kifungu namba 5

kinasema madini kama ilivyo maliasili nyingine humiliikiwa na kusimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, inapotokea wananchi wakagundua kuwa kwenye mashamba au makazi yao kuna madini wanashauriwa kufika kwenye Ofisi ya Madini iliyo karibu nao ili kupata maelekezo ya taratibu za kupata *Primary Prospecting Licence* kwa ajili ya utafutaji wa madini, au *Primary Mining Licence* kwa ajili ya kuchimba madini endapo eneo hilo halitakuwa limetolewa kwa kampuni au mtu mwngine.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Madini ya mwaka 1998 kifungu cha 38 kwa upande wa *Special Mining Licence* au kifungu cha 64 cha sheria hiyo hiyo kwa upande wa *Mining Licence*, inamtaka mwekezaji kabla ya kupewa leseni ya uchimbaji madini kufanya tathmini ya athari za mazingira na kijamii zitakazotokana na shughuli za uchimbaji. Tathimini hizi hujumuisha pia maoni ya wananchi waliopo katika eneo linalotarajiwa kuanzhishwa mgodi. Ikiwa katika kufanya maamuzi mwekezaji anaamua kufanya uwekezaji ambao utaathiri makazi na mashamba ya wakazi, baada ya kupata leseni, Mwekezaji huyo anawajibika kufanya taratibu stahili za kuwahamisha wananchi, kwa kuandaa na kulipia masuala ya fidia kwa kushirikiana na viongozi wa maeneo hayo wa ngazi mbalimbali. Wananchi watahama ili kupisha uwekezaji baada ya sheria za nchi kuzingatiwa, ikiwemo ya kufuatwa kwa taratibu zote za malipo ya fidia.

Sio sahihi kusema kwamba mikataba hutiwa saini na Serikali bila wananchi kuelewa kinachoendelea. Serikali yenewe ni ya Watanzania, na hufanya kazi zake kwa niaba ya wananchi. Utaratibu wa utengenezaji mikataba duniani kote ndiyo ulivyo. Hufanywa kwa usiri wa kiwango Fulani ili kulinda taarifa za kibashara za mwekezaji dhidi ya wawekezaji wenzake (*confidentiality clause*). Katika uingiaji wa mikataba hii ni Serikali yenye jukumu la kulinda maslahi ya wananchi. Wananchi wa maeneo yenye madini hunufaika kwa huduma za kijamii na kiuchumi ambazo hugharamiwa na Serikali katika taratibu za kawaida za kugharamia shughuli za maendeleo na pia kutegemeana na makubaliano ya awali yaliyopo baina ya mwekezaji na Serikali, Mwekezaji huingiza kwenye makubaliano ya mkataba kugharamia shughuli mbalimbali zenyne mwelekeo wa maendeleo ya ustawi wa jamii. Ajira na huduma zitolewazo na wananchi waishio jirani na maeneo ya madini pia hunufaisha wakazi wa maeneo hayo na huwa sehemu ya makubaliano hayo.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Ahsante kwa kunipa nafasi finyu ya kuuliza swali la nyongeza na nikiwa wa kwanza kuanza hivyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kuwa na mimi nafahamu nilikuwa mmoja wa walipitisha Sheria hiyo ya mwaka 1998 sina ubishi na hilo. Ila nauliza hawa wananchi wa Itanana walipokuwa wanaingia kwenye mkataba ni baada ya kulalamika lakini kwanza huyu mwekezaji alikuja kiubabe tu na wakaweka mkataba wa miezi 18 ambao unaanza Julai 2007 na kuisha Desemba mwaka huu. Jana nimepata barua kwenye ofisi yangu kwamba wanalipwa haki yao. Je, Desemba kama hajamaliza kazi yake ya *Research* wanaandika mkataba mwngine mpya au unaendelea huo huo kwa bei hiyo au kuna nyongeza kwa sababu kuna madiliko mengi ya fedha kudidimia?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tedddy Kasela- Bantu Mbunge wa Bukene swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utafiti unaoendelea Itanana ni utafiti wa Almasi unafanywa na kampuni ya KIMBRAY ni utafiti ambao katika viwango vya utafiti ni utafiti mkubwa

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu juzi taratibu za kutoa leseni katika Wizara yetu ni kwamba leseni ikishatolewa lazima taarifa iende Mkoani kwenye ofisi yetu ya Mkoa, na kwa maana hiyo ni lazima taarifa ziende kwenye ngazi zote husika za utawala wa Mkoa Wilaya, mpaka Kijiji.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mama yangu Teddy Kasela- Bantu kwamba hatuna ushahidi wa kwamba taarifa hazikufika, labda kumekuwa na matatizo kidogo hapo katika kupeana taarifa lakini barua zipo zinazoonesha kwamba taarifa zimekwenda Mkoani na zimesainiwa na mamlaka ya Mkoa na Wilaya ya kuwapa taarifa wahusika kwenye maeneo hayo kwamba kuna uwekezaji wa namna hiyo unakuja.

Mheshimiwa Spika, kusema kweli si uwekezaji ni shughuli za utafiti, swali lake la pili kwamba utafiti huo kama utakuwa umekamilika Disemba, tumekuwa tukitoa leseni kwa kipindi Fulani na baada ya kipindi hicho leseni hii ya *prospecting*, Mtafiti kwa maana ya mwekezaji wa baadaye atakapokuja atatutamkia Wizarani kwamba amefikia wapi kwenye utafiti wake na lengo lake, je ni la kuendeleza utafiti kama muda huo upo au kuanza na uwekezaji, akifikia tathmini hiyo na sisi Wizarani tunaifanya kazi na tunatoa leseni kama inavyostahili.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge ingawa muda wa maswali umekwisha lakini nisingependa kuyaacha haya maswali ya Wizara ya Fedha. Maswali ni mengi sana kwa hiyo tutatumia dakika chache kwa ajili hiyo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Kwamtipura.

Na. 102

### **Matumizi ya Dola ya Marekani Nchini**

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID** aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na tabia ya baadhi ya wafanya biashara nchini na wamiliki wa hoteli kubwa kutoa huduma kwa kuwauzia wananchi kwa thamani ya dola ya Marekani (*USD*):-

- (a) Je, Serikali ina taarifa kuwa utaratibu huo unaendelea nchini?

(b) Je, Serikali inawaeleza nini wananchi juu ya utaratibu huo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Mbunge wa Jimbo la Kwamtipura, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia kwa makini hoja za mara kwa mara za Waheshimiwa Wabunge na wananchi kuhusu suala la matumizi ya fedha za kigeni katika malipo ya ndani na athari zake kwa uchumi; na kwa kuzingatia sheria ya usimamizi wa fedha za kigeni ya mwaka 1992(*The Foreign Exchange Act, 1992*) na kanuni za uendeshaji wa maduka ya fedha za kigeni ya mwaka 1999 (*Bureaus de Change Regulations 1999*), Serikali mwezi wa Augosti, 2007 ilitoa tamko Bungeni kuhusu matumizi ya fedha za kigeni kulipia bidhaa na huduma katika soko la ndani. Tamko hili pia lilianisha dhana ya (*dollarisation*) sababu za kuwepo kwake na athari zake kwa uchumi, katika tamko hilo, Serikali iliagiza yafuatayo:-

(i) Gharama na bei kote nchini zitangazwe kwa fedha ya Tanzania yaani shilingi ya Tanzania.

(ii) Kwa bidhaa na huduma zinazowalenga watalii au wateja wasio wakazi wa Tanzania, matangazo ya bei yanaweza yakawekwa kwa shilingi ya Tanzania na fedha za nje na malipo kupokelewa kwa fedha ambayo mlipaji atakuwa nayo.

(iii) Viwango vya kubadilisha fedha vitakavyotumika katika kuweka bei, kama ilivyolezwa kwenye kipengele (ii) cha jibu viwekwe na visizidi vile vya soko.

(iv) Mkazi yejote wa Tanzania asilazimishwe kulipia bidhaa au huduma yoyote hapa nchini kwa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kufuatia tamko hili, Serikali ilitarajia kuwa wafanyabiashara wote nchini na wananchi wangefuata na kutekeleza maamuzi haya ya Serikali. baada ya kutolewa kwa tamko hilo, Serikali inazo taarifa kuhusu ukiukwaji wa agizo hili.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilitoa tamko kuhusu suala hili na kwa kuzingatia sheria na kanuni za fedha za kigeni, ni kinyume na sheria na pia ukiukwaji wa maamuzi ya Serikali kwa wafanya biashara na wananchi kuendelea kukaidi utekelezaji wa maamuzi haya. Serikali inarudia tamko hili leo na kuwataka wananchi na wafanyabiashara kote nchini, kutambua kuwa shilingi ya Tanzania ndiyo fedha halali kwa malipo yejote nchini.

**MHE. MOHAMMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza, hivi ni kwa nini Serikali isiweke

utaratibu wa makusudi, kwamba mgeni yeote anayeingia nchini aidha anapitia bandari yeote ya Air port au bandari ya kuingilia katika nchi, asibadilishe pesa zake kwa pesa za Tanzania ili Serikali ipate pesa za kigeni.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Rished Abdallah, kama ifuatavyo:-

Wageni wanapokuja nchini tunategemea kwamba watakuja na fedha na za kigeni, iwe *dollar*, iwe *Euro*, ama *YEN*. Tunategemea kwamba ama watabadilishia benki ama kwenye maduka yaliyo na *lisence* ya kubadilisha fedha au pale hotelini wanapokaa, hatutarajii kwamba watabadilishia barabarani. Vile vile hatutarajii kwamba wanapoingia pale bandarini ama uwanja wa ndege pale watabadilisha fedha zao isipokuwa kama kuna hayo maduka ya kubadilisha fedha, tunawakaribisha waje na fedha hizo za kigeni.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Nashukuru Mheshimiwa Spika kwa kuniona, nina swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa maduka ya kigeni yamekuwa yakikataa zile noti za Marekani zenyne vichwa vidogo na kule Marekani zinapokelewa. Je, Serikali inasema nini kuhusu hili?

**SPIKA:** Nadhani picha zake zile ndogo za wale Marais na vingine.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. JEREMIAH S. SUMARI):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi naomba nijibu swali la Mheshimiwa Lucy Owenya kama ifuatavyo:-

Kukataliwa kwa fedha hizi zenyne picha ndogo na maduka ya kubadilisha fedha mara nyingi ni kwa sababu mashine wanazotumia kuhakiki zile fedha zimebadilika na kwa hiyo hazitambui zile fedha za zamani. Lakini dola ya Marekani kwa sera zao haifi inaendelea mpaka inaporudi kwao halafu wanateketeza, lakini bado ni fedha halali za Kimarekani ingawa si fedha halali hapa nchini.

Na. 103

#### **Huduma za Benki Mkoa wa Kaskazini Pemba**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba ni mashuhuri sana katika shughuli za kilimo na biashara; na kwa kuwa tasisi za fedha zikiwemo benki ni kiungo

muhimu sana cha kuwezesha wananchi kujipatia mikopo itakayowasaidia kujikwamua na umaskini; na kwa kuwa Mkoa huo hauna hata taasisi moja ya kibenki na hivyo kudumaza shughuli za kiuchumi na kijamii:-

- (a) Je, Serikali haioni kuwa inawasababishia wananchi hao usumbufu wa kufuata huduma ya benki Mkoa wa jirani?
- (b) Je, Serikali itatumia utaratibu upi utakaowawezesha wananchi wa Mkoa huo kupata huduma ya mkopo wa Fedha za JK bila usumbufu wowote?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziriwa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Jimbo la Wete, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa wananchi wa kupata huduma za kibenki karibu na maeneo yao pamoja na msaada wa taasisi hizo kwa wananchi katika kujikwamua kiuchumi. kufuatia mageuzi ya kiuchumi katika sekta ya fedha yaliyofanyika nchini, Serikali imejitoa katika uendeshaji wa moja kwa moja wa biashara za kibenki na fedha nchini.

Jukumu la kuanzisha biashara ya benki ni la sekta binafsi pamoja na wananchi, hata hivyo, Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya kiuchumi nchini ili kuiwezesha sekta binafsi kuanzisha vyombo vya fedha na kutoa huduma zinazohitajiwa na wananchi. Pia Serikali itaendelea kuhamasisha benki binafsi kupanua shughuli zao ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kufika Mkoa wa Kaskazini Pemba.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika mpango wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi, imeainisha Benki tatu yaani, *National Microfinance Bank (NMB)* Benki ya Wananchi wa Zanzibar (*PBZ*) na Benki ya Posta ya Tanzania kushiriki katika mpango wa mikopo ya uwezeshaji na kukuza ajira kwa wananchi. Kwa kuwa kila Mkoa umetengewa kiasi chake cha fedha, ni dhahiri kwamba fedha hizi zitawanufaisha wananchi wa Mkoa husika.

Hata hivyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na uongozi wa Mkoa ili kuelewa utaratibu mzima utakaotumika kwa lengo la kunufaisha upatikanaji wa mikopo kwa wananchi wa Kaskazini Pemba, bila ya usumbufu.

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na kwamba Serikali imejitoa katika biashara ya Kibenki, lakini nafahamu kwamba Serikali ina hisa katika mabenki ya *CRDB*,

*NMB* na *NBC* ni kwa nini Serikali haitumii nafasi yake kama ina hisa kuishauri benki hizi kufungua matawi Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali ina hisa katika benki ya *NMB* na *CRDB* na hiyo ndiyo kazi yetu sisi kama Serikali kuzishawishi benki hizi kwenda kufungua matawi katika maeneo ambayo kibashara yanaonekana yamekua na ukweli ni kwamba benki hizo zinafanya kazi hiyo. Panapo majaliwa pengine watafika katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *Peoples Bank of Zanzibar* ilikuwa na *Branch* Wete na mimi niliwahi kuwa *incharge* wa *branch* hiyo miaka ya 1970 na kwa kuwa *NMB* imeweza kubaki hai kwa sababu imelelewa na benki kuu mpaka ikawa hai. Ni sababu zipi benki kuu iliyoifanya mpaka *Peoples Bank* ikafa wakati 1978 mimi nilikuwa *incharge* na ilikuwa ikifanya vizuri Mkoa huohuo wa Kaskazini ambao leo hakuna benki.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nataka nianze kwa kusema kwamba *PBZ* hajifa, *PBZ* ipo na inaendelea kuwepo, kilichojojiteza hapa, mimi nilikuwa ni mmoja wa wataalam ambao tuliwekwa pale na Serikali mbili kuiangalia *PBZ*, kilichofanyika ni kwamba *PBZ* ilihitajiwa kufanyiwa *restructure*. Kwa maana hiyo tulilazimika kutoa mapendekezo mengi, moja ni kupunguza wafanyakazi wa *PBZ* ili iweze kujiendesha kibashara. Benki ile ndugu zangu ilikuwa na wafanyakazi wengi kuliko benki nyingine yeoyote. Tulilazimika vilevile kufunga baadhi ya matawi ya benki ile ili sasa benki ile iweze kujiendesha kibashara. Benki ile ililazimika vilevile kuwa *computerized* kwa sababu ilikuwa inafanya kazi zake *manually* na yote ilihitajika kuwa na mtaji mkubwa zaidi ili kuweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo tulilazimika kutoa ushauri huo kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na *BOT* na wakakubaliana na sisi kwa ushauri ule. Kwa hivyo sasa hivi *PBZ* inafanya kazi zake kama Benki nyingine za kawaida zilizopo hapa nchini. (*Makofi*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge muda wetu wa maswali umepita, sasa ni matangazo.

Waheshimiwa Wabunge nimepokea hapa kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabungekumba Wizara ya Maji na Umwagiliaji, itupatie orodha ya Wilaya zilizofaulu

kupata fedha za ule mradi wa *Quick wing*, imekuwa ikitamkwa tamkwa sana, nimeliafiki wazo hili na ningeomba Serikali itusaidie tuipate hiyo orodha ili Wabunge waweze kuifanyia kazi.

Waheshimiwa Wabunge, kule ambako hawakufaulu itasaidia kwa sababu utajua mahali pa kuuliza kwa nini Wilaya haikufaulu na pengine kusaidia kuharakisha utekelezaji wa mradi muhimu sana huu.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wetu kwanza ni Bwana *Hans Ratshildars*, ni *First Secretary, Embassy of the Kingdom of the Netherlands in Tanzania* sijui yupo naona kama hakuja. Halafu kuna Mama *Lina Soiri*, yeye ni *Counselor of the Embassy of Finland* na yeye pia hayupo, basi labda ni kesho.

Wageni wa Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba ni kama ifuatavyo: Sheik Hussein kutoka Katoro Geita, ahsante sana na karibu sana na David Azaria naona ni yule pale karibu sana. Wapo wanachuo 35 wa Udaktari wa Binadamu kutoka chuo Kikuu cha Kumbukumbu Herbert Kairuki Mikocheni. Tunao kundi jingine la wanafunzi 50 kutoka shule ya Sekondari Jamhuri hapa Dodoma, jana tulikuwa na kundi jingine leo tuna kundi jingine leo tuna kundi jingine pamoja na Walimu naomba wasimame, karibuni sana vijana wetu pamoja na Walimu sisi Wabunge tunawatakiwa mafanikio katika masomo, mfanye kazi kwa bidii, tunao pia wanafunzi watano kutoka shule ya sekondari Dodoma, karibuni sana na ninyi pia tunawataki mema katika masomo.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Gideon Cheyo Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji ameomba niwatangazie wajumbe wote wa Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuwa kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo saa saba mchana ukumbi namba 227.

Mheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Omar Kwaang'w Mwenyekiti wa Kamati ya huduma za Jamii, anahitaji wajumbe wote wa Kamati ya Huduma za Jamii wakutane leo saa tano asubuhi ukumbi 219.

Mheshimiwa Jenister Mhagama, Mwenyekiti, wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii anahitaji wajumbe wake mkutano saa tano katika ukumbi namba 231 jengo la Utawala.

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma kwa Wabunge anaomba wajumbe wote wa Kamati ya Tafrija, wakutane leo mara baada ya kuahirishwa Bunge. Nadhani ni jioni, tumekuwa na jioni ambazo hazikuchangamka. Kwa hiyo, Kamati hii ichangamke ili tuweze kuona tofauti kidogo. Kazi ya kupitia Makadirio ni ngumu sana. Kwa hiyo, *weekend* ni lazima ziwe na burudani, na huu ndiyo mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2008/2009  
Ofisi ya Waziri Mkuu na Tawala za Mikoa na  
Serikali za Mitaa**

(*Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge orodha yangu bado inawachangiaji watarajiwa 73, lakini wengi watasikitika tu kwa sababu haitawezekana. Pale ofisini tumetafakari hili jambo tumeona kwamba tutoe siku ya Ijumaa yote kwa majibu kutokana na uzito wa hotuba hii, kuanzia asubuhi kadri watakavyopangana wanaomsikiliza Waziri Mkuu.

Ofisi hii ya Waziri Mkuu ina vifungu vingi sana. Kwa hiyo hakuna nafasi ya kuchangia siku ya Ijumaa, ni leo na kesho tu, na kwa hesabu zetu huwa tunafikia kiasi cha Waheshimiwa kama 44 kwa hiyo kwa 73 ni dhahiri kutakuwa wengine wataachwa. Nawasihi mvumilie hali hiyo, wale amba pengine walikuwa na hoja mahususi katika Wizara tutawapa kipaumbele katika sekta zinazohusika kwa sababu rekodi ipo tutatoa kipaumbele kwa Wizara zinazofuata.

Waheshimiwa Wabunge, ili kuelewa nitaomba niwataje Wabunge nane wa mwanzo kwa asubuhi hii ya leo.

Nitaanza na Mheshimiwa Hassan Rajab Khatibu, Mheshimiwa Jacob Shibili, Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelili, Mheshimiwa Al Haji Mohamed Misanga, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Aziza Suleim Ally, Mheshimiwa Said Juma Nkumba na Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, namwita sasa Mheshimiwa Hassan Rajab Khatibu.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwanza kukushukuru wewe kwa kunipa heshima hii leo kuwa mchangiaji wa kwanza.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hasa Mheshimiwa Rais Aman Abeid Karume, Waziri Kiongozi, Shirika la Umeme Zanzibar, *TANESCO* kwa kurejesha umeme wake wa kawaida Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mimi nasema hili kwa sababu baada ya kupata matatizo yale kuna watu wasioitakia mema Zanzibar walizungumza mambo mengi sana, walisema kwamba umeme ule hauji tena hadi mwakani. Lakini tunashukuru kwa hekima na busara ya viongozi wetu wameturejeshea umeme kwa kipindi kifupi. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, lakini niseme tu kwamba umeme si kitu cha kutegemea sana, ni lazima Zanzibar tujipange vizuri na tuiwekee akiba yetu wakati wowote inapotokea tatizo la umeme kuwe na kitu cha dharura cha kusaidia ili kuweza kuleta Maendeleo Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa shukrani hizo sasa nianze shughuli yangu niliyokusudia leo. Kwanza nimpongeze Waziri Mkuu, Mawaziri wake wote wawili na *Comrade* Naibu Waziri Mwanri Katibu Mkuu na Maofisa wake wote kwa hotuba nzuri kabisa iliyokidhi kina ya ilani yetu ya *CCM*. Hongereni sana. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Spika, nishukuru tena kwamba Tanzania imeweza kabisa kupata fedha za matumizi yake ya ndani, kwa vile matumizi yetu yote ya ndani Mishahara na mambo mengine, hiyo itakwenda kulingana na fedha zetu bila kutegemea taasisi nyingine ya nje nayo nawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, ni lazima Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tujipange vizuri ili hii Bajeti tegemezi ninavyohisi mimi huko tunapokwenda wafadhalii wetu wametuchangia nahisi kwamba watakuwa wamechoka. Ninasema hivyo kwa sababu miradi yetu mingi ya Maendeleo huwa inakawia sana kutekelezwa kwa sababu ya kuchukua muda wa kuleta fedha ambazo tunazikusudia zinazotoka kwa wafadhilli wetu. Ningeshauri kwamba utaratibu huu tujipange ni lazima Bajeti yetu tujitegemee wenyewe na uwezo huo upo.

Mheshimiwa Spika, hili si jambo geni wenzetu Kenya wanajitegemea na nina amini vyanzo vya mapato katika nchi yetu vya kuweza kujihimili tunavyo sawasawa, nitaanza na bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, niipongeze *TRA* kwa namna inavyokusanya fedha, inakusanya vizuri lakini tatizo moja ambalo inaweza kukusanya zaidi ya bilioni 2 kwa mwezi kama itakuwa haina urasimu kama ilivyo hivi sasa, *TRA* kidogo kuna urasimu utaratibu wa bandarini pale haujaka vizuri meli zinazoleta bidhaa kutoka nje zinachukua muda kuteremsha mpaka zinaondoka kwenda sehemu nyingine na tunakosa mapato na hilo ni moja katika sehemu inayoweza kutupatia mapato makubwa sana katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, mimi ningeshauri Serikali kwamba bandari ya Dar es Salaam ijipange vizuri na iweke vitendea kazi vizuri, utaratibu mzuri, kusiwe na urasimu wa kutoa ushuru, na wanaotaka kutoa mizigo yao ninaamini kwamba tutapata fedha zaidi na hii billions wanazokusanya kwa mwezi ninaamini wanaweza kukusanya zaidi ya bilioni 4 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, ninchotaka kuzungumza sasa hivi ni shughuli za utalii. Utalii ni moja kati ya chombo kikubwa kinachowenza kutusaidia mapato sana katika nchi hii, na utalii katika nchi za wenzetu nafikiri hata Seychelles uchumi wao wote na shughuli zao wanazoendesha katika Serikali inatokana na utalii. Ningelishauri serikali fedha zinazotengwa kwa shughuli za utalii ni finyu mno na kama tumejipanga vizuri tukaipa fedha idara ya utalii, ikajitangaza katika mataifa mbalimbali watalii wataingia kwa nguvu sana hapa. (*Makofi*)

Nchini Tanzania kwa sababu ina vivutio vizuri, ina wanyama wazuri, ina *beaches* nzuri, kama kule Kusini kuna sehemu moja wanaita Msimbati ambayo *Whitesands* ni safi sana, kule Matemwe Kaskazini ambazo hizo watalii wanaweza kuingia vizuri kabisa

kama tutafuata utaratibu mzuri tukaingiza fedha na taasisi hii ikaweza kuwa ya pili katika kutoa pato la Taifa katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema ukitaka fedha ni lazima utoe fedha, Serikali ipeni hii idara ya utalii ijitangaze, waje watalii watatusaidia sana katika kuinua uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu ina rasilimali nyingi sana, tutafute mbinu za kujitegemea na uwezo wa kujitegemea katika nchi hii, tunao. Katika nchi hii, tuna rasilimali nyingi sana kwa mfano dhahabu, almasi, petroli, gesi, makaa ya mawe, chuma, jamani, umaskini unatoka wapi? Kwa nini tusijitegmee? Kwa nini mpaka sasa tunazitegemea nchi za nje na kusababisha mambo yetu hayaendi vizuri kwa sababu fedha haziji kwa mpangilio wakati uchumi wote huo tunao?

Mheshimiwa Spika, mimi ninaamini kwamba huko tunakokwenda lazima tujipange vizuri na tujitegemee wenyewe. Wafadhalii wetu hawa, ninahisi huko mbele tunakokwenda, watakuwa wanachoka na mambo yetu tunayopanga, hayatakwenda vizuri, kwa suala hili lazima tujiweke vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa ninaingia kwenye kilimo ambacho tunasema ni uti wa mgongo wa nchi hii lakini Serikali hatujajipanga, tunazungumza maneno tu. Ukulima... (*Makofi*)

Nyie pigeni makofi lakini hiyo ndiyo kazi ya CCM, nyie pigeni makofi lakini hiyo ndiyo hali halisi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa utaratibu wa kuweka ruzuku katika mbolea.

Pigeni makofi sasa na hiyo ndiyo kazi ya CCM. Imeweka utaratibu mzuri wa kuagizia matrekta, imefanya Serikali ya CCM, *CUF* pigeni makofi, huo ndio ushauri wa CCM. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, ongea na Spika.

**MHE. HASSAN RAJAB KHATIB:** Mheshimiwa Spika, ninaongea na Spika.

Mheshimiwa Spika, sasa ninasema, kazi sasa ni kujielekeza zaidi kwenye kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, nimebahatika kuwa Uchina, kuna kisiwa kimoja kinaitwa Ganzoo, wanafanya *irrigation* kule ambapo kwa eka moja wanatoa gunia 70 za mpunga na wanalima mpungu mara tatu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, sasa tujikite huko, tugeuze hali ya kilimo chetu kwa sababu maji tunayo, mabonde tunayo, maziwa tunayo, mito tunayo, ardhi nzuri tunayo, wataalamu tunao, nini sasa? Tukijikita katika sehemu ya umwagiliaji, naamini tutajinasua kabisa na tatizo la chakula.

Mheshimiwa Spika, nataka niipongeze kidogo *TBC*. *TBC* inafanya kazi nzuri sana na ninawapongeza sana kuanzia mwenyewe Waziri na Naibu Waziri wake na wataalamu wake wote na Mkurugenzi. Radio hii inafanya kazi vizuri lakini sasa kuna baadhi ya sehemu bado haijasikika. Sasa Serikali ijithahidi nako huko ifike ili na wao wanufaikie na radio hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka kuzungumza habari ya utafiti wa petroli. Hili suala tumezungumza kwa muda mrefu sana kwamba kuna petroli na bahati nzuri katika *speech* yako, Mheshimiwa Waziri Mkuu, umesema mmeshaangalia ni namna gani ya kugawana mapato lakini tunaanza lini kuchimba hii petroli? Tatizo hasa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni nini? Ulimwengu mzima sasa hivi kila kitu kimeharibika, bei za vyakula ziko juu kutokana na petroli na wakati huo tunasema hapa nchi kwetu *petrol* tunayo, ni nini kimekuwa kizito, hatujaweza kuyachimba mafuta hayo ili na sisi angalau tukajinasua kiuchumi katika nchi yetu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakwenda rafu ili nisije kugongewa kengele ya pili, nakwenda kunako hii Mahakama ya Kadhi. Katika Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 132, kifungu (d), kimesema kwamba suala hili litatatuliwa, ni kitu gani kinachofanya mpaka sasa hivi kuna uzito na ugumu na hii ni Ilani yetu wenyewe tumeitunga wenyewe ya Chama cha Mapinduzi, lazima tuitekeleze. Sasa ninashauri sana suala hili tulimalize ili haya mambo yakae vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho kabla sijagongewa kengele, jana mchangiaji mwenzetu wa upande huu hapa chini, bondeni hapo alisema, Mheshimiwa Rais Kikwete aingilie kati suala ya muafaka. Mheshimiwa Rais keshafanya kazi yake nzuri tu na kuipa Tume ya Muafaka chini ya Katibu Mkuu wa CCM, Katibu Mkuu wa *CUF* na bahati nzuri wajumbe wamo ndani humu, yumo Ali Ameir Mohamed, *Comrade Kingunge* yupo, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed yumo humu lakini nilitaka niulize hawa wenzetu hasa wanataka nini?

Mheshimiwa Spika, wenzetu hawa walisema kwamba wanataka muafaka, hatujakaa vizuri, wanasema wanataka Serikali ya Mseto, hawajakaa vizuri, wanasema sisi tutajitenga, sasa wanataka nini wenzetu hawa? Hebu waseme nini wanachokita, tukae pamoa tuzungumze lakini hili halijamalizika... (*Makofi*)

(*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kuisha*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ambayo imegusa maeneo mengi.

Mheshimiwa Spika, nianze kukupongeza wewe kwa jinsi unavyoliendesa Bunge hili kwa umahiri wa hali ya juu. Lakini pia nimpongeze Waziri Mkuu ambaye kwa kweli ni mnyenyeketu, ni mchapakazi na ameanza vizuri, tunampongeza sana. Nimpongeze Waziri Mkuu wetu wa kipindi kilichopita, amefanya mapinduzi makubwa sana katika suala la elimu, naye tunampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kazi ya Ubunge, ni kazi ya kutumwa na watu. Kwa niaba ya wananchi wa Misungwi, napenda nifikishe maneno yao katika Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Misungwi tunalo tatizo la maji na katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameelezea suala hili. Katika hotuba ya Wizara ya Fedha, wamezungumzia maji na mgawanyo wa fedha katika sekta mbalimbali ultolewa lakini kipaumbele cha maji kimeshuka sana. Sisi wananchi wa Misungwi, tunaumia kweli kwa sababu tuna matatizo makubwa ya maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sina matatizo na mradi wa maji kwenda Shinyanga na Kahama kwa sababu umeanzia kwenye Jimbo langu la Misungwi ambapo vijiji sita, vitapata maji kati ya vijiji 78. Asilimia 28 ya wananchi wa Misungwi ndio wanaopata maji safi na salama, hali ni mbaya kweli na tuko umbali wa kilomita saba tu kutoka Ziwa Victoria yaani Makao Makuu ya Wilaya ya Misungwi.

Mheshimiwa Spika, ahadi mbalimbali zimetolewa pale. Mheshimiwa Rais ametoa ahadi zake mara nyingi. Viongozi mbalimbali wanapotembelea Misungwi, wanaelezwa tatizo kubwa ni maji, sasa hivi hata katika hotuba, Misungwi haitajwitajwi, hatuna mbadala wa maji Misungwi. Tunategemea bwawa lililopo pale lakini litakauka wakati wowote ule. Wananchi wa Misungwi wananiuliza hivi Serikali hii inawatazamaje wananchi wa Misungwi kuhusu suala la maji? Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika majumuisho yako, uwaeleze ni nini umewapangia wananchi wa Misungwi kwa sababu tatizo ni kubwa kweli.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Edward Lowassa alipokuwa Waziri wa Maji, alikuwa anapanga. Kipindi kilichopita tulipewa milioni 400, juzi juzi ndiyo zimefika shilingi milioni 250 kati ya 400 kwenye mradi unaotegemea kutumia bilioni 15, tunawatakania nini wananchi wa Misungwi? Mna nia gani na wananchi wa Misungwi? Wananchi hawa wana mateso makubwa sana.

Mheshimiwa Spika, namuomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika majumuisho yake, awaeleze angalau wajue kwamba kuna nini katika bajeti ya maji. Tuna imani sana na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya lakini kwa bajeti hii ilivyo ndogo, tutamlamu bure, tunahitaji maji Misungwi yapatikane.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kilimo. Katika suala la kilimo, wakulima wamesahaulika sana. Bei ya zao la pamba, nizungumzie hiyo, mwaka jana wakulima wa zao la pamba walipewa Sh.450/-, Sh.500/=, Sh.550/=, bei ilikuwa inacheza hapo mpaka Sh.600 wakati bei katika soko la dunia ilikuwa ni senti 55, 50 ilikuwa inacheza hapo. Safari hii, bei katika soko la dunia iko kwenye senti 75, 76, 70 mpaka sasa hivi iko kwenye senti 64 inacheza hapo. Mwaka jana ilikuwa senti 55 mwaka huu iko kwenye senti 76 lakini Serikali imetangaza wanaanzia Sh.400/=, tunawatachia nini wananchi hao? Mpaka sasa hivi, hawajauza pamba yao, wanasubiri bei ipande, ianzie Sh.600/= na kuendelea juu ndiyo waweze kukokotoa gharama zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimejaribu kukokotoa gharama za kilimo cha pamba. Kulima eka moja ni Sh.25,000/=, mbegu Sh.25,000/=, palizi mara nne inakuja kwenye Sh.100,000/= na zaidi, kuvuna, madawa hayo ambayo kidogo sasa hivi yana ruzuku inakuja karibu Sh.180,000/=, wastani wa eka sasa hivi ni kilo 400, sasa 400 x 400, inakuja Sh.160,000/=, atapata nini mkulima huyu? Naomba bei iwe ni Sh.600 na kuendelea. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nenda ukakae na Bodi ya Pamba ili wanunuzi, waongeze bei ya pamba. Zungumza nao, waeleze sasa hivi bei iko juu, tunawatesa wakulima, sijui wafanyaje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji Ukirigulu ambaio unasihamiwa na Wizara ya Kilimo lakini zaidi zaidi ni Wizara ya Fedha. Fedha ziko hapa, hatuombi fedha, tunaomba usimamizi wa Serikali. Kulikuwa na wakandarasi watatu, mmoja wa kushughulikia umeme, amefanya kazi vizuri. Wa pili alikuwa ni kuleta pampu pamoja na *motor*, ameleta vizuri. Yule wa kukarabati ile bomba, nafikiri Mheshimiwa Waziri Mkuu, barua yangu imeshakufikia huku, nimetembelea pale Ukirigulu, wale wataalamu wetu pale wana matatizo makubwa sana. Zaidi ya miaka 10 wanahangaikia mradi huo, fedha zipo, Mheshimiwa Keenja, anafahamu suala hilo. Nimejibowi mara mbili hapa, ukarabati umeanza lakini yule jamaa analipua kazi. *CAG* aende akafanye kazi hiyo huko ataona maajabu ya kutosha kule. Watu wanataka kula fedha hivi hivi tu, wanataka kugawana fedha hapo hapo, hakuna kazi inayoendelea, yule mkandarasi miezi mitatu sasa hivi hayupo kwenye eneo la kazi, ameziba kabisa mahali pa kuweka vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, lile bomba limesimikwa kwenye nguzo *zinazo-hang* na halijavuta maji. Wamejenga matanki mawili pale juu Ukirigulu, lile tanki moja kubwa lina ujazo wa lita 380,000. Mkandarasi aliyejenga, ni wa Daraja la Pili, ukienda kuangalia lilivyojengwa, utafikiri ni wa daraja sijui la ngapi, likipasuka hapo ni maafa. Watu wa *CRB* wa *IRB* wamepita pale kuangalia hawajatoa ripoti, sijui wana nini hawa nao? Mheshimiwa Waziri Mkuu, agiza vyombo vyako watoe ripoti na utueleze nini kinachoendelea kwa sababu hali ni mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, watu wa Ukirigulu wana matatizo, maji ni historia, vijana hawajui maji, kama kijana ana umri wa miaka 10 lakini hajui suala la kufungua maji. Wataalamu wetu wapo hapo Ukirigulu, ni karibu lita 50 za *diesel* wanaweka kwenye magari yao kufuata maji Mwanza kwa ajili ya Wanachuo waliopo hapo. Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulishughulikie suala hili.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye maombi maalum. Shule ya Msingi Mitindo, ni ya watu ambao kwa kweli wana matatizo, ni ya wasioona, tuna Albino wengi sana sasa hivi, tumeomba Serikali itupe zaidi ya shilingi milioni 240. Maombi maalum yako kule Wizarani, yashughulikieni ili tuweze kupata fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kituo chetu cha Afya, sasa hivi tumekipandisha hadhi na kuwa Hospitali ya Wilaya. Tumeomba maombi maalum kama Sh.950,000,000/= ili tuweze kupanua hospitali yetu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la maji, tumeona tujipange, tumeomba kama shilingi bilioni 2.8 kwa ajili ya kutandaza bomba kwenda Ziwani na kuvuta yale maji yaje kwenye bwawa letu ili angalau kupata maji hapa na yaingie kwenye mzunguko wa kawaida. Tumeomba kama Sh.150,000,000/= kwa ajili ya nyumba za watumishi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madai ya Walimu, lipo tatizo kubwa sana kwa Walimu. Wilaya ya Misungwi, bado inadai madai ambayo yameshahakikiwa kama Sh.150,187,000/=, hali ni mbaya sana. Kuna madai ya likizo, matibabu, mafunzo masomoni, uhamisho, kujikimu, mnawakwamisha sana Walimu hao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi mbalimbali. Waziri wa TAMISEMI, aliahidi kuja kwetu lakini bahati nzuri akawa amepanda, tunakupongeza sana Mheshimiwa Kombani lakini matatizo bado yako pale pale kwenye barabara ya Mwaniko, hali ni mbaya kweli. Tafuta fedha kwa ajili ya barabara yetu hiyo ili wananchi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *NMB*, benki hii inatupa shida kweli wakati mwengine kama tungakuwa tunaweza kubadilishana, ningewapa ile ya Misungwi kwa sababu inatesa watu kuliko utaratibu. Huduma yake ni mbovu, Walimu wangu wanapanga foleni mpaka siku tatu kufungua akaunti tu yaani sijui kama unafanya nini, nafuu uende Mwanza. Wanaohusika na *NMB*, jamani hebu waende wakaifuatilie ile *NMB* iliyoko kule kwetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine, ni hili suala la Madiwani, nawapongeza sana lakini hebu waongezee ni fedha katika zile fedha za fidia.

Mheshimiwa Spika, suala la *barrier*, zinasumbua sana watu njiani. Kuna moja ile ambayo iko ndani ya uwezo wetu na Halmashauri yangu, ile ya pale Misasi. Nimeongea na Mkurugenzi, kuanzia leo haitakuwepo, tumeitoa kabisa. Wananchi wangu wa Misasi na maeneo mengine ya Buhingo, Busongo, Mwagiligili waendelee kufanya biashara yao vizuri. Imefutwa mara moja ili angalau sasa wananchi wawahi kwenye shughuli zao. Ni vema sasa watu wafanye biashara zao bila matatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho nirudie tena kukupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Haya yote niliyoyazungumza, nina imani utayafanya kazi lakini kubwa zaidi maji, bei ya pamba, shughulikia sana masuala hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, hongera sana.  
(*Makofii*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, itifaki ya salamu na pongezi, nimeizingatia.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikipokea hisia na salamu za tofauti tofauti kutoka kwa wapiga kura na wananchi mbalimbali hasa kutoka kwenye Mikoa yetu ya Kanda ya Magharibi na Kanda ya Ziwa, hasa kuulizia mipango iliyopo ya maji, umeme, barabara, kilimo, reli na mengine minge.

Mheshimiwa Spika, kwa haraka sana nasema hivi, mipango iliyokuwepo katika suala la maji, nadhani imefika mahali ambapo gari hii imezama na Serikali haitaki kukiri na kusema ukweli kwamba hapa kwenye suala maji gari hii imezama. Hii ni kutokana na kwamba toka bajeti ya mwaka 2004/2005, zilitengwa Wilaya 50 ikiwemo na Wilaya ya Nzega kupelekewa maji kwa kupitia mradi wa Benki ya Dunia, kwa mradi ule wa *RWSSP*. Ukipuutilia sana, utaona kwamba, Serikali haijakiri kwamba imeshindwa kutimiza ahadi hiyo, mara nyingi inasingizia visingizio mbalimbali, mara Benki hawajatimiza sijui masharti, mara Halmashauri hazijatimiza masharti yake, mara kuna *Quick Wins*, hebu tuambieni ukweli, kama mmeshindwa au kama imeshindikana, wananchi wakae wakijua kuliko kusubiri ahadi ambayo wala haiwezi kutekelezeka.

Mheshimiwa Spika, kwa hili, naomba Serikali itamke wazi, Waziri wa Maji atamke wazi na kwa kweli katika Wizara ya Maji, tunamtumia salamu kabisa, hapa kwa kweli hakitaeleweka chochote kwa sababu hata bajeti ya mwaka huu ya maji imeshuka ikilinganishwa na bajeti ambayo ilikuwa imepitishwa mwaka fedha uliopita! Napendekeza bajeti zijazo sasa msisitizo na kipaumbele kiwekwe kwenye suala hili la maji ili kuwapatia wananchi wetu maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la kilimo. Naomba Serikali isione aibu kwani dunia nzima inazingatia maslahi ya wananchi wake. Katika hili, naiomba Serikali izingatie maslahi ya wakulima wetu, wananchi wa Kitanzania. La kwanza, napenda Serikali ijizatiti vema katika suala hili la mbolea ya ruzuku. Hili napenda Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahakikishe mbolea kwa Mkoa wa Tabora imefika kama siyo mwezi Agosti, basi mwezi Septemba, mbolea ikifika baada ya miezi hiyo, inatuletea matatizo. Matatizo hasa yanakuja kwa wakulima kwa sababu hawawezi kwenda na kipindi kizuri cha kulima kwa kutumia mbolea pamoja pembejeo zake kwa maana ya mbegu na vitu vya namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini suala kubwa ambalo ninapenda kulisitisiza katika suala la kilimo, ni suala la umwagiliaji maji. Ukiangalia hata hizi *scheme* za umwagiliaji, zote zinategemea mvua, ni chache sana ambazo zinategemea moja kwa moja umwagiliaji maji.

Mheshimiwa Spika, ninapenda misamaha hii ya kodi wanayoitoa mpaka inafikia asilimia 25 iweze kwenda kwa wakulima ili wakulima waweze kulima kwa kutumia pembejeo lakini kiasi kikubwa kikaenda kwenye suala la umwagiliaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la umeme, Waziri wa Nishati na Madini, tafadhali sana, kaa mkao mzuri, bajeti yako tunaisubiri kwa hamu. Mheshimiwa Waziri, alishatuhidi hapa kwamba atapeleka umeme Punge mpaka Ndala na Bukene kwa mwaka huu wa fedha lakini kwenye vitabu sijaona. Kwa hiyo, tafadhali, kaa vizuri, hapa kwa kweli hapatatoka mtu na shilingi yako, natanguliza kabisa ukae nayo mapema, hapataelewaka.

Mheshimiwa Spika, toka miaka ya 1980, Wilaya ya Nzega, ilipata umeme ulioukuwa unakwenda Tabora kwenye *grid* ya Taifa iliyopita Ndala na Punge, wananchi wanaangalia tu mpaka leo hawajapewa umeme.

Mheshimiwa Spika, hili, utatuwia radhi sana. Mwaka jana, walituhidi, wakasema tuwe na subira, kumbe subira yanaumiza matumbo. Tafadhali kaeni mkijua kwamba bila umeme kwenda Ndala, Punge na Bukene, hapatoki mtu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala sugu...

**SPIKA:** Mtu hatoki wapi sasa?

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, humu ndani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nakuja kwenye suala sugu na ninaomba uniunge mkono, nalo ni suala la barabara. Maendeleo ya uchumi ya nchi yoyote, yanategemea sana miundombinu ya barabara na reli. Bajeti ya mwaka huu 2008/2009, imekuwa kimya kabisa kwenye bajeti ya barabara ya kutoka Itigi -Tabora - Kigoma. Imekuwa kimya kabisa kwa barabara ya kutoka Nzega - Tabora - Ipole - Mpanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi, toka mwaka 2006/2007, kama unakumbuka, nakuomba sana urejee mwaka 2006/2007, mwenyewe uliniomba kwamba hebu acha, hebu tulia, mimi ni Chifu wako na *Hansard* ninayo hapa nitakupa, wakati huo Serikali ikaji-*commit* kwamba barabara hiyo itajengwa mwaka 2006/2007. Mwaka jana, bajeti hii tunayomaliza mwezi huu ya mwaka 2007/2008, Serikali ikaji-*commit* tena kwa mara pili, bahati nzuri wewe mwenyewe ulikuwepo kwenye Kiti na wakasema barabara hiyo ya Itigi -Tabora - Kigoma imepandishwa hadhi, ikapewa na namba ya *Trunk Road* ambayo ni T18. Mwaka huu wa fedha, nimesoma vitabu vyote hivi kuanzia Kitabu cha Kwanza mpaka Kitabu cha Nne, nimesoma Kitabu cha Mipango ya Maendeleo, nimesoma hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, nimesoma kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu, nimesoma na majedwali yake, barabara hii haimo.

Mheshimiwa Spika, inamaanisha kwamba kumbe humu ndani wanatukebehi? Inamaanisha humu ndani wanatudharau? Inamaanisha ile ahadi ya kutoka mwaka

2006/2007 na hata wewe Mheshimiwa Spika, uliji-*commit*, ni kebehi na ni dharau kwa wananchi wa Kanda ya Magharibi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi wanataka tuseme na Kinyamwezi au Kisukuma, ndiyo watuelewe? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Jaribu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucas Selelii, hiyo si lugha rasmi ndani ya Ukumbi huu.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, ukae na wewe mwenyewe utoe hoja. Inauma sana, tena inaumiza.

Mheshimiwa Spika, nimesikitika sana hata kuitaja katika sentensi hata moja tu, hotuba ya Waziri Mkuu, hotuba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, wote hawakuitaja. Inamaanisha hata Waziri wa Miundombinu na wengine, wala hawana habari nayo. Au ndiyo ile methali inatimizwa kwamba ‘funika kombe mwanaaharamu apite’, hatukubali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi, imewekwa wazi kabisa, Mheshimiwa Rais amekuja mara mbili, tatu akisema wazi kabisa hata Bunge nalo linadanganywa! Kwa kweli hapa, lazima ieleteweke. Mimi naomba Waziri Mkuu aji-*commit* sijui kwa kauli ya Mawaziri, aji-*commit* sijui kwa kuandika tena hotuba yake nyingine mpya kwamba barabara hii ya kutoka Itigi – Tabora - Kigoma, Nzega - Tabora itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia mwaka huu wa fedha. Hapo ndipo nitaelewa na hapo ndipo kitaeleweka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu gani? Barabara hii hatuihitaji tu ili kwamba barabara iwepo, ina faida zake kijamii. Ukijenga barabara toka Tabora - Kigoma kuanzia Itigi kuja Tabora - Nzega - Ipole na bahati nzuri barabara hii ilikwishafanyiwa usanifu tangu mwaka 1994. Usanifu ulikwishafanyika tokea Manyoni - Itigi –Tabora - Ipole - Mpanda toka mwaka 1994. Kijamii wale wananchi wa Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Kigoma na Mkoa wa Tabora, unawapa uhakika wa usafiri kama Mikoa mingine inavyofanya.

Mheshimiwa Spika, wakati ule, nilikuuliza kwamba kama unataka kuondoka leo kwenda Urambo utaweza? Hauwezi! Itabidi urudi Dar es Salaam upande ndege uende Urambo, lakini wakubwa wenzio wanaondoka hapa wanakwenda kwao, wanatumia masaa tu. Hivi sisi watu wa Kanda ya Magharibi, tumeifanya nini Serikali hii?

Mheshimiwa Spika, barabara hii kijamii, itatusaidia sana kuwa na *movement* ya watu wa Magharibi, watu wa Kanda ya Rukwa ambao wana mazao ya kutosha, watu wa Kigoma, watu wa Mwanza, itatuwezesha kuwasiliana kijamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine itatusaidia kwenye suala la utalii. Kuna mbuga za wanyama ya Katavi, Gombe kule Kigoma, tu-*diversify* kutoka mbuga za wanyama za Kaskazini twende kwenye mbuga mpya ambazo zinalipa.

Mheshimiwa Spika, lakini kiuchumi, kuna DRC Kongo. Pale DRC Kongo, kuna mzigo wa dola bilioni mbili, huwezi kuzisafirisha kama hauna barabara wala reli.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba hizi zote, mipango ya barabara haikutajwa, mipango ya reli vile vile haikutajwa. Reli yetu sasa hivi, ukienda *station*, ni aibu, wanawasafirisha wananchi utadhani kuni. Wasafiri wa reli wanajazwa kwenye treni kama kuni! Wanajazwa mle utadhani wamepanda bure kumbe wamelipa pesa na ni wananchi wa Tanzania hii hii. Tufike mahali ndugu zetu, mtuelewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nawaambia hao waliokaa mstari wa mbele, watuelewe kwamba hata Kanda ya Magharibi, Kanda ya kwetu kule na sisi ni Watanzania, tunataka barabara, tunataka reli.

Mheshimiwa Spika, reli hii, asilimia 51 ni ya mtu binafsi, ya Muhindi, asilimia 49 ni ya Serikali. Kuna kazi ambayo Serikali inatakiwa ifanye kwa sababu asilimia 49 ni ya kwake! Tunataka reli, tunataka barabara kwa sababu ambazo nimezitaja za kijamii, utalii pamoa na kiuchumi.

Mheshimiwa Bwana Spika, kwa sababu ahadi ni deni, nitaomba Mwongozo wako, ahadi hii ya mwaka 2006/2007, ahadi hii ya 2007/2009 na mwaka huu kutokuiweka kabisa kwenye bajeti, naomba Mwongozo wako, tufanye nini ili barabara hii ya Ipole - Tabora - Itigi - Kigoma - Nzega iwemo kwenye vitabu hivi vya maendeleo? Nitakuomba sana unipe Mwongozo na niko tayari kukaa sasa hizi ili nipate Mwongozo wako, hata dakika tano zilizobaki nitaziacha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ...

**SPIKA:** Tutasubiri majibu ya Serikali. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, lingine ni kumwinua Mtanzania. Ukiangalia Mtanzania wa kawaida, wale wananchi wa kawaida wako wengi sana hapa chini, Watanzania wachache hasa wenye *Passport*, ndiyo wako juu, hao ndio wenye nacho. Hapa katikati, ipo *gap* kubwa sana kati ya Watanzania wasionacho ambao ndiyo Watanzania halisi na Watanzania wenye *Passport*, wachache ambao wanacho.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwenye Serikali kwamba imefika wakati sasa ifanyike hatua ya makusudi, hatua ya kisiasa ili kutafuta daraja la kati, daraja ambalo litawainua Watanzania halisi ambao ni wafanyabiashara, wasomi ili waweze kushika uchumi kwa sababu kuwapata Watanzania wachache wenye *Passport* walioko juu, ni

ngumu sana na ni parefu sana. Hivyo liwekwe daraja la kati ambalo litawainua Watanzania wetu halisi ambao wana uchungu na nchi yao.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia nchi hii, uchumi mwingu ambao Mwalimu Nyerere aliuchukua wakati wa Azimio la Arusha, kwa sasa kidogo kidogo umerudi kwa Watanzania wa *Passport*, tena tumeurudisha kwa haraka sana.

Mheshimiwa Spika, nakupa mfano, nenda *Pugu Road*, *Pugu Road* yote imechukuliwa na Watanzania wachache wa *Passport* wale Watanzania halisi, wapo Pugu Kajiungeni, ndiyo wanapelekwa kule. Angalia Upanga, ni Watanzania wachache wa *Passport*, Watanzania wenyewe Kinyerezi. Watanzania wachache wamenunua *PSRC*, wale wa *Passport*, Watanzania wenyewe ndiyo wanaambiwa nendeni mkanunue *NMB*, nendeni mkanunue *CRDB*, huko sio kushika uchumi. Tunawataka Watanzania halisi wa ngozi kama ya kwangu wamiliki uchumi, wawe na utashi katika mabenki, wawe na utashi katika mashirika ya umma na wawe na utashi katika mashirika yao binafsi yenye nguvu. Angalia hata *Bureau de Change*, ni za wachache sana. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili hiyo sasa.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Eeeh!

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nina udhuru kidogo, nitamwomba Mheshimiwa Mwenyekiti, Jenista Mhagama, aweze kushikilia Kiti kwa muda uliosalia.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Msemaji anayefuata sasa, ni Mheshimiwa Missanga.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa salama ili niweze kutoa mchango wangu kwenye hoja hii tulio nayo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nitoe shukrani zangu za dhati kwako kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri na kwa maandalizi mazuri, ye ye na Mawaziri wake wote na wote ambao wanamsaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie nafasi hii, kwanza kumpongeza Mku wa Mkoa wangu, Mheshimiwa Kone, kwa sababu kwa kipindi ambacho amekuwa na sisi Singida, kwa kweli ametusaidia sana. Tumepata maendeleo mazuri kwa

ushirikiano mkubwa ambao tumeupata kutoka kwake na hasa sisi Wabunge tunajivunia ya kwamba anatusikiliza na anatushauri na tunashirikiana naye vizuri. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikiipongeza Serikali kwa mafanikio ambayo yamepatikana chini ya Serikali ya Awamu ya Nne, naendelea kumpongeza Mkuu wa Mkoa kwa sababu alipokuja alitukuta sisi tuna shule na sekondari kama 30 hivi, 18 za Serikali na 12 za watu binafsi lakini kwa jitihada zake, katika kipindi ambacho amekuwepo yeye, zimejengwa sekondari 90, ukichanganya na zile 30 ambazo alitukuta nazo, tumefikia sasa sekondari 120. Kwa kweli, anastahili sana sifa na shukrani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninyi mna kawaida kwa Singida, mkileta watu wazuri, wakifanya vizuri, mnawondoa, sasa huyu mkimwondoa, tutafanya maandamano. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka nijielekeze kwanza Jimboni kwangu. Kwa muda mrefu, nimekuwa nikieleza Bunge hili tatizo la wanyama wakali ambao ni simba na tembo.

**MBUNGE FULANI:** Sio tembo ni ndovu.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Alaah. Haya ndovu, zaidi ya mara tatu nimeeleza katika Bunge hili katika vikao hivi ya mikutano ya bajeti, naweza kusema kwamba sijasikilizwa na suala hili halijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza hapa, wananchi ambao wameshaliwa na simba ni 14 tena kwa kipindi kifupi tu, wa mwisho ameliwa juzi tarehe 20 kuamkia tarehe 21. Hili ni tatizo. Suala hili, nimelieleza mara nyngi sana lakini mpaka sasa, hakuna hatua zozote ambazo zimechukuliwa ndiyo maana wananchi wanaendelea kupoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kule kwenye Tarafa ya Ikungi, watu wanaishi kwa wasi wasi, hawaendi kwene kazi za maendeleo, hawaendi kulima, hawaendi kuchunga, vijana wanasa kwenda shulenii hasa wakichelewa kwa sababu shule ni mbali na wanakokaa, wanakuwa na wasiwasi wa kurudi majumbani mwao. Wananchi 14 wameliwa na simba kwa kipindi cha miezi miwili iliyopita, hili ni tatizo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa na *DC* wangu, kwa kweli *DC*, amejitahidi sana. Tumepata msaada wa kikosi cha Wanyamapor pale Manyoni lakini hata hivyo bado hawajafanikiwa kuwapata hawa simba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu ingilie kati na utafute njia ya kusaidia ili wananchi wasiendelee kuliwa na simba kule Singida. Ikiwezekana, ushauri wangu ni kwamba, maadam sasa jitihada za hawa Askari Wanyamapor hazifanikiwi, hebu Mheshimiwa Waziri Mkuu aamrishe Polisi

washirikiane na Askari hawa wa Wanyamapor, kutumia helikopta walau wanaweza wakawaona hawa simba na wakawashughulikia ili kusudi kero hii iondoke kwani wananchi sasa hawashiriki katika shughuli za maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokwenda kwenye mazishi ya kijana yule wa 13, vijana waligoma kwenda kuzika, wakasema Serikali hamchukui hatua, sisi hatuendi kuzika kwa sababu ninyi mnafurahia huu mchezo na asilimia kubwa ya waliouliwa na simba, ni vijana. Ilibidi nifanye kazi kubwa sana kuwapiga siasa, mwisho nikaingia kwenye mambo ya dini kwamba twendeni tukazike kwanza halafu baadaye tutakuja kuzungumza suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, amsaidie Mkuu wa Mkoa wangu na *DC* wangu, watafute njia za kumaliza tatizo hili ili wananchi hawa waweze kufanya kazi zao za maendeleo maana sasa hivi hawafanyi, ikibidi watumie helkopta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo nataka nizungumze ni suala la barabara. Sisi watu wa Singida, kwa kiasi Fulani, tunaendelea kushukuru kwamba barabara sasa zinaendelea kutengenezwa na karibu zitakamilika ingawa zimechelewa. Barabara ya Singida - Babati – Minjingu, nayo imo kwenye programu ya kujengwa mwaka huu, kwa hiyo, tunashukuru. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ya Dodoma – Manyoni – Singida, inajengwa lakini kwa kusuasua. Tatizo hapa ni Wakandarasi hawalipwi pesa katika wakati unaotakiwa matokeo yake wanaweka vifaa chini, wanaweka vifaa vyao chini. Mkandarasi huyu ambaye ni Konoike, anayejenga barabara ya Dodoma – Manyoni, mara kadhaa ameweka vifaa vyake chini kwa sababu hajalipwa, ndiyo maana barabara hii haijaisha, ilitegemewa iihe mapema lakini mpaka sasa haijaisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha kile kipande *SIETCO* cha Manyoni – Singida, kwenye hii barabara ya Dodoma – Manyoni, haikuwa na sababu kwa nini isishe katika wakati uliopangwa, ni sababu ya sisi au Serikali imeshindwa kumlipa Mkandarasi kwa wakati unaotakiwa na ndiyo maana amekuwa akiweka vifaa vyake chini, barabara haikamiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, atumie njia zozote zile, kuhakikisha kwamba hizi kazi ambazo zimeanzwa, zinamalizike ili barabara zingine nazo ziweze kujengwa. Hatuwezi kuendelea kila siku kuzungumzia tu barabara ya Dodoma – Manyoni – Singida - Mbwemkulu, haiwezekani, tuimalize ili tuingie kwenye maeneo mengine ambayo nayo yanahitaji ujenzi wa barabara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposhindwa kumlipa Mkandarasi, kuna faini kubwa katika mikataba yetu na faini hizi, zina *interest* kubwa za kibiashara, utakuta tuna deni kubwa lakini ni kwa sababu ya faini na *interest* ambayo inatozwa ambayo ni kubwa kulikoni zile fedha ambazo walitakiwa walipwe kwa kujenga. Kwa nini tuijingize kwenye habari ya kutozwa faini na *interest* kubwa hizi wakati tunaweza kukamilisha

suala hili mapema iwezekanavyo? Naomba Waziri Mkuu, kwa kushirikiana na Serikali kwa ujumla, zitolewe fedha za kutosha kwa ajili ya ujenzi wa barabara hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muda mrefu, tumeomba uwanja wa ndege wa Singida utengenezwe. Sisi kule Singida tunakosa wawekezaji kwa sababu mwekezaji hawesi kutoka Dar es Salaam mpaka Singida masaa 12 amekaa kwenye *Land Rover* au kwenye gari, haiwezekani! Mwekezaji anataka atumie saa moja, anakuja Singida, anaangalia mahali panapohusika, kwenye madini, kwenye kilimo, anarudi lakini wewe unamwacha kwenye gari atembee masaa 12, masaa 20, mwekezaji gani atakayekuja huyo? Tunakosa watalii kwa sababu hatuna uwanja wa ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, Mkuu wa Mkoa amejitahidi kwa zile Sh.100,000,000/= ambazo tulikuwa tumepewa kwa kushirikiana na wafadhili na wahisani wetu walau kimetengenezwa kwa changarawe lakini mvua zikinyesha mara mbili nina hakika ile kazi yote iliyofanywa, fedha yote iliyotumika pale, itakuwa imepotea bure.

Mheshimiwa Spika, niombe sana, maadam sasa changarawe zipo pale tayari ni vizuri angalau itiwe lami, kile kipande kidogo tu cha kilometa moja na *point* ngapi, cha *run away*, sisi hatutaki lote, kipande ambacho kitasaidia ndege za abiria 20 au 28 waweze kutua ili kusudi wawekezaji waje. Lakini hata viongozi wetu wakati mwingine tunawakosa kwa sababu ya usafiri tu, Rais anafikiria atoke Dar es Salaam mpaka kule kwa barabara, atakuja saa ngapi? Mheshimiwa Waziri Mkuu, atoke sijui wapi, kwa barabara, atakuja saa ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba hili nalo liweze kufikiriwa, maadam sasa kazi imefanyika vizuri, hebu wamalizie hiki kipande kilichobakia kwa lami ili na sisi tuweze kupata *run away* na ndege ziweze kutua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenzangu amezungumzia habari ya *TBC*, mimi nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Tido Mhando, kuwa Mkurugenzi Mkuu wa *TBC* na anafanya kazi vizuri. Mabadiliko yako makubwa, *television* yetu sasa *ime-improve* sana ukilinganisha na zamani. Hata watazamaji wa *television*, sasa wametoka kwenye *TV* nyingine wanaangalia zaidi *TBC*, kwa hiyo, nampongeza lakini Singida, haisikiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, anapozungumza na wananchi kuititia *TBC* au kuititia radio, sisi wananchi wa Singida hatumsikii, hatupati maelekezo yake na wala hatusikii nasaha zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aliyekuwa Waziri wa Habari wa zamani, Mheshimiwa Mohamed Seif, alikuja kule, akaahidi vitu kadhaa kwamba hali itakuwa nzuri, mpaka leo, hakuna chochote ambacho kimefanyika hata Mheshimiwa Mkuchika amekuja, lakini hamna lolote. Ndugu Tido mwenyewe amekuja, amezungumza na uongozi lakini hakuna kinachofanyika. Hivi sisi tuna makosa gani, wananchi wa Singida wana makosa gani

hadi kuwafanya hawapati habari kutoka *TBC* iwe ni kwa njia ya *television* au radio? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wachache wale wenye ungo, ndio wanaona *TV*, wenye uwezo lakini walala hoi hawana uwezo wa kununua haya madubwasha makubwa ambayo tunanunua sisi wengine haya. Naomba sana, nampenda sana Tido, rafiki yangu, hebu aliangalie suala hili, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu ili kusudi na sisi Singida tuweze kupata huduma za *TBC*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Nne, ina msemo wa ‘nguvu mpya, kasi mpya na ari mpya’ lakini ni katika mambo mengine kasi ya maamuzi siioni. Kwa mfano, tumezungumza muda mrefu kwamba maadam sisi fedha za ndani za kujenga barabara hatuna na miundombinu mingine, tuingie kwenye mpango wa *PPP (Public Private Partnership)*. Tumezungumza hapa mara nyingi sana lakini hakuna kitu kilichofanyika. Mpaka leo ninavyozungumza hapa, Sera ya *PPP*, haipo matokeo yake ni kwamba wawekezaji wanakuja toka nje ili watusaidie kujenga barabara, *flyovers*, bandari zetu hizi, wanazungushwazungushwa kwa sababu sera haipo, kulikoni? Kuna tatizo gani la kutokamilisha sera hii? Upande mmoja tunasema hatuna fedha za kujenga miundombinu upande wa pili, kitu ambacho kingetusaidia kupata miundombinu ya uhakika chini ya Sera ya *PPP*, hata sera hatutengenezi, tunaji-*contradict*, tatizo ni nini? Kwa nini maamuzi hayafanyiki kule Serikalini? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine ambalo limeshindikana kutolewa maamuzi kwa muda mrefu, ni daraja la Kigamboni. Kila siku daraja la Kigamboni, daraja la Kigamboni na Ilani ya Uchaguzi, inasema lishughulikiwe. Mara ngapi hapa tumeahidiwa, Kamati zimekaa, wewe Mwenyekiti unajua Kamati yako na Kamati yangu mimi, tumekaa kuzungumzia daraja la Kigamboni, tukaahidiwa lakini hakijafanyika kitu mpaka leo, kuna nini? Hiyo kasi mpya iko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili ambalo amezungumzia mwenzangu Sheikh Hassan hapa, suala la Mahakama ya Kadhi Mkuu. Suala hili limepigiwa kelele mara chungu mzima hapa na ndani ya Ilani, limezungumziwa, ni maneno matupu yanapigwa hapa. Ngojeni, sijui umuulize huyu, utamwuliza nani, muulize mtu anayehusika na hiyo Mahakama ya Kadhi, unakwenda kumwuliza mtu ambaye hahusiki, si atakuambia hapana! Muulize mtu anayehusika kama kweli wewe utanufaika kwa kuwa na Mahakama ya Kadhi, hilo nalo halijafanyika mpaka leo, kuna nini, kwa nini maamuzi hayatoki? (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vitambulisho vya uraia, toka tumeanza kuimba habari ya vitambulisho hapa, huu sijui ni mwaka wa ngapi, kila siku ngojeni itakuwa hivi, kasi mpya iko wapi katika kufanya maamuzi juu ya jambo kama hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, kaanza vizuri. Hebu atilie mkazo katika kufanya maamuzi vinginevyo, yanakuja kutugharimu haya kwa sababu tumechelewa kuyashughulikia.

Mheshimwia Mwenyekiti, muda unakwenda, liko tatizo la mikopo ya JK, wanaofaidi, ni watu mijini lakini watu wa vijijini, hawafaidi hizi pesa, asilimia 80 ya wananchi wako vijijini lakini fedha hizi hawapati. Mabenki yapo mijini, wanasema hawana watumishi wa kwenda vijijini kwenda kuwapa mikopo, sasa kama asilimia 80 hawapati hizi fedha wanapata asilimia kumi na ngapi au ishirini, hilo ni tatizo. Kwa nini wananchi wa vijijini wanapata matatizo hivi na wao wanalima lakini *at the end of the day*, wanaofaidi, ni wale wengine ambao wanahangaika kiasi fulani. Hawa walala hoi walioko vijijini, hawasikilizwi wala hawapati hayo manufaa yanayohitajika, naomba hili nalo liweze kuangaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, mradi wa maji umezungumzwa. Wilaya ya Singida, ni mionganoni mwa zile Wilaya ambazo alisema ndugu yangu pale, zilikuwa ziingie kwenye mradi huu. Yako malumbano kati ya Wizara ya Maji na Halmashauri zetu, tatizo lipo wapi? Ukienda Halmashauri, wanakuambia Wizara wanachelewesha, ukienda Wizarani, wanakuambia Halmashauri zinachelewesha. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu waite ukae nao pamoja ili ujue tatizo lipo wapi. Mwananchi kachangia fedha yake mwenyewe toka mwaka 2003, akitegemea atapata maji, huu ni mwaka wa sita, mwaka wa saba, hajapata maji na fedha katoa! Tatizo ni urasimu na mgongano uliopo kati ya Wizara ya Maji na Halmashauri zetu. Tatizo lipo wapi, hebu waweke chini hawa, uwaulize tatizo lipo wapi ili wananchi waweze kupata maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maombi mengi sana ya ugawaji wa Kata na ugawaji wa vijiji, ni ya muda mrefu sana. Mimi nilitazamia katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu walau angedokeza hatua ambazo zimefikiwa katika kugawa Kata na Vijiji, lakini sijasikia. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, hili nalo alishughulikie, wakati umefika. Mwakani, tunaingia kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ni vizuri sasa yakatolewa maelekezo vijiji vikagawiwa, Kata zikagawiwa, ili tukiingia kwenye uchaguzi mwakani basi mambo yatakuwa yanakwenda sawa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pensheni ya wastaafuli. Ni aibu mtumishi aliyefanya kazi kama Katibu Mkuu wa Wizara, kwa uaminifu, kwa uadilifu, hakujihusisha na rushwa, analipwa Sh.21,000/= kwa mwezi, ni aibu. Tunawadhalilisha hawa, tunawafanya wengine nao waone kwamba, mmh, kama sikuchukua changu mapema, mwishoni sitapata chochote. Hivi hili nalo, kweli hata kwa busara ya kawaida tu, Serikali haioni kumlipa mstaafuli aliyefanya kazi kama Katibu Mkuu wa Wizara, amefanya kazi nzuri, miaka nenda miaka rudi mpaka amestaafu, Sh.21,000/= ni kumuonea? Akina Apiyo, akina Mulokozi, wengi tu mpaka tunawaonea huruma kwa sababu walikuwa waaminifu, walikuwa waadilifu, nadhani wamesikia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Ni kengele ya pili hiyo?

**MWENYEKITI:** Kengele ya pili Mheshimiwa!

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Missanga, kwa mchango wako mzuri kabisa. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Felix Christopher Mrema, Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, ajiandae, Mheshimiwa Said Nkumba na yeye ajiandae.

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii.

Nianze kama wengine walivyoanza, kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wawili walio chini yake, Mheshimiwa Marmo na Kombani na Naibu Waziri Mkuu, samahani, Naibu Waziri, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, *Inshallah*, Makatibu Wakuu na Viongozi wote walio chini ya Ofisi hii ya Waziri Mkuu, kwa bajeti nzuri iliyowasilishwa na Waziri Mkuu Jumatatu hii. Nianze kwa kusema, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuanza, niseme machache juu ya Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda. Mheshimiwa Mizengo Kayanza Pinda, yule ambaye tulikuwa tunamfahamu akiwa mtumishi wa Serikali, ni huyo huyo tunayemwona sasa hivi hapa kama Waziri Mkuu. Vyeo havijamkwaza, mtulivu, msikivu, ametulia, hana papara. Mimi binafsi, wananchi wa Jimbo la Arusha na naamini Watanzania wengi, tuna imani kubwa na amani ya kipekee kwamba chini ya uongozi wake, haki itatendeka wakati wote na uzalendo utadhihirika katika maamuzi yake atakayoyafanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yeye hahitaji semina ya Ngurudoto, hahitaji pia kukumbushwa kwamba eti ana bajeti zingine mbili zilizobakia na ile ya pili ni ya lala salama. Huyu naamini anaelewa kabisa umuhimu wa kujipanga kuanzia sasa. Taifa linategemea kwamba miaka hii miwili na nusu itakapokwisha tutakaporudi tena kwa wananchi, tutakuwa na kila sababu ya kusema kwamba zile ahadi tulizozitoa kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi, zimetimizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa namshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, ili tuweze kwenda kifua mbele kwa wananchi mwaka 2010, uzingatie yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tutaendelea kutegemea mapato ya kodi na fedha za wahisani peke yake, hazitatosha kufanikisha ahadi zetu tulizozitoa kwenye Ilani ya Uchaguzi, mikopo haikwepeki. Mimi nimefarijika kwamba katika bajeti hii, angalau mmeanza kuzungumzia kwamba Benki Kuu iko mbioni kukamilisha utaratibu wa kutumia *Sovereign Bonds* na kupata fedha kuititia utaratibu huu. Lakini ninavyowaelewa wenzangu wa Benki Kuu, azma ni kitu kimoja lakini *speed* ya kukamilisha mambo, ni kitu kingine kabisa. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, wasimamie hawa viongozi ili wakamilishe jambo hili upesi iwezekanavyo ili na sisi tufaidike na kupata mikopo kutoka masoko ya duniani pamoja na huku ndani nchini, tuige mfano wa wenzetu hapa Kenya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti ya mwaka huu, wenzetu wa Kenya, wata-float *Sovereign Euro Bonds* na *Infrastructure Bonds* na wamejipangia kabisa kwamba kwa mwaka huu wanategemea kupata shilingi bilioni 88 kwa mpango huu wa *Sovereign Bonds* kwa mahesabu ya haraka haraka hiyo ni kama bilioni moja na nusu *USD dollars*, iko kwenye bajeti yao kwa mwaka huu wa fedha. Sasa na sisi twende hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshauri Mheshimiwa Waziri Mkuu, awasimamie kabla ya mwisho wa mwaka huu utaratibu huu ukamilike, mwakani wakija hapa na sisi tuje na mpango wa kuweka kwenye bajeti yetu, tutapata pesa ngapi kupitia *Sovereign Bonds* tutakazo-float. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyoangalia, kuna tatizo kubwa huku ndani ya Serikali huku, nalo ni tatizo la maamuzi. Pengine sijui ni kwa sababu ya hili wimbi la ujisadi ndiyo watu wanashindwa kuamua, sijui, lakini mimi nauita ugonjwa huo uliopo ni ugonjwa wa ‘*paralysis by analysis*’, sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu tafuta dawa na tiba ya ugonjwa huu wa *paralysis by analysis* ulioko huko ndani ya Serikali ili maamuzi yafanyike. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano mmoja tu wa suala la *mortgage financing*, tumelizingumzia sana. Tulikuwa tumeambiwa kwamba hili lingekamilishwa na lingeletwa sambamba na ile *Financial Bill* iliyoletwa katika Bunge lililopita, tumengojea lakini haikuja. Tukaambiwa itakuja kwenye bajeti hii, tunaambiwa bado, pengine kwenye Bunge lijalo, kuna nini huko? Nina hakika kabisa itakapokuja, hamna cha ajabu tutakacholetewa kwa sababu hii siyo *rocket science* hayo yatakayoleta hiyo Miswada, *amendments* au nini, ni mambo ya kawaida kabisa ambayo tunaweza tukayafanya maamuzi kwa haraka na tukatumia sheria hizi katika kujikwamua kiuchumi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, wasimamie wenzako. Naomba maamuzi yafanyike haraka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, uchumi wowote ambao hauna *mortgage finance*, una madhara makubwa sana katika uchumi wake. Nitoe mfano mmoja tu, sasa hivi inasemekana kwamba ziko nyumba zaidi ya 50,000 katika nchi hii ambazo zina zaidi ya miaka mitatu mpaka miaka mitano, watu wameshindwa kuzikamilisha. Kwa nini wameshindwa kuzikamilisha? Ni kwa sababu hawakuwezesha kupata mikopo ya miaka 20 mpaka 30 ili kuweza kuzikamilisha hizo nyumba za makazi au za biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii maana yake ni nini katika uchumi wetu? Mathalani kama nyumba moja tu mtu alikuwa amewekeza zaidi ya shilingi 30,000,000/= kwa hizi nyumba 50,000 ambazo hazijakamilika tuna shilingi trilioni 1.5 ambazo zinaitwa ni mtaji mfu (*dead capital*), haina faida yoyote katika uchumi wetu, sasa tutaendeleaje namna hii jamani? Ni lazima tuwe na uchungu na watu wetu. Kwa nini tumewafikisha wananchi wetu mahali ambapo wao wanajaribu sana kujikwamua lakini Serikali haifanyi kazi yake ya kuwasaidia ili wakamilishe nyumba zao na kujikwamua kiuchumi? Naomba ulivalie njuga suala hili Mheshimiwa Waziri Mkuu, ili tuondoe aibu hii katika nchi yetu.

*Mortgage Finance* ikamilishwe ili watu waweze kupata mikopo ya ujenzi wa makazi na nyumba za biashara ya miaka 20 mpaka 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kusema kwenye hili hili la mambo ya ujenzi wa nyumba kwa sababu sikuwa na matatizo hata kidogo, watumishi wa Serikali walipouziwa zile nyumba. Kwangu mimi niliona hiyo ndio njia ya ku-*empower* Watanzania, utawa-*empower* namna gani kama sio hivyo? Huyu Mtanzania, mtumishi, atawezaje kuwa na rasilimali *Oysterbay*, kama hawakusaidiwa na Serikali? Sisi hapa tumetunga Sheria ya makusudi kabisa ya *Economic Empowerment*, inanisikitisha sana kwamba katika bajeti hii kile kifungu cha *empowerment* tumetoa shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya *recurrent expenditure*, lakini pesa za kuwawezesha wananchi ni Sh.150,000,000/= peke yake, hii ni aibu! Hatuonyeshi *seriousness* katika kazi hii kubwa ya ku-*empower* Watanzania. Mheshimiwa Waziri Mkuu, lifanyie kazi suala hilo mtakapokuja kurekebisha bajeti tuonekane tuko *serious* katika azma yetu hii ya *economic empowerment* kwa Watanzania wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ninalotaka kulizungumzia kuhusu *General Tyre*, Arusha. Wamenituma nitoe shukrani zao za dhati kabisa kwa sababu hatimaye wameweza kulipwa mishahara yao baada ya muda mrefu sana. Hii ni jitihada za Mheshimiwa Waziri Mkuu, kutekeleza yale maamuzi yaliyofanyika mwaka jana na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyestaafu, Ndugu yangu, Edward Ngoyai Lowassa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonisikitisha ni kwamba imechukua muda mrefu sana kutekeleza yale maamuzi yaliyofanywa na Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa. Alifanya maamuzi mazuri sana akishirikiana na Mawaziri wenzake, Waziri wa Fedha na Waziri wa Viwanda na Biashara, wakaamua kwamba *General Tyre* lazima iendelee kuishi, ifufuliwe, isaidiwe ku-*play its role* katika uchumi wetu wa Tanzania. *General Tyre* walikuwa wana mpango mzuri tu, walikuwa wana mipango ya kuweza kuzalisha matairi kutoka 250 mpaka 1,000,000, walikuwa na mipango ya ku-*upgrade* uzalishaji wa matairi kuingia kwenye *radial tyres*, walikuwa wana mpango wa ku-*link* uzalishaji wa matairi na *rubber industry* yetu hapa Tanzania ili Muheza, Korogwe, Tanga, Morogoro na Zanzibar, waweze kuzalisha mpira kwa ajili ya kiwanda chetu cha *General Tyre* na pia kwa ajili ya kuuza nje. Tulikubaliana hiyo mwaka jana na Waziri Mkuu aliyepita, Mheshimiwa Edward Lowassa na namshukuru sana kwa kusimamia suala hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotusikitisha ni kwamba mpaka leo hii Serikali haijakamilisha sehemu yake ya makubaliano haya ya mwaka jana. Kinachonisikitisha zaidi, ni kwamba ni kama wamefungua tena majadiliano na hii inanishangaza mimi na inawashangaza wabia wenzetu kwamba je, kwa sababu tu ya mabadiliko ya uongozi ndio pia tunabertilisha makubaliano tuliyokuanayo?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba sana ulichukulie suala hili kwa uzito wake. Usikubali kuyumbishwa, tekeleza yale maamuzi mazuri ya kizalendo yaliyofanyika na yaliyofanywa na viongozi waliokutangulia. Hakikisha *General Tyre* inaendelea ku-

*survive*, ifufuke ifanye ili kazi yake, ichangie katika uchumi wetu hapa Tanzania na ishindane na hao wengine ambao walitaka kutugeuza sisi kuwa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, alifanyie kazi kwa nguvu zako zote suala hili vinginevyo hapa ndani hapa, kwa kweli, itabidi na mimi nianze kulia na mimi sipendi kulia, sio hulka yangu. Wengine wanasema hapatatosha, sasa mimi sijui niseme nini? Naomba msinifikishe huko. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine tulikuwa na *USR*, (*Urban Sector Rehabilitation Program*), iliingia kwenye miji yetu tukasema, *Alhamdulilah*, huu ndio mwanzo wa ku-rehabilitate miundombinu ya miji yetu. Pale Arusha, tulipata kilometa 20 za lami, tukategemea kwamba itakuja *USR number II, III, IV*, mpaka miji yetu yote iwe rehabilitated ifanane na miji. Hatujui ni nini kilichotokea, *USR 1*, ikafa, hatujasikia chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunachoona ni kwamba unakuja utaratibu mwingine tu wa kupeleka pesa kwenye Halmashauri zetu kwa ajili ya miundombinu. Wenzangu wamelalamika hapa hatuna *capacity* ya kusimamia hizo pesa zinazokuja na zikija sisi huku, wajua mkao wetu, tukae mkao wa namna gani, zitazama tu maana sisi ni wazuri sana wa kuzizamisha hizo hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba turudi kwenye ile dhana ya *USR* (*Urban Sector Rehabilitation Program*), tuzungumze na wafadhili, warejee kwenye dhana hiyo ili tuendelee na mpango ambao unaeleweka wa ku-rehabilitate miji yetu na *ikibidi tu-float Municipal Bonds* kwa ajili ya kuzibia hayo mapengo ambayo yataoonekana. Bila kufanya hivyo, tutakuwa tunatizamana tu hapa mwaka hadi mwaka na miji yetu itaendelea kuwa na sura hiyo ambayo inaendelea kuwepo ambayo ni mbaya sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kabla kengele nyingine haijalia, nzungumzie kuhusu kilimo. Huyu mkulima, wenzangu wameelezea vizuri sana, huyu mkulima tumemwonea sana, ni wepesi mno kusimamia mazao yake, ni wepesi mno kumwambia asiuze mazao yake nje...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. FELIX C. MREMA:** Hiyo ni kengele ya pili?

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**MHE. FELIX C. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi hii.

Awali ya yote, naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha siku ya leo kuweza kusimama hapa na kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaendelea, naomba nimuunge mkono Mheshimiwa Felix Mrema, kwa suala la *General Tyre*. Naongelea suala la *General Tyre* kwa sababu na mimi pia ni mhusika mmojawapo wa *General Tyre*. Aliyoyasema, ni kweli. Mheshimiwa Edward Lowassa, alitusaidia sana kwa kutoa mwongozo na taratibu ili kuisaidia *General Tyre* isiweze kufa, tunamshukuru sana na pia wafanyakazi wa *General Tyre* wanamshukuru kwa kuweza kuwasaidia ili kuweza kupata haki zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza moja kwa moja katika suala la barabara. Tabora ni Mkoa ambao una historia kubwa katika nchi hii, nina imani tunaisahau tu lakini bado katika nafsi zetu, katika kumbukumbu zetu, katika historia bado tunajua Tabora ina historia kubwa, Tabora imezaa viongozi wengi wa nchi hii. Waswahili wanasema, “*usimdharau mkunga wakati uzazi ungalipo*” na nina imani hili litatuingia katika miyo yetu. Kule ndio mlikotoka, ndiko historia ilipo, kura tatu zilipigwa Tabora mwaka 58, tunazikumbuka na hizo kura tatu, ndio kura ambazo zimetufikisha hapa, demokrasia ilianzia pale, tusicahau. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililingia Bungeni mwaka 2000. Tangu nilipoingia Bungeni mwaka 2000, nilikuwa nikilizungumzia suala la barabara. Wabunge wa Tabora wamelizungumzia, waliopo na wale ambao hivi sasa hawapo hapa Bungeni. Inasikitisha, inatia huruma, inaumiza roho na inatumiza sana sisi pamoja na wananchi wetu au wananchi wa Tanzania waliopo katika Mkoa wa Tabora, Kigoma, Mbeya na Rukwa kwa sababu sisi tumeunganika na tumepakana nao. Ni barabara ya kutoka Tabora – Itigi - Kigoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Waziri Mkuu au Waziri wa *TAMISEMI*, wakati akitoa majibu, atueleze sababu tano tu za msingi zilizofanya barabara hizi kutotengenezwa na kutotengewa pesa. Sitahitaji maelezo mengi, nitahitaji sababu tano tu na wananchi wanasubiri hizo sababu tano. Wakiambiwa sababu tano, nina imani wataridhika na watatulia na Wabunge wa Tabora na hata wa Kigoma, hatutahoji tena suala la barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka juzi niliuliza swali kuhusu barabara ya watumwa, nawashukuru sana *BBC* kwa sababu majibu yaliyotolewa, ilirusha matangazo yake. Wako Waafrika walioko katika nchi mbalimbali duniani, waliposikia redio *BBC* wakawa na shauku kubwa sana ya kujua barabara hiyo ambayo inaanzia Kigoma – Tabora – Rukwa - Dodoma - Bagamoyo. Baada ya kusikia hayo, wakafurahia kwamba mwaka 2009, tutapata wageni ambao watapita katika barabara hiyo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama hatujajiandaa kwa haya na wao wanakubali barabara ile iwe ni urithi wa Waafrika wote duniani, yaani iwe urithi wa kihistoria wa Waafrika duniani. Kwa maana hiyo, mnawaambia kwamba waje wakute ile historia ya utumwa na wao waje kuionja kwanza baadaye ndio barabara ipatikane ili wajue bado historia ya utumwa ipo katika barabara ile ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tubadilike, tuwahurumie watu wa Kigoma, Tabora na Rukwa angalau Rukwa wao wameanza kuguswaguswa, wanashukuru. Kwa hiyo, hawa wenzetu kidogo watakuwa na ahueni, wanakomboka lakini tunaomba sana barabara hii iweze kuangaliwa jamani. Naomba mtufikirie, mtuhurumie, nina imani zile sababu tano zitatolewa, nisiendelee sana, ninazisubiri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu reli, leo Mheshimiwa Waziri Mkuu, sijui anakumbuka, wakati anakuja Bungeni, pale kwenye maungio ya reli, treni ilisimama ili Waziri Mkuu apite lakini nilikuwa napenda sana gari ya Waziri Mkuu ingesimama halafu treni ingepita aone kile ambacho kimebebwaa mle ndani, mabegi yananning'inia kwenye madirisha na watu wananning'inia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina tatizo kuhusu kuingia ubia na Wahindi wale wa *TRL*. Tatizo langu ni kwa nini baada ya kuingia ubia, hali imekuwa mbaya zaidi kuliko Tanzania ilipokuwa inaendesa reli peke yake ina maana tukishaingia ubia, tunaachia moja kwa moja wao ili waiendeleze? Ninaomba twende *Railway Station*, siku ambayo treni inatokea Dodoma tukaangalie, hakuna haja ya kwenda Dar-es-Salaam, tukaangalie tu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ina utaratibu wa kazi za zimamoto, likishatokea jambo ndio inaanza tena vimulimuli na kila kitu vinakimbilia kwenye tukio ambalo linatokea. Tunakumbuka kuna tatizo la treni ambalo lilitokea, Mwenyezi Mungu aepushie mbali lisije likatokea, angalau tuliweza kujua idadi ya watu kutookana na siti namba na majina lakini sasa hivi ukienda kukata tiketi hakuna siti namba, wewe unapewa tiketi na zipo tiketi nyingine za kurusha pale pale, ili mradi tu tafrani, vurugu mech. Wanaoingia kwenye behewa hakuna mtu mwenye siti, anayewahi ndio kawahi kama India kule, sasa tusiibadilishe Tanzania yetu ikawa kama yale mabehewa yale ya India, nina imani, tuna haja ya kuboresha suala hili katika nchi yetu. Wale Watanzania hawajazoea matatizo hayo jamani. Wajue ya barabara, wajue na ya reli, hebu tuwfikirie! Tunasema tunaenda na *standard* na..., najua mmemalizia. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la Urambo, nalisema hili kwa sababu Mheshimiwa Spika, hatosimama hapa akasema, kuna Mheshimiwa Kapuya, hatosimama hapa akasema. Tabora sisi kuanzia Halmashauri ya Urambo, tukapeleka *RCC*, tukakubaliana kuwa Urambo, ipewe Wilaya mbili, Wilaya ya Urambo na Wilaya ya Kaliua kwa sababu vigezo vinavyohitajika viro kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Urambo, sehemu zote mbili kuna umeme, barabara za ndani zinajitosheleza, tunazikubali, kuna idadi ya watu wapatao 600,000, tunaweza tukaweka huku tatu na huku tatu, wakawa 600,000, wamekamilika. Vitalu tunavyo, Wilaya ya Urambo kwa Mheshimiwa Sita vipo, kwa Mheshimiwa Kapuya vipo, ambavyo vinaleta rasilimali katika nchi yetu. Hospitali tunazo, tena hospitali ya Urambo mjini ni hospitali nzuri sana, mwende mkajifunze tu jinsi tunavyoboresha pale. Hospitali ya Kaliua, ni hospitali ndogo, tutaiinua, itakuwa ni hospitali ya Wilaya, wananchi watapata huduma bila tatizo lolote. Haya sisi viongozi tunayasema lakini wanaohitaji Wilaya ni wananchi wenyewe. Tunaimani Serikali itakuwa sikivu, itazingatia maombi yetu ya kupitia Halmashauri zetu, *RCC* na wataweza kutekeleza yote. Tunawaomba sana wawe wasikivu kwa haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pesa za *JK*. Mwaka jana katika pesa za *JK*, ilitengwa shilingi bilioni moja kwa kila Mkoa lakini mimi nasema hizi pesa zilitengwa wakati wananchi walikuwa hawajaandaliwa. Unapoingiza pesa Benki, Benki inazunguka, wananchi wanaambiwa waende kuandaa mchanganuo, wanaambiwa mkajiunganishe huko muwe na *SACCOS*, pesa zimeingia Benki tarehe 20, mpaka wapate *SACCOS*, ni mpaka tarehe 20 mwezi ujao. Kwa utaratibu wa Benki, pesa zinavyozunguka tayari zinazaa, wananchi bado wanaendelea kuzunguka, mara hujaandika mchanganuo vizuri, peleka kwa Afisa Ushirika, anapeleka, anarudisha, mambo mchanganyiko tu, mwezi mzima umepita, pesa zinachelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazo langu ni kwamba kama ni shilingi bilioni moja kila Mkoa na shilingi milioni 500, unaweza kuanzisha Benki, kwa nini Mikoa yetu yote hii 26, nasemea ya Bara kwanza, ingeanzisha Benki za wananchi kila Mkoa na ile milioni 500 ingekuwa ni mwanzo wao wa biashara. Halmashauri zetu wanatenga 10% ambapo wanawake ni 5% na vijana ni 5% na wao wangkuwa wanaziingiza kwenye ile Benki ili kutoa mikopo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zile benki za Mkoa zingeanzisha matawi yao kwenye kila Wilaya, nina imani hizi pesa wananchi wale wa chini zingeweza kuwafikia vizuri sana. Kuliko ilivyo sasa ambapo mwananchi wa Igalula aende *NMB*, mwananchi wa Usisia kule Urambo, aende *CRDB*, Bukene kule kwa Mheshimiwa Teddy, wananchi watoke Bukene waende kwa Seleli kwa sababu kule hata *NMB* hakuna. Kwa hiyo, bado wale wananchi wanazidi kupata shida. Nina imani Benki ya Wananchi wa Mkoa wa Dar-es-Salaam, wameshaweka matawi angalau ni sehemu ya kwenda kujifunza. Tusikubali tu pesa zile zikae bure, tuziingize Benki wakati ile *capital* tuliyonayo tunaweza tukaanzisha Benki katika Mikoa. Nakumbuka Waziri wa Fedha, alisema kuna uwezekano wa pesa kuendelea kutolewa kwa wananchi ili mikopo ile izidi kuendelea kutolewa basi pesa hizi ziingizwe kwenye Benki za Mikoa yao. Nadhani hilo limesikika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *solar*, nilisema tuondoe kodi kwenye *solar* lakini matokeo yake tumeenda kutoa kdi kwenye Motopoa, hivi chungu cha ugali

kweli cha kilo tatu nitaenda kuweka kwenye Motopoa, wakati kale kajiko kenyewe ni kadogo? Wananchi wa kijiji ni maisha ya watu wengi, nyumba moja wanaishi watu 15, 20...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na ninapenda niseme tu kwamba itifaki imizingatiwa, naomba nianze. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, wakati tunachangia hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mbunge mmoja wa Upinzani alisema, Wabunge wa CCM hawako pamoja, wana mgawanyiko. Nataka niwathibitishie Watanzania na wanachama wa Chama cha Mapinduzi wenzetu walioko huko nje, Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, tuko pamoja, tuna mshikamano mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uthibitisho wa hili ni huu, wakati tunapiga kura za kuunga mkono au kutounga mkono hotuba ya Waziri wa Fedha, Wabunge wote wa Chama cha Mapinduzi, walisema ndiyo wakati Wabunge wa Upinzani, wengine walisema hawako upande wowote na mwingine akaunga mkono, hili linaonyesha dhahiri kwamba CCM tuko pamoja na wao ndio wamegawanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea suala hilo, nataka nianzie na suala la ufisadi. Anayesema kwamba tukija hapa tusizungumzie habari za ufisadi kwa sababu Ilani ya Uchaguzi inazungumza tu habari ya maji, sijui barabara, nafikiri hajaismwa vizuri Ilani hiyo. Ukifungua Ilani ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 135, kifungu cha 110 (a) na (b) vinasema, naomba ninukuu:-

*“kuendelea kuchukua hatua za kisheria, kiutawala na kinidhamu, kwa wale wote watakaobainika kuhusika na vitendo vya rushwa. Kujenga mazingira mazuri zaidi yatakayowapa wananchi uwezo, ari na ujasiri zaidi katika kupambana na rushwa, wizi na ubadhirifu wa mali ya umma”.* Mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapofika mahali una miradi ya maji, una miradi ya barabara halafu unaruhusu watu wanaiba fedha za umma, hiyo miradi itatengenezwa na fedha gani? Kwa hiyo, lazima tukemee kwa nguvu zetu zote ubadhirifu wa fedha za umma na kwa hapa, tunakemea kwa jina la Chama cha Mapinduzi. Kama hutaki

kusemwa, usiibe, kama hutaki kusemwa, usijiingize katika mashaka mashaka ya rushwa, kaa katika misingi ya uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanatusikiliza, mimi nimetumwa na wananchi wa Sikonge, ndio mabosi wangu, bosi wangu mwagine, ni Chama cha Mapinduzi, ndio wamenileta hapa. Hivi mimi nikija hapa, nikizungumza mambo ambayo hayana maslahi na wananchi wangu, kwanza ni kujidhalilisha, lakini naonekana nimewasahau wapiga kura wangu na kwamba hapa napo Bungeni kuna Jimbo lingine ndio linakutuma ufanye kazi. Huku ni kujidhalilisha wewe mwenyewe na kuwadhalilisha wapiga kura wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu tunaenda Misikitini, watu tunaenda Makanisani, watu tumekuja humu kwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, tuseme kweli. Pale ambapo kuna makosa, tuseme kweli, tutaendelea kutetea Ilani ya *CCM*, tutaendelea kusema pale ambapo mtu amekosea, awe anatoka Chama cha Mapinduzi, awe anatoka Upinzani, hapa hatuna sababu ya kumuoneea mtu aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kuzungumzia matatizo ya wananchi wa Sikonge. Tuna uhaba mkubwa sana wa watumishi. Naomba Mheshimiwa Waziri wa *TAMISEMI*, umeshafika, hata mnapopanga watumishi mnajua mkitupangia Sikonge watumishi 20, 10 hawatakuja, pangeni watumishi 40...

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kuhusu utaratibu

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Wangwe.

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68, nazungumzia Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inasema kwamba:-

“*Mbunge, hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli*”.

**MWENYEKITI:** Kanuni ya 68, kipengele cha ngapi?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Kanuni ya 68 yenyewe inaniruhusu kusema kuhusu utaratibu halafu nina *refer* Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inasema kwamba hatatoa ndani ya Bunge, taarifa ambazo hazina ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nina...

**MWENYEKITI:** Una *refer* Kanuni ya 62 au 64?

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64.

Mheshimiwa Nkumba, amesema kwamba Wabunge wa *CCM* hapa ndani wao wameungana na ni kitu kimoja na kwamba Wabunge wa Upinzani, ndio wamegawanyika. Lakini katika *statement* yake iliyofuata, amevuta Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kuwakemea Wabunge wa *CCM* ambao wanassema tusijadili ujisadi na amesema ni muhimu tujadili ujisadi, kwa hiyo, hapo tayari kuna *contradiction*, inaonyesha kwamba kuna mgawanyiko. Kwa hiyo, mimi nilitaka a-*observe* kwamba hapa ni sehemu ya kuonyesha mgawanyiko wa mawazo, ndio maana ya Bunge, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, namwomba Mheshimiwa Chacha, anapozitumia hizi Kanuni, aelewe maana ya Kanuni na tukio halisi ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Chacha, unachokisema, kwa kweli unavunja Kanuni ambayo inatukataza kuchelewesha shughuli za Bunge ndani ya Bunge kwa sababu alichokisema Mheshimiwa Nkumba, ni kudhihirisha, kwa sababu unatakiwa udhihirishe uwongo ambao upo, Nkumba amedhihirisha kwa kusema kwamba hawakugawanyika kwa kutoa mfano wa kupiga kura zote za ndio kwenye bajeti na ametoa mfano halisi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Chacha, kwa kweli anatuchelewesha, namwomba Mheshimiwa Said, aendeelee. (*Makofi*)

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba dakika zangu ziendelee na huyo ndio Chacha Wangwe. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Nitazingatia hayo Mheshimiwa Mbunge, naomba uendeelee.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasisitiza suala la watumishi. Mnapotupangia watumishi katika maeneo ambayo mnajua watumishi wote wanaopangwa katika maeneo yale nusu yao hawatafika, tupangieni ziada!

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Mahakama ya Wilaya. Wananchi wa Sikonge, wanapata shida sana na hasa kwenye ngazi ya Mahakama ya Wilaya. Kesi zinazoamuliwa kwenye Mahakama ya Mwanzo, zinapopata rufaa kwenda kwenye Mahakama ya Wilaya, tunapata matatizo makubwa na wananchi wengi wanapoteza haki zao. Kwa hiyo, naiomba Serikali kwa kweli ilitizame jambo hili, tuna Wilaya ya Sikonge tayari, tuna Mkuu wa Wilaya, tuna Mkurugenzi, tuna Halmashauri, tunaomba kabisa tuhakikishiwe kwamba Mahakama ya Wilaya nayo inakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni sambamba na suala la Polisi. Yuko Polisi pale *OCD*, lakini tuna cheo tu cha *OCD* pale, hana vitendea kazi. Nilikuwa ninaomba sana

suala hili Serikali ilizingatie kabisa kuhakikisha kwamba *OCD* aliyepo Sikonge anapata vitendea kazi vya kutosha ili aweze kufanya kazi yake kama *OCD* wa Wilaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalofuata sasa ni suala la kilimo. Suala la mbolea, kwanza tumeshabitishiwa kabisa kwamba mbolea inayoagizwa kutoka nchi za nje na inayozalishwa nchini haitoshelezi mahitaji ya wananchi wetu. Sasa nilikuwa ninaomba, maana hata kama ingekuja mbolea yote ikatosheleza mahitaji kwa gharama zilizopo sasa hivi za mbolea, wapo wananchi ambao wangeshindwa kununua mbolea. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Serikali kwa kweli iwekeze katika suala hili la kuhakikisha kwamba huduma hii ya mbolea inapata unafuu, gharama zake zipungue ili wananchi wetu waweze kupata nafasi na uwezo wa kununua mbolea kwa gharama ya chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mbolea ya ruzuku, mimi ni mmoja wa watu ambao kwa kweli wanapingana kabisa na wazo la Serikali la kugawa mbolea ya ruzuku kwa baadhi ya maeneo tu hapa nchini. Huu ni ubaguzi na hauwezi ukaendelea kuvumiliwa. Huko mwanzo tulisikia kwamba mbolea ya ruzuku inapelekwa katika baadhi ya Mikoa kwa sababu ya kukuza uzalishaji, lakini baadaye tumepata taarifa kwamba huko inakopelekwa mbolea ya ruzuku wanakwenda kupewa watu wasio na uwezo. Hivi watu wasio na uwezo Tabora hawapo? Singida hawapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunasema, kama hamwezi kusambaza mbolea ya ruzuku nchi nzima, acheni. Wakati Mheshimiwa Rais anapita huko kunadi Ilani ya Uchaguzi, suala la mbolea ya ruzuku liko humo na wananchi walisikia. Sasa leo mnapeleka baadhi ya maeneo, maeneo mengine tuendelee kununua mbolea kwa bei kubwa. Hatukubali jambo hili! Ninaiomba Serikali itafute utaratibu wa kuhakikisha kwamba tunateremsha gharama za mbolea ili wananchi wote wanunue mbolea kwa gharama nafuu bila kubagua maeneo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka kwenye maeneo yanayolima tumbaku na vilevile nataka tu niseme kwamba mimi ni Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku. Kwa hiyo, niiombe Serikali, wakulima wa tumbaku wana tatizo kubwa moja, wanaendelea kulima kwa kilimo cha mkataba. Kilimo hiki cha mkataba ni kilimo kinachomfanya mkulima aendelee kulima kwa kukopa. Kule unakokopa, huko huko ndiko unakouzia tumbaku. Sasa mkulima wa tumbaku amefungwa. Kwa hiyo, Bodi, Serikali kwa ujumla, wanaushirika pamoja na wakulima tumeamua tutafute namna mbadala. Kwenye hili, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, anatusaidia sana. Tutafute suala mbadala la kuondokana na suala la kuwakopa watu ambao tunawauzia tumbaku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabenki yapo yaliyokwishajitolea kwa mfano *CRDB*, lakini tunaomba, kwa sababu tunalo deni la karibu Shilingi bilioni 1.8, tunaiomba Serikali, haya makampuni wanayosema mkitaka kuachana na sisi tulipeni deli letu. Sasa Serikali tunaiomba kama mlivyofanya huko kwenye pamba, kwenye korosho, fanyeni na kwenye tumbaku. Tulipeni hili deni tuondokane na hawa ili tuendelee kulima vizuri na kwa faida kubwa. Shilingi bilioni 1.8 najua Serikali ina uwezo, inaweza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu barabara, wamesema wenzangu, nami ninarudia, nimeingia mwaka 2000, hapa tulikuwa na Mheshimiwa Magufuli, Mheshimiwa Mramba, Mheshimiwa Chenge, hawa wote walituambia tuishi kwa matumaini. Barabara hakuna mpaka leo! Sasa amekuja Mheshimiwa Shukuru Kawambwa, inawezekana yeye akatuambia tumshukuru Mungu. Kwenye hili, hatukubali! (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu Tabora, kule huna sababu ya kufanya mazoezi asubuhi. Yaani wewe kama una ziara, ukiingia kwenye gari, ukirudi, tayari umefanya mazoezi kwa sababu ya mashimo. Mimi kwa kweli kama kulikuwa na uwezo wa kuhamisha Serikali, tungepeleka Serikali hata wiki mbili mkae Tabora mwone.

Hali ni mbaya, wananchi wanapata shida, watumishi masika wanapata shida, barabara zote Kaskazini, mnakuwa kama Waislam. Sisi Waislam wakifunga, ibada ni Kaskazini tu, hata uwe wapi! Jambo hili haliwezi kuvumilika. Tunahitaji barabara na hii siyo hisani. Sasa na sisi tunahitaji barabara, tena za lami. Leo nikimtoa mtu Urambo, hata Mpanda, Sikunge, nimpeleke Kaskazini, anaweza akang'ang'ania huko asirudi. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mnatupangia na watumishi. Mtumishi akija tu mara moja anaangalia barabara. Atakaa kule! Tunahitaji barabara. Mheshimiwa Kawambwa, kwa kweli kama alivyosema Mheshimiwa Selelii, ajiandae. Kwenye hili hatuna mchezo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli mimi sipendi nigongewe kengele, lakini nataka nimalizie. Hii reli ya kati ya kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora mpaka Kigoma na ile ya kwenda Mwanza ndio inayotusaidia. Sasa barabara hamtupi, hata reli! Hivi sisi tukose vitu vyote! Hapa kwenye reli, jamani, nasema, kama kuna uwezekano, siku moja hebu twende pale tukaone wananchi wetu wanavyopata shida Stesheni. Humo humo mtu anaingia na mizigo na watoto, huna nafasi hata ya kutoka. Ninaomba hii adha tuiondoe, tushirikiane na sisi tunataka kwa kweli tupige hatua za maendeleo kama wanavyopiga hatua maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naomba nichukue nafasi hii sasa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niliona nisianze na pongee maana dakika zangu zingeweza kwisha. Sasa nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, nawapongeza Mawaziri, Mheshimiwa Kombani, Mheshimiwa Philip Marmo na Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Hawa Waheshimiwa Mawaziri wote ukiwaangalia ni watu waadilifu, wachapa kazi, hatuna mashaka nao. Sisi tunawaunga mkono sana katika kazi zao za kila siku. Wamepewa majukumu makubwa na mimi nina hakika tutawasaidia kutekeleza wajibu wao. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa nami niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyoiwasilisha hapa Bungeni kwa ustadi na ufasaha mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba kumshukuru sana Mheshimiwa Spika, vilevile Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi wa Tanzania walioniombea sana nipone haraka baada ya kuugua ghafla hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuugua kwangu kutiwa chumvi sana kiasi cha baadhi ya watu kusambaza uvumi kwamba nilikuwa mahututi na nimefariki dunia, naomba tu kusema, ninamshukuru Mungu, mimi ni mzima wa afya. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema mwaka huu maeneo mengi ya Nyanda za Juu Kusini yalipata mvua nyingi sana na kusababisha maji mengi sana kuanza kutiririka kuelekea kwenye maeneo yaliyo chini na Wilaya ya Kyela, ndiyo sehemu iliyochini katika Nyanda za juu Kusini na huko huko Kyela mvua kubwa zilikuwa zinanyesha vilevile.

Mheshimiwa Mwemnyekiti, matokea yake, mito mikubwa minne inayopita Kyela kwenda kumwaga maji yake Ziwa Nyasa ilifurika, Mto Lufilyo, Mto Mbaka, Mto Songwe na Mto Kiwira. Tukapata mafuriko makubwa sana ambayo yaliharibu miundombinu ya Kyela, mashamba ya watu, mali, mifumo ya maji na kadhalika na vilevile kusababisha vifo vya wananchi sita wa Kyela na kusababisha mserereko wa ardhi ambaao ni *land slide*, sijui tafsiri hiyo kama ni sahihi, ambayo imemega kipande cha milima ya *LivingStone* na mawe yake yale mazito yakaserereka na kuporomoshwa kuingia kwenye kijito kidogo kinaitwa Mwalisi ambacho kilikuwa na ukubwa kama wa mita tatu tu, lakini sasa hivi kimepanuliwa, kina zaidi ya upana wa mita 80.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina wasiwasni kuwa kipindi cha mvua za masika, kwa kweli kipande hiki cha barabara cha Kikusya hadi Matema hakitapitika. Kitaikata kabisa sehemu yote ya Wilaya ya Kyela na hospitali muhimu tuliyonayo Kyela ya Matema, ambayo inategemewa na watu wengi sana.

Hivyo nilikuwa ninaiomba sana Serikali iongeze kasi ya mchakato wa ujenzi wa barabara hii ambayo ni sehemu ya ahadi ya Rais:- kujengwa barabara hii kwa kiwango cha lami. Tayari upembuzi yakinifu umefanya, kwa hiyo, ujenzi wa barabara hii kwa haraka utawasaidia sana wananchi wanaoishi katika Kata sita za Kyela ambao wanasumbuka sana na usafiri na sehemu hii yenye ukorofsi kuweza kurekebika: Kata za Matema, Makwale, Lusungo, Ipinda, Ikama na Mwaya. Wananchi wanateseka sana kutokana na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi karibu 40,000 walioathirika na mafuriko, ninaomba niishukuru Serikali hapa kwa chakula tulicholetewa cha msaada. Aidha, ninawashukuru Wabunge wote kutoka Mkoa wa Mbeya wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Gideon Asimulike Cheyo - Mbunge wa Singida Mjini - Mheshimiwa Mohammed Gullam Dewji, wafanyabiashara, Ndugu Mohamed S. Nassor,

Ndugu Rashid Amour Rashid na Ndugu Mohamed Abdullah wa *Scandinavia Express*, *NGO ya Friends of Tanzania*. Shule ya *Heaven of Peace Academy* ya Dar es Salaam, *Kyela Development Fund*, *NGOBE Group* ya Kyela na *Lucy's Hope Centre for Orphans* ya Rungwe kwa misaada ya hali na mali tuliyopewa wananchi wa Kyela kutokana na tatizo hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii vilevile kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa - Mheshimiwa Dr. Hussen Ali Mwinyi na Naibu wake na viongozi wote wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania JWTZ kwa kusikia kilio cha wananchi wa Kyela cha muda mrefu kuhusu daraja kwenye Mto Lufilyo, sehemu tata ambayo ilikuwa inalazimisha wananchi, watoto kwa wazee, walemaavu kwa wajawazito kuvuka kwenda upande wa pili kwa kuning'inia kwenye kamba na hata Mbunge mnayemwona hapa, nilishapa ustadi wa kwenda sehemu ya pili kwa kuvuka hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja hilo la vyuma ni ukombozi mkubwa kwa wananchi wa Kyela. Nina maombi mawili tu kwa Waziri Mkuu kuititia kuititia kwako. Ombi la kwanza, tumeambiwa kwamba daraja hilo ni la muda tu, litaondolewa baada ya miezi tisa. Naomba hapa tuelewane vizuri. Mling'oe kwenda wapi? Hivi jamani hamwelewi kwamba kuling'oa daraja hilo na mimi ndio mnaning'oa Ubunge? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba baada ya kilio changu hapa kuhusu sehemu hiyo, Serikali ikaamua kutujengea daraja wananchi wa Kyela na tayari tumetengewa Shilingi milioni 50 kwa ajili ya upembuzi yakinifu. Mimi ninaiomba Serikali, hiyo shilingi milioni 50 tuirejeshe Serikalini na pesa yote iliyotengewa kwa ajili ya daraja hilo nayo wapewe Jeshi la Wananchi wa Tanzania wanunue daraja lingine la vyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaku hakikishia, tukishafanya hivyo, Jeshi litafurahi, wananchi wa Lusungo ambao wamehanganya sana na hiyo sehemu na vilevile wamesaidia kubeba vyuma hivyo kujenga lile daraja watafurahi sana na mimi Mbunge nitafurahi kwa sababu nitabakia kuwa Mbunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili. Nimevutiwa sana na *style* ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ya utendaji kazi, tena kazi ya uhakika. Ujenzi wa daraja tuliozoea na makandarasi wetu wa kawaida unachukua miaka miwili, mitatu na hata minne. Wataanza na upembuzi yakinifu, mara sijui kupima ardhi. Itachukua mwaka, miaka miwili, mitatu. Lakini kwa Jeshi, makamanda wetu wamekuja pale, yote hayo ya upembuzi yakinifu yalichukua siku moja. Ujenzi wa daraja umechukua siku tatu na daraja liko imara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kutokana na hali hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu akihamishe Kitengo cha Maafa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu kiende Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Ninasema hivyo kwa sababu uamuzi huo utaondoa ukiritimba na ule urasimu wa kiraia uliopo kwenye kile Kitengo cha Maafa. Wanajeshi wanaitikia

mara moja, wamezoea. Tena hicho kitengo kiundiwe shirika, *a corporation and sole*, chini ya Jeshi na kiwe *constituted* na wanajeshi wastaaafu. Ninasema hivyo kwa nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanajeshi wetu hatuwaandai. Wanastaafu wakiwa watoto wadogo sana na ujuzi mkubwa kichwani. Wanaishia kufanya kazi za kuwadhalilisha, za ukolokoloni kwenye mabohari, sijui wapi, kanali mzima! Hiki kitengo kiundwe, kiweze kuwachukua wanajeshi wote wastaaafu watusaidie kwenye masuala ya maafa. Tukifanya hivyo, tutakuwa tumewalindia heshima wanajeshi wetu wanaofanya kazi nzuri sana nchini hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inastahili pungezi kwa kusikia kilio cha muda mrefu cha Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuboresha posho za Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninasema sitaki kuongeza zaidi kwamba Wabunge tunasubiri kwa hamu. Tumeambiwa kuhusu Miswada ya Marekebisho ya Sheria kuwawezesha wenzetu Madiwani kupata matibabu kuitia Bima ya Afya na vilevile kuweza kupata misamaha kwa ajili ya usafiri, ufanisi kwenye Halmashauri zetu, nina uhakika kutokana na maamuzi haya, utaongezeka mara dufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nina taarifa ya kuanza kwa utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi za mazao. Nimefurahi sana kusikia Kata ya Ipinda, Kyela imo. Mfumo huu utawasaidia sana wananchi, wakulima kupekana na *middlemen*, walanguzi ambao wanakuja, wanawajua tu wakulima hawa wameishiwa, na wanununa mazao yao kwa pesa ya chini sana. Kyela imefika mahali wanununa hata mpunga ambao bado uko shambani kwa pesa ya kutupwa. Ninaomba Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mfumo huu ili sehemu nyingi zaidi zinufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 76 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukisoma hapo unamkuta Mheshimiwa Waziri Mkuu anatujulisha kwamba Tanzania imependekezwa kuwa Makao Makuu ya Kamisheni ya Kiswahili ya Afrika Mashariki na kututia moyo kuwa Tanzania ni mama wa Kiswahili. Hivyo, tunatakiwa kwa kweli tuzalishe zaidi wahitimu wa Kiswahili na tuandike vitabu vingi vya Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Waziri Mkuu wetu ni njema sana, lakini ninajua itasahauliwa na Watendaji wetu mara tu baada ya kumaliza Bunge hili. Ninasema hivyo kwa nini? Sisi huko nyuma tulikuwa kweli mama wa Kiswahili katika Afrika na katika dunia, lakini katika miaka ya 1970 kutokana na sisi Watanzania kujua kuongea sana kuliko vitendo, Kenya ikatupiku.

Leo hii Kenya inazalisha wahitimu wa Kiswahili zaidi ya 2,100 kwa mwaka, sisi kwa kujitahidi sana tena sana tunazalisha wahitimu 700 wa Kiswahili kwa mwaka. Nilitaka hii picha Mheshimiwa Waziri Mkuu aisikie na ninataka watendaji waisikie rai ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuifanyia kazi kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wenzetu Kenya hawatoi Shahada hiyo ya Lugha. Sisi tunatoa *a general degree*, inakuwa ni *BA* ya Lugha humo humo umesomea

Kiswahili. Kenya ni *Degree* ya Kiswahili. Ni *BA* ya Kiswahili au *Masters in Kiswahili* mpaka *PHd* ya Kiswahili. Sisi tunategemea kufanya hivyo kuiga utaratibu huo wa Kenya, pengine baada ya mwaka mmoja. Lakini nadhani tunahitaji kuvisaidia Vyuo vyetu Vikuutuweze katika hili eneo na sisi tukajidhatiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia kengele ya mwisho ikipiga.

**MWENYEKITI:** Ni ya kwanza.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Ni ya kwanza! Pengine nimalizie kwa kuongelea suala moja linalonikera kidogo. Kumekuwa na michango kadhaa hapa ya Waheshimiwa Wabunge ikijaribu kukosoa kwa ujanja ujanja maamuzi yaliyofanywa na Bunge hili kuhusu *Richmond* na vilevile kumekuwa na *attempt* ya kutaka kusafisha baadhi ya watu waliotajwa ndani ya ile ripoti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine baadhi yetu hatuelewi, pengine tunadhani maamuzi yale yalikuwa ni maamuzi, mpaka leo ni ya Mwakyembe, Selelii, Manyanya, Mntangi na Mnyaa. Hapana! Yale ni maamuzi ya Bunge! Siyo maamuzi ya Mwakyembe tena! Kwa hiyo, tunapokaa hapa kukosoa maamuzi ya Bunge, tunajidhalilisha sisi wenyewe. (*Makofi*)

Tulianza kupata heshima kubwa sana kwa wananchi hapa. Heshima hii imeanza kupotea kwa ajili ya kuja hapa badala ya kupigania kuhusu matatizo chungu nzima katika Majimbo yetu, tuko *busy* kusafishana. Unamsafisha nani? Nchi hii siyo ya mabwege bwana! Watu wanaelewa! Utasafisha kitu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *there must be a finality in our deliberations*. Ndiyo maana hiki kitabu, katika Kanuni ya 53 na 54 kwa kifupi:-

*“Mbunge ye yeyote haruhusiwa kufufua jambo lililokwishaamuliwa na Bunge ama katika Mkutano huo uliopo au uliotangulia.”*

Kanuni ya 54 inasisitiza tu hayo. Nini sasa tusizidi kuendelea kila siku na malalamiko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Kiti chako kinaruhusu hizo *discussions* hapa, mimi ninatoa pendekezo. Kama kuna Wabunge hawajaridhika na maamuzi ya Bunge kuhusu *Richmond*, ninakuomba Mwenyekiti tutengue vipengele vya 53 na 54, hilo suala lije tena hapa Bungeni, waliyosahau kuyasema wakati huo wayaseme sasa. Hatuwezi kuwa Bunge la kila siku kuoendesha malumbano utafikiri sio watu wazima! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba waseme yote hapa tulipo na sisi turuhusiwe, tuliokuwa Kamati Teule, tuseme yote hata yale ambayo hatukutaka kuyasema kulinda heshima ya Serikali yetu. Mimi nataka niseme hapa, maana

tumechoka na maneno haya ya pembeni, hayana maana. Mara magazetini, sisi tumechoka! Tusonge mbele na matatizo ya Tanzania sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naapa na kwa niaba ya wenzangu, tukikuta tulimwonea mtu ye yote hapa katika hiyo kesi ya *Richmond*, sisi tunajiuzulu Ubunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini tukidhibitisha kwamba wote walijotajwa wanahusika, nao wajitoe kwenye kila nafasi walijonayo katika Serikali ya nchi hii. Hatuwezi! Hili Bunge lina heshima yake! Tunaamua kitu halafu tunarudia yale yale, tutaheshimikaje huko nje? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana *Dr. Harrison Mwakyembe* na hasa kwa msisitizo wako. Basi, naomba sasa nimwite Mheshimiwa *Dr. Binilith Satano Mahenge* na kama muda utaturuhusu nitamwita Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENG:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kupata nafasi hii na kwanza nataka kuchukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Hotuba yake nzuri na labda ni *underscore* kwamba tunasema ni hotuba nzuri kwa sababu ni hotuba yake ya kwanza ya Bajeti akiwa Waziri Mkuu, kwa hiyo tunampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala wangu unaanzia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na hasa ukurasa wa 30, ukurasa wa 85 na ukurasa wa 86. Kwenye ukurasa wa 30 anaelezea usimamizi mzuri wa fedha ambazo zimepangwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za vijijini. Lakini kwenye ukurasa wa 85 anaelezea hilo hilo kwamba kama tukisimamia vizuri hizi fedha, basi tunaweza kupata malengo ambayo tumejiwekea na ukurasa wa 86 anaelezea changamoto ya kulinda uchumi unaokua hasa kwenye matatizo haya ambayo bei za mafuta zinapanda wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wataalam ambao wanasema kabisa na wazi kwamba utawala bora ni sawa sawa na *anticorruption*. Kwa hiyo, ukiweza ku-control corruption katika nchi ikawa *minimum*, yaani utakuwa umejijengea mazingira ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kuleta hapa, ni hoja ambayo amei-rise Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba ipo haja ya kuwa na mjadala kuhusu kuhamia Makao Makuu Dodoma. Ni ya msingi kwa sababu miaka mingi imepita halitekelezeki au linakwenda taratibu mno. Sasa kwa hoja hiyo nilikuwa ninamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye bajeti ijayo aongezee hoja ifuatayo ya mjadala wa Kitaifa kuhusu Utawala Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo na uchumi wa nchi yoyote yanategemea sana utawala bora wa nchi hiyo na katika utawala bora, tunaona kwamba viko vipimo vyake. Viko vipimo kama sita nitavitaja baadhi.

Kipimo cha kwanza cha utawala bora ni namna Serikali inavyoweza kusimamia sera ilizotunga jinsi zinavyoweza kutekelezwa, kwenye sehemu za Halmashauri wanasema ni *government effectiveness*. Lakini kipimo cha pili cha utawala bora ni namna hali ya kisiasa ilivyo katika nchi ile, wanasema ni *political instability and violence*. Kipimo kingine cha tatu ni jinsi utawala wa sheria unavyotekelawa katika nchi ile, ni *rule of law* na cha nne, ni namna Serikali inavyoweza ku-control corruption na cha tano, ni namna Serikali inavyoweza kuvisimamia na kuona vile vyombo vya *regulatory* kama TCRA, EWURA wanafanya kazi yao vizuri. Kwa hiyo ni *regulatory burden*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kujikita zaidi hapa ni kuhusu usimamizi wa matumizi ya hizi hela ambazo zimepangwa, ni kidogo ambazo tunasema hazitoshi. Lakini: Je, tunazitumia vipi? Ninasema kwamba, kama ni kufanya maamuzi, basi tufanye maamuzi sasa hivi ya kuamua namna ya kusimamia haya matumizi ya hizi fedha tulizonazo.

Ninayo mifano, wenzetu wa huko Chuo Kikuu *Harvard* walifanya *research* wakasema kwamba kama ukiweza kui-control corruption iliyoko Mexico ukalinganisha na *corruption* iliyoko Singapore, basi utakuwa umeiongezea Mexico revenue ya asilimia 20. Lakini wenzetu wa Urusi waliona kwamba asilimia hiyo 20 ambayo inapotea kwa sababu ya *bribes* na vitu vingine vya rushwa, basi ingeweza kuleta *a lot of trillions* za hela zao na ambazo zingekuwa ni bajeti ya Wizara kama tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kama wenzetu wako mbele katika ku-control corruption na sisi tumejithadi. Kwa hiyo, inawezekana na sisi haiwezi tukawa chini ya asilimia 20, kwa aina ye yeyote ile tutakuwa kati ya 20 au 30 na hiyo ni kama tunapoteza hela nyingi sana. Nlikuwa najaribu kufanya hesabu hapa kwenye mapato ya Waziri wa Fedha na Uchumi ya *revenue* ambayo ni Shilingi trilioni nne, ukichukua asilimia 20 ni karibu Shilingi bilioni 800 na hii tayari ni bajeti ya Wizara ya Afya katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani zipo juhudzi za makusudi ambazo tunamwomba Waziri Mkuu azifanye ili kuzuia tatizo hili la rushwa ambalo linatumeza na nadhani ndio mchwa mkubwa. Hebu tuangalie, kwa mfano leo katika manunuzi ya Halmashauri zetu tunajenga sekondari, kwa hiyo, kule kunatokea *over estimate*, ubao ambaou ungeuzwa Sh.3,000/= wanakuandikia kwenye BOQ 5,000 kwa hiyo, uchukue hizo mbao zote kwa Shule zote za Sekondari ulizojenga katika Wilaya yako uzidishe na Halmashauri nyingine, utaona ni kiasi gani cha pesa ambacho tunapoteza kwenye ku-over estimate mambo ya manunuzi. Uende hivyo hivyo kwenye mafuta, uende hivyo hivyo kwenye vyombo vya usafiri, utagundua ni fedha nyingi sana ambazo zinapotea.

Kwa hiyo, nadhani ipo hoja ya msingi ya kuona ni namna gani Serikali inaweza ikaonyesha *competence* yake ya kusimamia hasara, lakini vilevile kusimamia utekelezaji wa hizi sera ambazo zinalenga kwenye matumizi bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulinda uchumi wetu, najaribu kujiuliza kwamba hivi leo hii bei ya *diesel* ni Sh. 2,000/= pale Iringa Mjini, nadhani hata hapa ni kama Sh. 1900/= na sisi hatupangi hiyo bei ya *diesel*, wanaopanga ni wale ambao wanazalisha hayo mafuta. Hivi tukiamka kesho wakafanya kama walivyofanya huko miaka ya nyuma ya 1973 ambapo waliongeza bei ya zile *bare* kutoka dola nne mpaka kumi na mbili, kesho tukaambiwa *diesel* lita moja ni Sh.50,000/=, ni gari la nani litakwenda barabarani kesho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inajiandaa vipi kulinda uchumi wake katika mazingira haya ambayo bei ya mafuta inapanda bila sisi kushirikishwa? Sasa najiuliza, ni kwa nini Serikali inapata kigugumizi cha kubana matumizi?

Kwa mfano Dar es Salaam kwenye Wizara hizi kubwa, tunayo matumizi makubwa ya hayo magari ya VX. Hivi kuna sababu gani ya VX kutumika Dar es Salaam? Kwa nini tusitumie magari madogo ambayo Kiongozi yeoyote anaweza akafika kazini bila matatizo na hivyo tukabakiza magari machache kama VX nne au tano kila Wizara ambazo zitakuwa zinakwenda Mikoani ambapo ndiyo kunahitajika magari kama hayo kufika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule tunaangalia wenzetu wa *Denmark*, ukienda kule unakuta baiskeli nyingi sana, lakini hii inatokana na wakati ule bei ya mafuta ilivyopanda wakaamua kutumia baiskeli. Kwa hiyo, pendekezo langu hapa ni vilevile katika kuboresha barabara Dar es Salaam, wahakikishe wanaweka na *lane* za barabara za baiskeli ambazo zinaweza zikatumika na watu wengi ili kufika makazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu nadhani basi ipo haja ya kuanzisha *ant-corruption operation* kwa sababu wenzetu wa Italy walipofanya *ant corruption operation* ambayo walikuwa wakiita “*free hand*” walikuja wakagundua kwamba kwenye sekta ya ujenzi walipunguza matumizi kwa kiwango cha asilimia 20. Kwa hiyo, nadhani ipo haja kabisa ya kulifanya kazi suala hili la rushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili ninataka kuelezea kuhusu barabara za Makete. Kwanza, natoa shukrani zangu nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jinsi alivyolipokea na kuliona tatizo hili la Makete nataka kuwahakikishia wananchi kwamba kwa kweli tunachotaka sasa hivi ni kuungana mkono na Serikali yetu ili waweze kutekeleza hizi ahadi ambazo zipo.

Kwa mwaka huu tayari Makete kwa bajeti ya Mkoa tunaanza kujenga lami kilomita 2.5 kutoka Njombe, Makete mpaka Kikondo. Ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kama alivyokuwa ameahidi, kwamba, basi waongeze nguvu kwenye hii bajeti ya mkoa ili angalau zifanyike kilomita 10 angalau kila mwaka zinaweza zikafika mbali badala ya hizi kilomita 2.5 ambazo ni kwa uwezo wa Mkoa wetu wa Iringa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile nilitaka tu kuona kwamba wakati tunapanga hizi bajeti basi tuangalie hali halisi ya Wilaya kijiografia na mahitaji ya ile

Wilaya ya Makete ina milima, miinuko, udongo mweusi kwa hiyo unahitaji fedha nyingi kwa ajili ya kutengeneza barabara ambayo ni nzuri. Kwa hiyo, huwezi kulinganisha mgao ule na Wilaya nyingine ambazo pengine kilomita moja mahitaji yake hayawezi kulingana na kilomita ya Makete. Kwa hiyo, nawaomba kwamba mgao izingatie hali halisi ya barabara ilivyo ngumu kule Makete.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile kuongelea kuhusu suala la maji. Wilaya ya Makete ina vyanzo vya maji na vyanzo hivi vinapeleka maji Mtera na vingine vinakwenda ziwa Nyasa. Sasa ziko Kata zangu za Matamba, Ikuwo, Mlondwe ambao wao ni walini wazuri wa vyanzo vya maji lakini wao hawana miundombinu ya maji. Kwa hiyo, namuomba Waziri anayehusika atakapofika awe tayari basi kutusaidia wana Makete ili hawa waweze kupata motisha ya kulinda vile vyanzo vya maji vizuri basi na wao waweze kupata maji safi ya kutumia.

Lakini lingine katika sekta hii ya Nishati na Madini najaribu kuona ni namna gani tunaweza tukachangamki fursa ambayo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi ya kutumia kuhusu kuzalisha mazao mengi ya chakula. Nilikuwa nadhani kwamba bonde la Mbarali ambako inakwenda mito hii ya Makete ya Ruaha na hii kutoka Kimani, yale maji yangestahili sana yatumike kwenye umwagiliaji badala ya kupelekwa tu Mtera kwa ajili ya umeme na hasa ukizingatia kwamba Mtera umeme ule ni *megawatt 80* tu lakini tungetumia vyanzo vya pili wakati yale maji yanamwagiliwa tu kupata mpunga mwingi na baadaye kupata chakula kwa wingi lile bonde basi upande wa pili ambao maji ambayo yanakwenda ziwa Nyasa ambako sisi hatuyatumiii kwa sababu ardhi yetu ni nyevunyevu miezi yote 12.

Kwa hiyo, kule tungeweza kuzalisha umeme ambao uko kwenye Mto Lumakalya wenyе megawatt 220 ili tuzalishe na ukizingatia kwamba ule upotetu wa maji kwenye uzalishaji kwenye haya ma-*turbines* kimsingi ni kama kidogo sana, kwa hiyo, maji mengi yatakwenda kwa ndugu yangu Mheshimiwa Mwakyembe, kule watafanya shughuli ya umwagiliaji na kila kitu kinawezekana. Lakini utakuwa una-*maintain* yale maji ya Bonde la Mbarali na kule Chimala yanakuwa kwa kazi ya kilimo tu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuhusu uwanja wa Songwe ambao unajengwa. Ninataka kutoa mapendekezo haya kwamba ili uwanja huu uweze kuleta mafanikio na kuliingizia Taifa letu mapato, basi ni vizuri vile vivutio vya utalii ambavyo viko katika sehemu za Mbeya na Iringa vikaimarishwa kwa upande wa miundombinu.

Leo hii ule uwanja ukiwa unafanya kazi, hakuna miundombinu ya kuwafikisha watalii *Kitulo National Park* yenyе maua mazuri ya asili, mwezi wa Kumi na Mbili wakati mvua inanyesha kwa sababu barabara hazipitiki. Kwa hiyo, ninaomba Serikali ilione hilo ili ule uwanja usionekane *redundant*, lazima uandaliwe mazingira ya matumizi ambayo yatazalisha na yatatoa mchango mzuri, kwani Mtu akifika *Kitulo National Park* ataona maua, lakini vilevile atakuwa na nafasi ya kwenda Milima ya *Livingstone* na kuteremka kwenda *Matema Beach* kwenye Wilaya ya Kyela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkoo kwa hotuba yake na kwamba wananchi wa Makete wako tayari kufanya kazi na kama unavyojua wana Makete ni wachapakazi sana wanachohitaji muwatengenezee barabara ndiyo ombi letu kubwa na ubunge wangu wote uko kwenye barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofit*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Dr. Mahenge na wale wananchi wamekusikia kule. Sasa namwita Mheshimiwa Lediane M. Mng'ong'o na kwa kadri ya muda, nafikiri atakuwa ndiye msemajii wetu wa mwisho kwa kipindi hiki cha asubuhi.

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkoo.

Kwanza kabisa, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkoo, Waziri wa TAMISEMI - Mheshimiwa Celina Combani, wote tunamjua alivyo chapakazi na tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuamini na kutupa Wizara hii ambayo karibu kila shughuli zinazofanyika ziko hapo. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutuamini wanawake.

Nampongeza Waziri Philip Marmo kwa kazi nzuri na pia nampongeza Naibu Waziri Mheshimiwa Aggrey D. J. Mwanri na Katibu Mkoo Ofisi ya Waziri Mkoo, Katibu Mkoo TAMISEMI na wafanyakazi wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nianze kuzungumzia suala la barabara maana wote tunazungumzia miundombinu. Yale yote tunayoyazungumza, kama hakuna miundombinu mizuri, basi mengine yanashindwa kutekelezeka. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkoo sikuona mahali popote palipozungumzia barabara ya Iringa – Dodoma ambayo imekuwa ni wimbo wa kila siku. Nilitegemea kwamba ningeiona kwenye hii hotuba kwamba ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa ajili ya kuendeleza barabara hii muhimu ambayo ni kiungo kikubwa na italeta mabadiliko makubwa katika uchumi wetu. Labda nitaelezwa barabara hii imepangiwa utaratibu gani katika bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niungane na Mheshimiwa Estherina Kilasi kuzungumzia barabara ya Madibira mpaka Mafinga ambayo ni barabara iliahidiwa kwamba itatengenezwa kwa kiwango cha lami na wananchi wakiwemo wananchi wa Sadani Wilaya ya Mufindi waliobomolewa nyumba zao ili kupisha ujenzi wa barabara. Lakini sasa tunavyoangalia hii barabara haikuelezwa chochote kama kweli ujenzi utaanza kwa kiwango cha lami, hata kama ni kwa kiasi kidogo ili wananchi wawe na matumaini kuona kwamba pamoja na kwamba wananchi walibomolewa nyumba zao, lakini kuna

kazi inafanyika ili kuwaboreshea huduma ikiwa ni pamoja na kuweka miundombinu mizuri ya barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumzia hayo, naomba pia nizungumzie masuala ya utalii kwamba Mkoa wa Iringa una vivutio vingi sana vya utalii, lakini tatizo kubwa tulilonalo hatuna uwanja wa ndege, yaani hatupati ndege. Sasa sielewi.

Mkuu wa Mkoa amejitahidi kuyaomba Mashirika ya Ndege ili yaweze kutoa huduma za ndege Mkoa wa Iringa kwa sababu unapoongea na watalii wengine, wakiuliza: Je, ni muda gani kutoka Dar es Salaam mpaka Iringa? Unasema ni masaa saba kwa njia ya gari. Wanauliza; Je, hakuna huduma ya ndege? Tunaomba kiwanja cha ndege kiboreshw, lakini pia Serikali itusaidie kuweza kuhamasisha wamiliki wa Mashirika ya Ndege ili waweze kutupa huduma za ndege hata kama ni mara moja kwa wiki basi na sisi tupate huduma hiyo ingawaje wengine wanadai kwamba hakuna vituo vya kujaza mafuta ya ndege. Nina uhakika kama watakubali, wale wanaomiliki vituo vya mafuta Iringa watakuwa tayari kuweza kutoa huduma za mafuta ya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la maslahi ya Madiwani. Naomba niipongeze Serikali kwa kuwa sikivu. Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni sikivu, imesikia kilio cha muda mrefu cha Madiwani, kilio ambacho tumekuwa tunakitoa hapa na mwisho ilionekana kama Wabunge hatutetei maslahi ya Madiwani. Ninashukuru sana kwa hili lililofanyika na Mheshimiwa Waziri Mkuu nakupongeza sana. Ninaelewa kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa Waziri wa TAMISEMI, anaelewa kabisa matatizo makubwa ambayo Madiwani walikuwa nayo na tunampongeza kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikipongeza hilo, lakini nina hoja ya kujiuliza kuhusiana na Madiwani wa Viti Maalum. Hivi ni kwa nini kwenye vikao vya Baraza la Maendeleo la Kata, Diwani wa Kata anapokuwa hayupo, Diwani wa Viti Maalum haruhusiwi kuwa Mwenyekiti wa kikao hicho na tukijua kwamba Diwani wa Viti Maalum anawakilisha zaidi ya Watanzania 51% ambayo ni Wanawake? Anakaa pale halafu anateuliwa Mwenyekiti wa Kijiji kuwa Mwenyekiti wa Kikao. Hivi sio udhalilishwaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaelewa kabisa kwamba kwenye Kamati za UKIMWI Madiwani wa Viti na Wabunge wa Viti Maalum walikuwa hawamo, lakini ulipolezwa hili ukiwa Waziri wa TAMISEMI ulishughulikia na sasa hivi ni Wajumbe. Ninaomba ulishughulikie hili la Madiwani wa Viti Maalum kudhalilishwa kwenye Vikao. Amekaa pale halafu Mwenyekiti wa Kijiji anakuwa Mwenyekiti wa Kikao na yeze amekaa hapo! Kwa kweli linatutia aibu. Naomba hili lichukuliwe hatua haraka ili kusahihisha hili kwa sababu tunaonekana kama sisi siyo Viongozi. Kwa hiyo, ninaomba Madiwani wa Viti Maalum wawe Wenyeviti wa Kikao pale ambapo Diwani wa Kata anapokuwa hayupo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa hosteli katika shule za sekondari na hasa matatizo makubwa yanayowapata wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupyitia kwako naomba nilete kilio ambacho nimetumwa na Wanawake wa Kata ya Igombavanu Wilaya ya Mufindi. Wakina mama wametoa kilio chao na wakaniomba na wengine wamerudi kunipigia simu wakasema naomba umweleze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba watoto wetu wa Kata ya Igombavanu hawana mahali pa kukaa wasichana, wamepanga kwenye nyumba za watu na huu ni mfano tu mdogo. Wasichana wanakuwa hawana ulinzi, tunajua wote tuliosoma shule za wasichana mnapokuwa mnakaa hosteli au shule ya bweni, kunakuwa na *Matron* anayeangalia maisha ya hawa watoto. Wameachwa tu kwenye nyumba, wanapanga nyumba za wenyeji tu na matokeo yake wamekuwa wanajihusisha kwenye masuala ya ngono isiyokuwa salama na matokeo yake ni ongezeko la virusi vya UKIMWI.

Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu atakapokuwa kwenye bajeti yake ameweka hosteli, naomba aiangalie Kata ya Igombavanu ili hawa wakina mama ambao wametoa kilio chao waweze kusaidiwa watoto wao wawe na hosteli na nina uhakika pia shule nyingine zitaangaliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la UKIMWI. Ninaomba niipongeze Serikali kwa juhudini kubwa ambayo imefanywa ya kuweza kutoa elimu na huduma mbalimbali katika masuala ya UKIMWI. Ninapongeza kabisa juhudini ambazo zimefanywa na Mheshimiwa Rais ya kuweza kuzindua kampeni ambayo imehamasisha wananchi kupima. Jana nililzungumza hili kwenye swali langu nililokuwa nauliza na katika kipindi kifupi kuweza kupima wananchi zaidi ya milioni nne kujitokeza kupima ukilinganisha na wananchi milioni mbili walijitokeza toka tatizo la UKIMWI lijitekeze hapa nchini miaka 25 iliyopita.

Hii ni juhudini kubwa na ndiyo maana nimeomba kwamba ili kuienzi siku hii, Serikali iitangaze hii siku kama siku ya UKIMWI ya Tanzania na hii ipo pia kwenye nchi nyingine na ile siku ya UKIMWI duniani, inakuwa ya dunia nzima ya kupima yale ambayo yamefanywa kwa mwaka mzima katika harakati za mapambano dhidi ya UKIMWI.

Napongeza kabisa utendaji mkubwa wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI kwa kazi nzuri waliyoifanya ikiongozwa na Mama mahiri, Mama Dr. Fatma Mrisho kwa kazi nzuri ambayo imefanyika na Viongozi wengine waliokuwepo akiwemo Meja Jenerali Mstaari Herman Lupogo ambao wameweza kufanya kazi nzuri na wakishirikiana na Makamishna ambao na mimi nilikuwa mmoja katika timu hiyo.

Tunapongeza kazi nzuri ambayo imefanyika na ninashukuru Serikali kutoa magari ya sinema. Tunajua kwamba zamani yalikuwepo hata ukulima wa kisasa uliendelea kwa sababu kulikuwa na elimu inayotolewa vijijini. Nina uhakika magari haya ambayo Serikali imetoa yataendelea kutoa elimu ya UKIMWI pamoja na elimu nyingine za maendeleo na kuweza kuhakikisha kwamba elimu inafika vijijini kwa sababu kulikuwa na tatizo la kutofika elimu vijijini kwa vile vitendea kazi vilikuwa havipo. Ninaipongeza sana Serikali kwa hili.

Kuhusu mfuko wa mapambano dhidi ya UKIMWI, ninapongeza Serikali kwa kuliona. Nimekuwa nalipigia kelele sana suala hili kwa sababu bila kuwa na mfuko wa mapambano dhidi ya UKIMWI hatuwezi kufika mbali kwa sababu pia tunategemea hela za wafadhili. Pale wafadhili watakapojoitoa, nchi itayumba na watu wanaotumia dawa za kupunguza makali ya Virusi vya UKIMWI wanaweza kukosa huduma. Mfano mzuri kabisa ni nchi ya Zimbabwe ina mfuko wa namna hii. Pamoja na matatizo ambayo Zimbabwe inayo, lakini wananchi wake wameendelea kupata dawa na kupata huduma za UKIMWI kwa vile wana mfuko amba ni endelevu. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu alete haraka huo Muswada wa Sheria ya kuanzisha mfuko huo ili uweze kuanzishwa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la watoto yatima na waliopo katika mazingira magumu. Naipongeza Serikali kwamba miaka yote imikuwa inatenga fedha kwa ajili ya kutoa elimu kwa watoto yatima na waliopo katika mazingira magumu ili waweze kupata elimu kama watoto wengine. Hili pia limesaidiwa na wadau mbalimbali. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba utusaidie, hivi hawa watoto wanapofika Chuo Kikuu, kwa nini wasifutiwe ile 40% wanayotozwa? Hivi wataitoa wapi hiyo 40% kama walishindwa kulipa ada ya sekondari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wale watoto amba wako kwenye mazingira magumu, kwa sababu upo utaratibu wa Serikali, wanawatambua, Mheshimiwa Waziri Mkuu awafutie ada ya Vyuo Vikuu na hata Sekondari kwa sababu siyo wote wana uwezo. Ninaomba Serikali ifanye kama ilivyofanya katika utaratibu wa MMEM kwa ajili ya kupeleka kwenye shule ziada ile ambayo wamefutiwa kuwafidia zile shule, ninaomba pia Serikali iweze kufidia Vyuo Vikuu kama ni zile gharama za 40% Serikali iwalipie hawa watoto ili nao wasome kama watoto wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto hawa wanahangaika sana, wamelipiwa huku, wamelipiwa na wafadhili mbalimbali, inapofika Vyuo Vikuu inakuwa ni ngumu. Ninaomba hili litazamwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bima ya Afya, ninaomba hawa watoto wapewe Bima ya Afya ili wapate huduma kama watoto wengine kwa sababu hakuna watu wanaoweza kuwahudumia kiafya. Wakiwa Sekondari, wanapougua, mfano mzuri kabisa watoto hawa wanaambiwa warudi nyumbani wakatibiwe ili waje waendelee na masomo. Hivi wanaendelea kutibiwa na nani na wengine ni wakuu wa kaya, wameacha wadogo zao kwa watu? Ninaomba hili pia liangaliwe shulen. Watoto wote waliopo mashulen kama ni sekondari na wale amba wako kwenye jamii wawekewe Bima ya Afya ili waweze kupata huduma kama watoto wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuja katika suala la habari vijijini. Habari ni muhimu sana kufika vijijini na ninakumbuka kwamba *UNICEF* ilianzisha utaratibu wa waandishi wa habari wa vijiji. Ninaomba Serikali iangalie uwezekano kukiendeleza hiki ili suala hili la kuwa na Waandishi wa Habari wa Vijiji ili hata Vijiji viweze kupata habari kama watu wengine kwa sababu wakati mwingle habari hazifiki Vijijini.

Kama tutaanzisha utaratibu huu, Waandishi wa Habari wa Vijiji tutaweza kuwatumia hata vijana wetu waliomaliza shule za sekondari wako huko vijijini hawana shughuli ya kufanya wanaweza kuwa wanatoa habari ambazo mwishoni tunaweza kuwa na Vituo vya Habari au vituo vya maendeleo vya Kata ambako zile habari zitakuwa zinatolewa zinafikishwa vijijini. Hili suala pia naomba liangaliwe na hizi *press club* pia ziimarishwe ili ziweze kutoa habari sahihi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la utamaduni, ninaipongeza Serikali kwa kuwa na Makumbusho ambayo yanatoa vielelezo vya utamaduni wetu. Mimi naomba haya makumbusho yaende kwenye ngazi za Mikoa na ngazi za Wilaya kwa sababu sidhani kama kila mwananchi anaweza kwenda kwenye makumbusho ya Taifa, kule kujuu historia ya kabilo yake au mambo yoyote yaliyopo kwenye eneo lile.

Ninaomba tuanzishe utaratibu wa kuwa na makumbusho kwenye ngazi ya Mkoaa ambapo wataelezwa historia yote ya Mkoaa husika kama ni historia ya Wangoni, basi watoto wote waelimishwe au Wahehe au Wajita wale wote wajue historia zao kwa sababu huko tunakokwenda historia hizi zitakuja kupotea. Tunaomba ziwekwe kumbukumbu na historia hata na nyumba zile ambazo zilikuwepo zamani ili watoto wetu wajue historia hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie wafanyabiashara ndogondogo kama Dar es Salaam wanawaita Wamachinga. Utaratibu mzuri umewekwa na Serikali, napongeza na iko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi, lakini ninaomba hata kwenye Mikoa tuanze kuangalia kuwatengea maeneo ya kufanya biashara badala ya kuwa kila sehemu, tuanze utaratibu huo kwa sababu ndiyo njia mojawapo ya kuboresha Miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumzie suala la mikopo kwa wanawake. Ninaomba wanawake pia wapewe mikopo na wale ambaa wameanzisha SACCOS zao SACCOS za wanawake zifikiwe kupewa mikopo na zile fedha ambazo zimetengwa zilizokuwa zinatengwa kwenye maendeleo ya jamii zihamishiwe kwenye SACCOS za wanawake ili ziweze kuwafaidisha wanawake wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kufanya hivyo hatutaweza kuondokana na umaskini kwa sababu wanawake hawawezi kushindana katika upataji wa mikopo na makundi mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya kusema hayo, ninaomba nizungumzie masuala ya mazingira. Nina uhakika kwamba Waziri anayehusika atalielezea vizuri na Mheshimiwa Waziri Mkuu amelielezea kwa ufupi. Lakini kila mwaka mimi nimeona usafi wa mazingira hautengewi fedha za kutosha. Tuna miundombinu ambayo hairidhishi vijijini, vijiji vingi au wananchi wengi hawana vyoo wala usafi wa mazingira hautiliwi maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. (*Makofî*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri muda wa shughuli za kipindi hiki cha toka asubuhi umekamilika na wale ambao walipaswa kuzungumza kwa kipindi hiki cha asubuhi basi orodha yao imefikia hapo.

Sasa kabla sijasitisha shughuli za Bunge kwa kipindi hiki cha asubuhi ninaomba tu niwatamke wasemaji wa mwanzo ambao watachangia kwa kipindi cha jioni.

Tutaanza na Mheshimiwa Mariam Reuben Kasembe halafu Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbii atakuwa msemaji wetu wa pili na msemaji wetu wa tatu atakuwa Mheshimiwa James Daud Lembeli. Kwa hiyo, wengine nitawataja kwa kadri tutakavyokuwa tunaendelea na kikao chetu cha jioni.

Baada ya kutoa matangazo haya mafupi, labda niendelee tu kusisitiza ile Kamati ya Burudani na Starehe ya Bunge kama ilivyotangazwa, Kikao kitafanyika jioni baada ya kuahirisha Bunge. Siyo mchana huu, ni baada ya kusitisha shughuli za Bunge.

Baada ya matangazo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.57 mchana Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na shughuli za leo jioni. Sasa nitamwita Katibu ili atuongoze na ratiba yetu ya jioni.

Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea kuhusu hotuba ya bajeti Ofisi ya Waziri Mkuu na msemaji wetu wa kwanza jioni hii atakuwa Mheshimiwa Mariam Kasembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Maghimbii. Mheshimiwa Mariam, karibu.

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu, hotuba ambayo kwa kweli nimeisoma vizuri, nimeipitia kipengele hadi kipengele na nimeweza kupata nguvu za kuamua kuchangia hotuba hii. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wa Nchi na Manaibu katika Ofisi hii na Makatibu kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kutuandalia hotuba hii ambayo inatupa mwelekeo na matumaini kwa wenzetu ambao tumewaacha vijijini. Nasema ahsanteni sana na mwendelee vizuri na kazi hii. *(Makofii)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naanza kwa kuchangia kwa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka Mikoa inayolima korosho kwa ushirikiano walioonyesha hapa Bungeni kushughulikia suala la kutatua tatizo la ununuzi wa korosho katika Mikoa yetu. Lakini sipendi kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge

peke yao, nitoe shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepita kwa sababu kila wakati tulikuwa tunawasumbua kuwaomba kukaa nao kwenye vikao kutafuta ni jinsi gani wanaweza kutusaidia kutatua tatizo hili. (*Makofi*)

Sio hivyo peke yake, jitihada zilivyokuwa zinaendelea za Waheshimiwa Wabunge pamoja na Waziri wa Kilimo kwenye Mkoa wetu, Mkuu wa Mkoa wetu pamoja na viongozi wa Chama (Mkoa), Waheshimiwa Madiwani walikuwa kidete pamoja na viongozi wa Vyama vya Msingi kupata taarifa kutoka kwetu na wao kuzifanya kazi na hatimaye tumeweza kufanikisha msimu huu.

Lakini Waheshimiwa Wabunge ambao tunatoka mikoa inayolima korosho niseme kwamba hii ni hatua moja ya kwanza, bado tuna jukumu kubwa sana la kuhakikisha kwamba sasa suala la pembejeo kuwafikia wakulima kwa wakati ni wajibu wetu kuishauri Serikali ili iweze kutusaidia wakulima hawa waweze kupata pembejeo mapema na kupuliza korosho zao mapema ili waweze kupata mazao yaliyo bora na hatimaye kuweza kupata tija na hatimaye kuondokana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamekuwa wakisimama hapa kuomba suala la pembejeo. Sisi kwenye Mkoa wetu wa Mtwara tumepata pembejeo kidogo, hazitoshelezi. Naiomba sana Serikali, yale makampuni ambayo yameteuliwa kutupelekea pembejeo hizi katika Mkoa huu nawaomba wahimizwe kutuletea pembejeo hizi kwa wakati na pembejeo ambazo wananchi wanazikubali na wamezizoea ili tuisiwichanganyi wakachanganyikiwa wakaacha kupuliza korosho zao tukarudi tena tulikotoka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la kilimo, nimesoma hii hotuba na taarifa ya Waziri wa Fedha niliisikiliza vizuri, tunaambiwa kwamba asilimia 80 ya Watanzania ni wakulima. Mimi binafsi inawezekana sielewi, lakini takwimu hii inanichanganya. Inanichanganya kivipi? Tukirudi kwenye vijiji vyetu, tukiangalia kwenye Wilaya zetu na Mikoa yetu tuijilize: Je, hivi kweli wale tunaowahesabu kwamba ni wakulima kweli wote ni wakulima au asilimia hii themanini tunayoihesabu hapa tunawahesabu na wale vijana ambao wanashinda kutwa nzima vijiweni? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali tuangalie upya, hawa wakulima tunaowahesabu kuwa ni wakulima ni wakulima wapi? Ninavyofahamu ni kwamba, ukifika kwa mfano kijijini, watu ambao unaweza kuamini kabisa kwamba ni wakulima, ni wale ambao wana mashamba, wanalima, wanavuna na wakapata chakula cha kujitosheleza wao na familia zao. Lakini wapo wanaojihesabu kwamba ni wakulima, lakini tukiangalia sio wakulima sahihi. Sasa namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu asimamie ile Sheria ya Nguvukazi itumike nchi nzima. Hawa vijana wetu wanaokaa vijiweni kuanzia asubuhi sheria iwabane warudi vijijini, maeneo ya kulima yapo, wakalime ili kuongeza pato katika nchi yetu na wao wenywewe kuondokana na umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka huko miaka ya nyuma Serikali yetu ya Awamu ya Kwanza, Sheria hii ya Nguvukazi ilitekelezwa hasa kwa Mji wa Dar es Salaam. Wakati ule aliyekuwa Waziri Mkuu alitoa tamko la hiari, watu wote ambao

hawana kazi maalum walipewa *warrant*. Kipindi kile zilikuwa zinatumika *warrant* kurudi vijijini. Wengi waliamaa kurudi vijijini. Lakini Serikali vilevile ikaamua kutenga maeneo kwa mfano Kibugumo, Gezaulole, wale ambaa walikuwa tayari kwenda kule walikwenda na hivi sasa ukienda katika vijiji hivyo ni wakulima wazuri, wameshanufaika na kutajirika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ifuate mfano huo kufanya kazi hawa wenzetu ambaa wamejazana Mijini na hawana kazi za kufanya wakati mapori yamejaa tele na kama katika maeneo wanayotoka hakuna maeneo ya kilimo, kuna Mikoa ambayo bado ina maeneo ambayo wanaweza kupatiwa ili kuendeleza shughuli za kilimo kuliko kuwapa hawa wenzetu wanaokuja kutoka nje kuchukua maeneo yetu, tuwape hawa vijana wanaozurura mijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo nataka kuchangia ni kuhusu suala la maji. Suala la maji kwa Mkoa wetu wa Mtwara bado mpaka hivi sasa hatujajitosheleza bado kupata maji safi na salama. Ziko Wilaya ambazo maji kidogo wanapata, lakini zipo Wilaya mpaka sasa hivi maji ni kitendawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano Wilaya ya Newala, hii ni Wilaya pana. Tunategemea kabisa maji yanatoka chini bondeni, maji ambayo yanatakiwa watumie kupampu yaje kwenye matanki na ni mpaka wapampu kwa masaa kumi ili matanki yaweze kuja ili wananchi waweze kupata. Lakini kwa kipindi hiki, hakuna maji kabisa kwa sababu ya tatizo la umeme. Kwa sababu Wilaya ya Newala sasa hivi wanapata umeme masaa mawili au manne ambayo hayatoshelezi kwa kupampu maji yakawafikia wananchi, kwa hiyo, akinamama na akinababa wanahangaika usiku kucha kutafuta maji. Naiomba Serikali ichukue hatua za haraka za kukarabati jenereta lililoko Masasi au tupelekewe jenereta la muda ili liweze angalau kusaidia kwa shughuli hizi za maji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wilaya ya Masasi, nafikiri Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mmesikia kila wakati tukisemea suala hili la maji. Nako kuna tatizo kubwa la maji, lakini kila mwaka tunapokuja kwenye bajeti tulikuwa tunaelekezwa kwamba tutapata maji kutoka Ngwinji. Lakini suala la maji kutoka Ngwinji sasa hivi limeshakuwa kitendawili na hatuelewii haya maji tutayapata lini. Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atakapokuwa anatoa majibu yake tupate jibu sahihi, maji ya Ngwinji yatakuja lini Masasi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji Masasi lisingefikia hatua mbaya, lakini pale kulikuwa na bwawa la Mcchema ambalo lilichimbwa toka ukoloni ndilo lililokuwa linatusaidia kupata maji pale. Bwawa hili lilipopasuka, Serikali haikuchukua hatua zozote za kutusaidia kukarabati bwawa lile. Kwa hiyo, limeendelea kukaa, halitunzi maji tena, tunahangaika usiku na mchana. Naomba sana suala la maji kwa Wilaya ya Masasi liangaliwe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuzungumzia suala la maji Wilaya ya Nanyumbu. Kwa wanaofahamu Nanyumbu, jiografia yake ni kukavu mno, ni vilima

vilima, hakuna mito ya kudumu inayotunza maji kwamba hata wananchi watakwenda kuokota maji kwenye mito hiyo, hakuna. Kuna mito mingi, lakini ni mito ya kifuku tu, mvua zikiisha na mito inakauka. Kwa hiyo, wananchi hao wanahangaika. Kuna baadhi ya vijiji suala la maji wao kwao ni hadithi. Naiomba sana Serikali itusaidie ili wenzetu nao waondokane na tatizo hili na ukizingatia kwamba hii ni Wilaya mpya. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nimepigwa simu na mpiga kura mmoja akiniomba nimsaidie kumtumia nauli haraka mke wake alikuwa Mto Ruvuma huko, watu wanalima mpunga huko, alivyokuwa anakwenda kuchota maji ili arudi nayo nyumbani kashikwa na mamba, mwanamke amekufa, walikuwa wanazika leo. Hiyo ndiyo hali halisi ya kule kwetu kwa sababu watu wanaokaa kandokando ya Mto Ruvuma wanategemea waende kwenye Mto huo ili kwenda kuchota maji na Mto wenywewe ndiyo huo uliojaa mamba. Jamani hili suala la maji litakwisha lini katika Mkoa wa Mtwara? Tunaomba mtuangalie sana. Suala la maji ni tatizo kubwa. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nimekuwa nikisikia hapa Bungeni kwenye maswali na majibu wanayotoa Waheshimiwa Mawaziri kutokana na hali ya upungufu wa watumishi hasa kwenye Mikoa iliyopo pembezoni ukiwemo Mkoa wa Mtwara. Majibu tuliyokuwa tukiyapata ni kwamba tuboreshe mazingira yetu ili kuweka vivutio watumishi hao waweze kukaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Serikali isijivue, vivutio ni pamoja na kutuwekea umeme vijijini, barabara nzuri na maji. Vikiwepo hivyo vyote wao watavutika kuja kukaa kwenye maeneo yetu. Haiwezekani mtumishi aje kijijini ambako itamlazimu kuamka saa nane za usiku kwenda kutafuta maji na asubuhi inabidi aende darasani. Haitawezekana hata kidogo! Tunaomba maji. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo nataka kuzungumzia ni kwamba, kwenye Wilaya ya Masasi tulikuwa na Chuo cha Wasioona. Inasikitisha Chuo kile sasa hivi hakina mwanafunzi hata mmoja, lakini majengo yapo ya kutosha kama vile madarasa, mabweni, yaani kila kitu kama shule za zamani zinavyokuwa. Majengo yale yametelekezwa, lakini Halmashauri ya Wilaya ya Masasi tulionba kwamba majengo yale kwa sababu sasa hivi hayatumiki na wale waliokusudiwa sasa hivi hawapo, basi tukabidhiwe sisi kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ili tuunganishe na Sekondari yetu ambayo ipo hapo hapo pamoja tuyatumie yale majengo kwa ajili ya sekondari. Tatizo liko wapi? Serikali kwa Serikali inagomba wapi? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hayo majengo tupewe ili tufungue Kidato cha Tano kwa sababu tuna shule ya sekondari mpaka Kidato cha Nne. Majengo yapo tayari pale, mabweni yaliyopo pale yanetusaidia kwa watoto wa kike, wakalala pale wakapumzika, lile suala la kutoka majumbani kwao lina matatizo. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI -Mheshimiwa Celina Kombani nafikiri anapata picha nzuri kwa sababu ye ye aliwahi kuja Masasi na aliyona majengo haya na alisikitika. Namwomba sana Mheshimiwa ampe ufanuzi wa kutosha Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu hali halisi ya pale ili tupewe majengo haya ili yaweze kuwa sekondari. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalotaka kulizungumzia ni suala la mauaji ya Maalbino. Mimi ni Mjumbe mmojawapo kwenye Chama chetu cha Skauti cha Bunge. Nilibahatika kwenda Mwanza wakati ule mauaji ya Maalbino yaliposhamiri. Katika maeneo tuliyotembelea tulibahatika kwenda shule moja inaitwa Mitindo. Tulikuta watoto wengi pale *Albino*. Naomba nichukue nafasi hii kuupongeza uongozi wa Mkoo wa Mwanza kwa jitihada walizozichukua baada ya matukio yale kushamiri, wamefanya jitihada ya kukusanya watoto wote wenye umri wa kwenda shule, lakini wamewapeleka kwenye ile shule ambayo ilikuwa ni shule maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, kwa sababu ile imetokea dharura ile shule wameongezewa mzigo, kwenye bajeti iwaongezee kwa sababu wale watoto Maalbino wanahitaji tiba nzuri, lishe nzuri na kulala mahali pazuri. Kama tunavyowafahamu, walivyo kwa kweli wanahitaji malezi mazuri mno. Naomba kama kutakuwa na uwezekano, Mheshimiwa Waziri Mkoo kama atakwenda Mwanza afike kwenye hiyo shule aone hali halisi ya hawa watoto jinsi inavyotia huruma. Wenzetu wa Mwanza walifanya jitihada ile. Nimewapongeza mno. Sasa tusiwakatishe tamaa, tuwaunge mkono kwa kuwapelekea bajeti ya kutosha ili waweze kukidhi mahitaji yao katika shule ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ni kuhusu Madiwani. Naomba niunge mkono kwa hoja aliyoitoa Mheshimiwa Waziri Mkoo kuwakubalia Waheshimiwa Madiwani kuongezewa posho na matibabu pamoja na vyombo vyaya usafiri. Kwa kweli nimefurahi na nafikiri hata Waheshimiwa Madiwani nchi nzima watakuwa wamefurahi. Lakini naomba atakapokuwa anatoa majibu Mheshimiwa Waziri Mkoo atoe ufanuzi, utaratibu huu unaanza lini kwa sababu nimeanza kupigiwa simu nikiulizwa utaratibu huo unaanza lini au tuanze leo?

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Wairi Mkoo atoe ufanuzi ili Waheshimiwa Madiwani wenye we waelewe unaanza lini ili Halmashauri zitakazokuwa tayari waweze kuwapa usafiri ili waweze kutusaidia kufanya shughuli zetu za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho, ni suala la kuhamia Makao Makuu Dodoma. Hili ni suala la nchi nzima, hata yule aliye kwa kijiji asiyekwenda shule anafahamu kwamba Makao Makuu ya nchi yetu ni Dodoma. Sasa naiomba Serikali chini ya Waziri Mkoo, Mheshimiwa Waziri Mkoo afanye jitihada atakazoweza, basi tuanze angalau kuonyesha kwamba Wizara hizi na hizi, hata tutakapokuwa tunamaliza kipindi chetu angalau Wizara hata sita ziwe zimeshamaria hapa Dodoma. Mnasita nini? Naamini kabisa kama Serikali ikihamia hapa Dodoma msongamano wa Dar es Salaam ungepungua kwa sababu pale watu wanafuata huduma kwa sababu Wizara zote ziko pale. Kama Serikali yote ingehamia hapa, wafanyabiashara wangeweza kuondoka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA - MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kasembe na hasa hizi dakika za mwisho umeshika kasi kweli. Nadhani kasi hiyo hiyo itatuleta Dodoma. Sasa namwita Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi na atafuatiwa na Mheshimiwa James Daudi Lembeli.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ili niweze kutoa mawazo yangu na mapendekezo yangu kidogo katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara nyingi ukiwa mtu wa mwisho unakuwa umeshafilisika hoja zako zote, lakini hata hivyo bado nina machache ya kuongeza katika hoja hii ya Waziri Mkuu. Kwanza, nitaanza katika elimu. Napenda kuwasifu sana Watanzania, Watanzania tumeumbwa kama askari, basi sijui huko nyuma ndivyo tulivyofundishwa na wazee wetu wakakua hivyo ndiyo maana mpaka leo tuko hivyo. Kwa sababu askari nasikia katika mafunzo yao akiambiwa kaa chini, atakaa, haulizi. Nenda mbele, atakwenda, haulizi, nenda kaue atakwenda haulizi, unaambiwa ufanye kwanza ndipo uje uulize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, laiti ingekuwa Watanzania wanauliza katika ujenzi wa shule hizi katika kila Kata basi labda shule hizi zingejengwa chache lakini zikatimia haja, kukawa na walimu wa kutosha, kukawa na vifaa vya shule vya kutosha kuliko kujenga shule nyingi kama ilivyo sasa hivi karibu katika kila Kata lakini hakuna walimu, vifaa wala chochote. Huu ni uaskari, wanaambiwa nenda, wanakwenda. Lakini baadaye wanakuja wanafikiri eeh, shule moja ina wanafunzi 400, ina mwalimu mmoja. Sasa kweli tutaweza kuwasaidia watoto wetu katika hali kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizo hizo hasa za sekondari mara nyingi zinakuwa na mabweni. Kuna mabweni wanakaa, kwa hiyo, kunahitajika kipatikane chakula kwa ajili ya wanafunzi. Anakuja mzabuni analeta chakula katika shule, anakaa hata miezi sita halipwi pesa zake; mzabuni huyu anayeleta vifaa katika shule ni mfanyabiashara, lakini anapofika kudai fedha zake anaambiwa mpaka deni hili liende kwa Mkaguzi Mkuu, aende kukagua kwanza kama ni deni la kweli au sio la kweli. Sasa sio la kweli vipi, wakati wanafunzi wameshakula na kunywa mwezi mzima, kisha unasema deni hili hatuwezi kabisa kulilipa mpaka lichekiwe! Huyu mfanyabiashara umemweka wapi? Biashara zake zilale, asilete chakula! Katika shule hizi nyingi zilizojengwa ningependekeza kwa Serikali kabla hawajafanya kitu chochote kwanza wafanye utafiti: Je, tunavyo vifaa vya kutosha kwa ajili ya shule hizi 1,000 tunazojenga? Watoto tunao, *Alhamdulillah*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja tulikwenda kijijini tukawaeleza jamaa habari ya nyota ya kijani, wakasema wao hawana habari ya nyota ya kijani. Wao wanajua nyota ni rangi nyeupe ndiyo inayong'aa juu. Ukimweleza kijana, hana habari nayo. Kwa hiyo, tunaza *Alhamdulillah* watoto tunao na mabanda tunayo, lakini je, vifaa tunavyo? Watoto hawa watasoma vipi? Shule moja ina wanafunzi 400, ina mwalimu mmoja, kweli mtoto huyu ataendelea mpaka amalize?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika hii Wizara ya Elimu, siku moja nilikuwa natazama TV, nikamwona Mheshimiwa Shemeji yangu Profesa Maghembe anazungumzia habari ya lugha. Alikuwa akiweka msisitizo kwamba lugha ya Kiingereza haitafundishwa kuanzia Darasa la Kwanza, nikafikiri sikusikia, nikasogea karibu na bahati nzuri alikuwa hazungumzi Kipare, maana sikijui, alikuwa anazungumza Kiswahili hasa. Nikasogea karibu nikamsikiliza nikaona kweli anasema kuwa Kiingereza hakitafundishwa toka Darasa la Kwanza.

Nikauliza wenzangu ni vipi? Nikasikia eti Walimu na watafiti katika *Institute* za Kiswahili wanasema Kiswahili kimedharauliwa, kwa hiyo, Kiingereza kisifundishwe kutoka Darasa la Kwanza kikafundishwe sikumbuki alisema Darasa la Tatu au la Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiswahili ni lugha yetu, hata kama hukumfundisha atajua Kiswahili na hata ukifanya vipi ndani mzungumzishe lugha yoyote, lakini akitoka nje atazungumza Kiswahili kwa sababu lugha yetu ya Taifa ni Kiswahili. Lakini Kiingereza ni lugha ya kigeni ambayo mtoto anatakiwa aisome mapema ili aweze kuiweka kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nikafikiri labda Mheshimiwa Waziri wa Elimu anafikiri mtoto hawesi ku-*master* lugha mbili au tatu. Sasa nataka kumhakikishia kwamba mtoto mdogo anayeinuka sasa unaweza kumsemesha lugha tatu anasikiliza, atachelewa kidogo kuzungumza kwa mujibu wa watafiti, mimi sijafanya utafiti huo.

Lakini kwa mujibu wa watafiti wanasema atachelewa kidogo kama mtoto kawaida anazungumza kwa miezi tisa au mwaka, basi atachukua muda kidogo. Lakini akifika wakati wa kuweza kuzungumza, atazizungumza lugha zote tatu kwa umakini sana na hatakosea hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sikuona sababu gani Profesa anasema kama Kiingereza kisifundishwe. Nahisi hii ni kuwadumaza watoto wetu. Sisi tuna mipango ya kuingia kwenye *East African Community*, hivi kweli mtu aliyekuwa hajui Kiingereza ukifika Muungano huu kutakuwa na kazi zitakazokuwa *created* kwa hii *community* na hawatawapa *portion* kuwa hii ya Watanzania, hii ya Wakenya na hii ya Waganda? Labda zile *post* kubwa, lakini hizi nyingine za katikati, wataingia kwenye *competition*, watakwenda kwenye *interview* na kila kitu na atakayekwenda kwenye *interview* hizi pengine siyo Mtanzania, wataita ma-expert waje wawa-interview watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli mtu anayekwenda shule anajifunza kuanzia *Form One* Kiingereza, huyu ateweza ku-*compete* na Mkenya anayeanza kusoma toka *nursery school*? Ateweza ku-*compete* na Mganda? Hizi *posts* zote si zitachukuliwa na wenzetu wa Kenya na Uganda! Kkwa kweli hapo nimeogopa kidogo kwa msimamo wa Wizara ya Elimu na kama sikuelewa, naomba nieleweshwe na nikieleweshwa napendekeza kwa Serikali ianze kutoa agizo kuwa toka *nursery school* watoto waanze kusomeshwa Kiingereza, Kiswahili kibaki kuwa ni lugha yetu ya Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa napenda kuzungumzia habari ya afya. Kwanza, napenda kuwapongeza Madaktari wa Tanzania, walivyokuwa mahodari na walivyokuwa wavumilivu hawa waliobakia, wengi wameondoka hawapo tena Tanzania, lakini hawa waliokuwepo kwa kweli ni Wazalendo. Lakini wengi Uzalendo umewashinda, kwa sababu gani? Kwa sababu kazi ni nyingi, vifaa hakuna na mshahara ni mdogo. Kwa hiyo, sioni sababu kwa nini Serikali isijaribu kuwakumbatia hawa tulionao, tukawabembeleza na kuwabembeleza kwenyewe ni kuwapa mishahara ya kutosha, vifaa vya kufanyia kazi ili nao waweze kujisikia kama wapo kazini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kwa mujibu wa Ripoti ya WHO, nchi zinazoendelea *ratio* ni *ten doctors* kwa wagonjwa 1000. Lakini hapa kwetu tuna *2.3 doctors* kwa wagonjwa 100,000. Kweli huyu ni *doctor au ni nini?* (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikufichi, mtoto wangu wa kwanza ni Daktari na mtoto wa mwisho ni Mwanasheria. Basi yule Daktari hukaa na kuniambia mama mimi najuta kusoma udaktari. Huyu mdogo wa tatu ana pesa zaidi, tena ana *time* ya *ku-relax weekend*, mimi *weekend* kama nalala, nakuja kuamshwa kuna *emergency*, lazima nikimbilie hospitali. Leo mshahara mdogo namna hii! Vipi mnategemea Madaktari wasiondoke?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwalaumu sana kuondoka na napendekeza Serikali iwabembeleze kwa sababu kusomesha Daktari ni ghali sana ili pesa zetu zisipotee bure, Madaktari wetu wajaribu kuelezwu huko waliko, wajue uzalendo umekaaje, lakini na nyie pia mlion Serikalini mjue naye huyu ni binadamu anataka *ku-make his hands meet*. Sasa hawezi *ku-make his hands meet*, anaona bora akimbie, wala tusimlaumu kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili katika Wizara ya Afya, hasa nataka kuzungumzia hiki Chuo Kikuu cha Muhimbili. Nilikuwa naomba sana mafunzo ya Udaktari, kidogo wabadilike, waende kwa mujibu wa ulimwengu unavyokwenda. Waondokane na zile enzi za zamani za akina Profesa Mwankemwa na Profesa Mwanukuzi. Enzi hiyo Daktari alikuwa akijiona kama mfalme, Daktari hazungumzi na mgonjwa wake, Daktari anakwenda ameshavaa suti yake ya kwenda kupasua mtu, hazungumzi na mtu na hicho chumba cha *operation* mimi sijawahi kuingia, lakini nasikia Daktari hata yule *nurse* hazungumzi naye, anataka mkasi ulio na saizi gani anafanya mkono hivi tu, *nurse* kazi yake ni kuleta, yeye aendelee kuchana. Akitaka sijui kisu cha aina gain, anapeleka mkono tu, apewe ili aje achane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nazungumzia hasa kwa sababu ya hii *accident* iliyotokea hivi karibuni ya daktari wa Muhimbili kwa mgonjwa wa kichwa akapasuliwa mguu na mgonjwa wa mguu akapasuliwa kichwa. Mimi wale siwalaumu kwa sababu wale siyo kosa lao ni kosa la *system*.

Mimi nimepata bahati ya kwenda kutibiwa India mwaka 1998, nilikuwa na matatizo ya moyo nikaenda India. Daktari wangu ile dakika ya mwisho alikuwa anazungumza na mimi. Nakwenda *theatre* amekwishafika *theatre* na yeche kazungumza na mimi mpaka nafanyiwa sijui inaitwa nini, lakini mimi katika mambo ya udaktari nitaita hiyo *operation* niliyofanyiwa alikuwa anazungumza na mimi ananiambia, unaona

hiki kinakwenda sasa kwenye moyo wako, hiki kitafanya hivi. Vipi? Unaogopa? Au nini! Alikuwa ananisemesha. Kwa hiyo, daktari kama huyo hawezi kufanya kosa.

Nimekwenda juzi juzi tena kutibiwa jicho hili, nilipokwenda kutibiwa jicho nakwenda zangu *theatre* sasa nilishafanyiwa *cancelling* huko kwenye wodi tayari, nakwenda *theatre* namkuta Daktari yupo. Kabla hatujaingia ndani ya *theatre* akaniuliza, unajua kama unakuja kufanyiwa *transplant* ya konea nikamwambia ndiyo najua. Akaniuliza unajua maana ya *transplant*? Nikamwambia ndiyo najua, akaniambia mimi nimweleze, nikamwambia ku- *transplant* maana yake ni kuondoa kitu kingine au kama hakipo ukapandikiza kitu kingine. Akaniambia sawa. Sasa hivi unajua wewe kama unataka kufanyiwa *transplant* ya jicho la mtu aliyekwishakufa? Nikamwambia najua. Akaniuliza, *are you ready?* Nikamwambia *I am ready*. Tumekwenda zetu *theatre*. Kwa hiyo, yeye anajua naumwa na nini. Sasa unamtoa mgonjwa huko kwenye wodi, daktari hajasomewa kawekewa faili tu hapa halafu tunakuja kumlaumu kuwa kwa nini kafanya *operation* ya kichwa wakati huyo anaumwa mguu au kwa nini umempasua mguu wakati huyu anaumwa na kichwa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningelikuwa laiti mkubwa kama nyie hapo mbele, basi ningeishtaki *system* ya Muhimbili wala nisingewashitaki wale Madaktari wala nisingewalaumu. Wale hawana kosa, kosa ni la *system* la kufuata toka enzi ya akina Profesa Mwankemwa na Profesa Mwanukuzi. Enzi hiyo Waziri wa Afya hata hajazaliwa *system* inaendelea ile ile. Wazungu wenyewe waliowafundisha walishabadilika katika *system* hii, wanazungumza na wagonjwa wao. Kwa hiyo, hawawezi tena kufanya kosa kama hili la kupasua kichwa wakati mtu anaumwa mguu.

La mwisho katika afya, nilikuwa nauliza habari ya Muhimbili. Muhimbili imejengwa karibuni hivi na bila shaka Muhimbili au Wizara ya Afya wameingia katika *contract* ya ujenzi wa hii hospitali ya Muhimbili. Sasa Muhimbili kama ukiingia katika *contract* ya kujenga chochote lazima mnawekeana *terms*, mimi ninataka ujenge Muhimbili, nataka jengo liwe hivi, choo kiwe hivi, hiki kitanda kikae hivi, mnakubaliana hivyo. Halafu mnapeana *time*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kuuliza, huko Serikalini mikataba inayofanywa na Serikali yetu huwa hawapeani *terms* za kazi yenye we iwe kiasi gani na ichukue muda gani na kwa fedha gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakupa *incident* moja. Nilipokuwa namaliza shule nilikuwa *Secretary* wa Marehemu Karume, siyo huyu wa sasa hivi, waliingia *contract* ya kujenga uwanja wa ndege Pemba. *Contract* waliyoingia ni kwamba *Airport* itue *Boing*. *Boing* ni ndege kubwa, walikuja Wazungu wakajenga *Airport*. Walipojenga *Airport*, ilipomalizika *Airport* ile ikawa inaweza kutua *Boing*, lakini isiwe na abiria wala isiwe na mizigo maana haiwezi kuhimili mzigo, *Boing* iwe tupu itue. Hata kuja kuuliza, wakasema sisi tulikubaliana tujenge *Airport* inayotua *Boing*. Hii inatua, hatukuambiwa iwe na mizigo kiasi gani au iwe na abiria kiasi gani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, isije ikawa hizi *contract* tunazoingia sisi hapa Tanzania ni za aina hiyo za tokea Hayati Karume wa mwaka 1960 huko ningeomba sana hizi *contract* ziangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningependa kuzungumzia habari ya barabara. Mimi nikiwa Dar es Salaam kwa mume wangu huwa tunakaa eneo la Mwenge. Kwa hiyo, nakaa katika barabara inayotoka Ubungo inayokuja Mwenge. Mimi siyo Mbunge wao. Lakini kwa mujibu wa sheria kwa vile nakaa sehemu ile, mimi pia ni Diwani, unaona ! Sasa wao wanajua Mbunge wao ni Mheshimiwa Rita Mlaki, lakini wakanifuata mimi wakanieleza na ningeomba nimwambie Mheshimiwa Rita Mlaki aende akawaone watu wa Kata hiyo ambao Kata yao ni Kawe, naye ni Mbunge wa Kawe, akaonane nao juu ya ile barabara. Barabara ile inawakera sana wananchi. Barabara ile ina *contract* tokea enzi ya Rais Mstaafu Benjamin Mkapa. (*Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, ni kengele ya pili.

**MHE. FATMA M. MAGHIMBI:** Kengele ya pili! Mbona ya kwanza sikuisikia? (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Mbunge anasema kengele ya kwanza hakuisikia, lakini ndiyo hivyo kengele hiyo ni ya pili. Sasa baada ya kumsikia Mheshimiwa Fatma Maghimbii, naomba nimwite sasa Mheshimiwa James Daudi Lembeli na Mheshimiwa Vedastusi Mathayo Manyinyi ajiandae.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kahama, napenda kuungana na Wabunge wenzangu katika kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na timu yake yote kwa kazi nzuri waliyoifanya kuandaa hoja hii ambayo kwa kweli inawapa matumaini Watanzania walio wengi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana wakati nikichangia hotuba ya Waziri Mkuu, nilianza mchango wangu kwa kuzungumzia Buzwagi, leo nitabadilisha kidogo, nitaanza na sekta ya madini.

Mchango wa sekta ya madini kwa pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2007/2008. Mchango wa sekta ya madini kwa pato la Taifa unatazamiwa kuongezeka katika mwaka wa 2008/2009 kwa asilimia 2.7. Ongezeko hili ni dogo sana. Nimesoma katika vitabu hapa vinaonyesha kwamba pato la Taifa litakalotokana na sekta ya madini ni shilingi bilioni 50. Haingii kichwani mwangu na hii ni kutokana na rasilimali ambayo inachukuliwa hapa nchini siyo tu kwa dhahabu, *Tanzanite* na madini ya aina mbalimbali shilingi bilioni 50 kwa kweli ni kichekesho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sekta ya utalii peke yake, pato linalotokana na Mlima Kilimanjaro na Serengeti, ni karibu bilioni 50. Sasa madini na migodi yote hii yanachangia shilingi bilioni 50 tu? Hapa lipo tatizo. Nimefurahi kusikia kwamba Serikali

sasa imeridhia, inakubali kupitia upya sheria ya madini, sera ya madini na kanuni za madini. Mimi naamini lengo lake ni kuhakikisha kwamba sekta hii nayo inachangia pato la Taifa kama inavyostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tatizo ni nini nchi kama Botswana haina rasilimali nyingi kama Tanzania; Botswana ina almasi, ina ng'ombe tena wachache na rasilimali nyingine ni jangwa; sisi tuna madini mengi na sasa inasemekana Tanzania ni nchi ya tatu Barani Afrika kwa utoaji wa dhahabu.

Sasa haya maneno wakati mwingine mimi huwa sipendi hata kuyasikia kwa sababu unaambiwa sifa kubwa sana, lakini Tanzania ni mionganoni mwa nchi maskini duniani. Sasa tunajiuliza ni kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba Serikali mjadala wa kupitia upya, sera, kanuni na Sheria ya Madini uletwe haraka iwezekanavyo ili nchi hii nayo ianzé kunufaika na madini tuliyonayo. Vinginevyo sioni sababu ya kuendelea kuruhusu au kuingia mikataba na makampuni mengine kuchimba madini yetu. Ni afadhali yabaki huko huko mpaka tutakapopata akili na uwezo wa kuweza angalau kuyatoa huko chini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi Shilingi bilioni 50 sijui ni kitu gani? *Royalty*, sijui na nini, basi. Hawa watu hawajaanza kulipa kodi, kila mwaka wanasema hawajapata faida mpaka wataondoka katika nchi hii hawajapata faida. Matokeo yake tutaachiwa mashimo.

Mbaya zaidi, mimi nimezunguka sehemu mbalimbali duniani, nimekwenda pia katika nchi ambazo zinatoa madini kama dhahabu na almasi. Ukienda Afrika ya Kusini kitu cha kwanza utakachokiona ni *land marks* katika maeneo mbalimbali katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Johannesburg kuonyesha kwamba nchi hii ni nchi ya dhahabu. Sasa sisi kwetu hapa ni kichekesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ondoka hapa nenda Mwanza kwa barabara Nzega pale kuna mgodi mkubwa tu, lakini hata *sign* inayoonyesha kwamba hapa kuna mgodi *resolute*, hakuna! Wale Wazungu kule ndani wamejifungia wanaendesha magari makubwa, wanafanya nini? Sasa sielewi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kahama sasa itakuwa na migodi miwili mikubwa hapa nchini, lakini nenda Kahama leo hii, ni aibu! Hata kutaja kwamba mimi natoka Kahama ambako kuna migodi miwili ya dhahabu, hakuna ishara yoyote inayoonyesha kwamba Wilaya hii ndiyo inayotoa migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu. Bado Serikali hata haioni kwa nini, mimi nafikiri sisi Watanzania hatujipendi. Leo hii wakati mchakato wa kujenga mgodi wa Buzwagi unaendelea, barabara ndani ya vile vichaka ni nzuri kuliko za Kahama Mjini. Serikali inaangalia tu. Wale watu ilikuwa ni kuwaomba kwa sababu wanakaa pale pale Mjini kuitisha greda siku mbili/tatu mafuta wanayo, uwezo wanao, hapana. Kahama huwezi kuamini kwamba uko Mjini, ni aibu tupu! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nilikuwa naomba mchakato huu wa kupitia upya sheria hii uletwe haraka iwezekanavyo ili mabadiliko yafanyike na mambo yaanze kwenda kama wenzetu wa nchi nyingine. Napendekeza kwamba Botswana pale huwezi kupata leseni ya kuchimba madini bila kuingia ubia na Serikali. Sasa sisi tunashindwa nini? Kwa nini Serikali isiwe na hisa Barrick?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Norway* wana hisa *Barrick*. *Barrick* Makao Makuu yao yako Canada, sisi tuna madini hapa wanakuja na tunawaruhusu. Kwa nini tusiweke sheria inayosema kwamba yejote atakayetaka kuchimba madini hapa lazima aingie ubia na Serikali au Serikali iwe na hisa angalau asilimia 30. Tunaambulia Shilingi bilioni 50 na tunaendelea kujisifia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nitoke kwenye hii sekta kwa sababu kila nikisikia habari ya madini napata kichefuchefu. Hiyo Buzwagi imepigiwa kelele, nenda kawaone wananchi wa maeneo yale!

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimalizie kwa kweli kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kahama na hasa wa Kata ya Mwendakulima, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu - Mheshimiwa Mizengo Pinda. Namshukuru kwa hekima na busara aliyoifanya kusikia kilio cha wananchi wa Jimbo la Kahama na wa Buzwagi kuhusu matatizo waliyokuwanayo.

Naamini siku zile 90 zilizotolewa kwao zitafanyiwa kazi na mambo yatakwisha. Namhakikishia Mheshimiwa Waziri Mkuu, Buzwagi sasa hivi ni shwari. Lakini nimpongeze na nimshukuru pia Naibu Waziri wa Nishati na Madini - Mheshimiwa Adam Malima, licha ya hali kuwa ngumu, lakini aliifanya kazi ile kwa uadilifu mkubwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu una kijana ambaye anaweza kutekeleza maagizo yako. Napenda nimshukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kidogo sekta ya kilimo, kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu. Wananchi katika Tanzania maeneo mbalimbali wameitikia na wanalfahamu hilo. Wakulima wa pamba wa Mkoa wa Shinyanga na nzungumzie wa Kahama wamejitahidi sana kuhakikisha kwamba wanalima pamba kwa wingi ili kuongeza pato la Taifa kwa nchi yao. Lakini wakulima wa pamba wa Kahama wana matatizo mawili makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tangu mwaka 2004 mpaka leo hawajalipwa fedha yao kwa pamba waliyouza kwa Chama Kikuu cha Ushirika cha *KACU* na Serikali zaidi ya mara tatu ndani ya Bunge hili imeahidi kuwalipa, haijawalipa mpaka leo hii. Sisemi, lakini mchango wangu nitakapokuwa nachangia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, hatutaelewana.

Nitaomba nihakikishiwe kwamba mwaka huu wanalipwa ? Vinginevyo, Serikali iwaambie hatuwalipi. Lakini tatizo la pili na ambalo ni kubwa ni mfumo wa stakabadhi ghalani. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, yuko hapa Bwana Balele,

amefanyakazi kubwa sana kuhamasisha wananchi wauze kwa mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, leo hii ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumeingia watu kama ilivyotokea kule Kusini mwaka jana mpaka wanataka kuchoma nyumba ya Mbunge. Kule Kahama wananchi kwa mamia wamelima pamba yao wanasubiri kuuza mazao yao kwa mfumo huo. Lakini mpaka leo hii yule aliyepewa leseni ya kununua kwa mfumo wa stakabadhi ghalani amenyimwa fedha, wajanja wameingia hapo katikati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, pamba ipo ndani, wanasubiri na kwa nini amenyimwa fedha? Wafanyabiashara wanaonunua pamba Wilayani Kahama wapo hapo katikati. Mimi ninasema haya kwa kujihadhari wasije wakanifanyia kama walivyomfanyia Mheshimiwa Juma Njwayo. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli ni kwamba wananchi wanaumia na kila siku wanapigia simu hapa na wa Bukombe vilevile. Sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie. Aliyepewa leseni ya kununua pamba kwa mfumo huo apewe fedha aende akachukue hiyo pamba ya wananchi kwenye maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla kengele ya pili haijalia, naunga mkono hoja. Lakini bado ninaendelea. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Utalii kuna wizi mkubwa sana unafanya huko na nchi hii inaibiwa kila siku. Inakuwaje Hoteli ya Sopa, Hoteli ya Serena inayochaji dola 400 kwa siku moja na kwa mtu mmoja inalipa *concession* kwa *National Park* dola moja, dola mbili, dola tatu na hawachangii lolote katika kuendeleza Hifadhi hiyo? Watu wanaolala kwenye *camp* wanalipa dola 60 kwa usiku mmoja kwa *National Park*. *National Park* wamejitahidi kutaka kurekebisha hali hiyo, wapo vigogo Serikalini wameweka vidole vyao hapo, mambo hayo wamewaruhusu waendelee kulipa hiyo dola moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI :** Mheshimiwa James Lembeli, nakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Naomba Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Vedastusi Manyinyi na Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili ajiandae.

**MHE. VEDASTUSI M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika hii hoja ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwanza kwa hotuba yake nzuri ambayo kusema kweli imeweza kueleweka vizuri.

Lakini kubwa zaidi namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya hasa baada ya kusikia kilio cha Waheshimiwa Madiwani ambacho kwa kusema kweli kimekuwa ni kilio cha muda mrefu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naamini kwa sababu Serikali yetu ni sikivu, ndiyo maana majibu yake sasa yamepatikana. Lakini pamoja na shukrani hizo, naomba tu kumkumbusha Mheshimiwa Waziri Mkuu kwamba anacho kiporo ambacho anapaswa kukimalizia. Wapo wale Wenyeviti wetu wa Serikali za Mitaa, wapo Wenyeviti wetu wa Serikali za Vijiji. Kwa kweli kazi wanazofanya ni kubwa hasa za kutusaidia kuhamasisha maendeleo kwa ajili ya wananchi wetu.

Kwa hiyo, tunafahamu fika kwamba fedha ni kidogo, lakini hebu m jitahidi ikiwezekana katika bajeti ijayo nao vilevile waweze kukumbukwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wapo watu ambao tunawasahau na tumewapa majukumu. Yapo Mabaraza yetu ya Kata. Mabaraza yetu ya Kata yanafanya kazi nzuri kila mmoja anafahamu. Badala ya ule mlundikano ambao ungekwenda Mahakama, unaishia katika Mabaraza yetu ya Kata, lakini bado wale watu hakuna wanachokipata. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ingeendelea kuwaangalia ione kwa kiasi gani na wao itawasaidia ili waweze kufanya kazi kwa moyo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa mwisho ambao ningependa kwa upande huo watazamwe ni wale Wajumbe au wale Wazee wa Mahakama. Maana wale wazee wanalipwa nadhani kama sikosei ni Sh.1,500/= kwa kesi. Lakini vilevile kesi ile mpaka hukumu itolewe na yule mtu alipe ndipo waweze kulipwa.

Kwa hiyo, inachukua muda mrefu sana na matokeo yake sasa, basi kuna wazee wengine wale wa Mahakama wanashindwa kuwa waaminifu, lakini ni kwa sababu ya shida ambazo zinawazunguka, yawezekana ndizo zinazowafanya waweze kufikia maamuzi kama hayo. Kwa hiyo, ni vizuri tukaendelea kuwaangalia katika bajeti ijayo namna ya kuweza kuyatatua na kuyamaliza hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ambalo nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu, maana tu naamini linahitaji tu ufanuzi wake, ni suala la chakula. Nakumbuka humu Bungeni Serikali ilisema wazi kwamba sasa kutokana na uhaba wa chakula, hawataruhusu chakula kiweze kwenda nje ya nchi kwa maana ya nje ya mipaka yetu. Kwa kweli hilo ni wazo nzuri na ninaamini kila mmoja aliliafiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sasa nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba wapo baadhi ya viongozi wenzetu kwa maana hasa ya Ma-DC badala ya kuzuia chakula kwenda nje ya nchi, sasa wameanza kuzuia chakula hata ndani ya Wilaya kwenda katika Wilaya nyingine.

Kusema kweli kama hali hii ikiendelea, basi itakuwa hatari zaidi. Maana kuna watu wengine ambao tumezungukwa na maziwa kwa maana nyingine hatuna mahali pa kulima, tumezungukwa na mbuga za wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wale wenye maeneo ya kulima ambao leo wanapewa ruzuku ya mbolea tukisema tena wasipeleke chakula kwenye yale maeneo ambayo hayana chakula, nadhani hapo tutakuwa hatuatendei haki.

Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu linahitaji tu maelekezo yako na utaratibu mwagine na mambo yataweza kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nizungumzie kuhusiana na hili suala la uchumi. Mimi ninakubaliana na wenzangu kwamba uchumi katika nchi yetu umeendelea kukua. Lakini pamoja na ukuaji wa uchumi ambao umeendelea kukua katika nchi yetu, bado tumesikia minong'ono mingi baada ya hotuba ya bajeti ya Waziri wa Fedha na Uchumi, wananchi wote wanaendelea kulalamika wanasesma hawaoni matokeo ya kukua kwa uchumi ambalo kusema kweli lina ukweli wake.

Lakini ni vizuri tungejiuliza kwamba hivi ni kwa nini wale wananchi wetu hawaoni matokeo ya ukuaji wa uchumi? Ukuaji wa uchumi katika nchi yetu umelenga zaidi katika zile sekta ambazo zinaajiri watu wachache na ndiyo maana ukiangalia kila mmoja anakubali kwamba sekta ya kilimo inachukua karibu asilimia 80 ya Watanzania.

Kwa hiyo, tunachohitajika kukisema Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna yoyote ile hatuhitaji kupuza kuimarisha kilimo katika nchi yetu, kwani ni kilimo pekee ndicho kinachoweza kuajiri idadi kubwa zaidi ya watu ikilinganishwa na sekta nyingine kama madini pamoja na utalii. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba kama hili tutaliangalia vizuri, basi litawenza kuleta tija na watu wetu wanawenza wakapata maisha bora kama tulivyowaahidi katika Ilani yetu ya Uchaguzi ya mwaka 2005/2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili la bajeti, mimi naunga mkono hoja kwa sababu ukiangalia bajeti yetu ya mwaka huu hakuna anayeweza kuichambua kwamba badala ya kipaumbele Fulani, ni afadhali tungekwenda katika upande fulani. Lakini kinachogomba, fedha zilizopatikana ni chache mno. Kwa hiyo, kutokana na uchache wa fedha, ndiyo maana kila mmoja anakubali kwamba elimu ni kipaumbele. Lakini bado mahitaji tuliyonayo ni makubwa kushinda hizo fedha ambazo zimetengwa katika kipaumbele hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusema kweli mimi niseme moja tu kwamba katika bajeti hii kule kwangu Musoma sina cha kwenda kuwaambia na ndiyo maana hata katika

ile bajeti ya fedha niliendelea kuiangalia, ina muundo mzuri, ina utaratibu mzuri wa vipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi leo mimi ninarudi kule Musoma kwenda kuwaambia kwamba mwaka huu tumepata nini? Maana kila fedha iliyopatikana, sana sana ni upembuzi yakinifu, lami kilomita 0.6, sasa hizo kilomita 0.6 maana yake ni kwamba hata ile kilomita moja haifiki.

Kwa hiyo, ndiyo maana mimi ninasema kwamba kwa mwaka huu kusema kweli hata ninashindwa nitakwenda kuwaambia nini wale watu wa Musoma kwa maana hakuna kitu chochote kilichokwenda Musoma. Lakini sio Musoma pekee yake, hata Mkoa mzima wa Mara.

Kwa hiyo, hili bado nazidi kusema kwamba katika bajeti yetu ya Serikali ya mwaka huu pamoja na mambo mazuri ya vipaumbele kwa kadri ilivyoweza kuviainisha, lakini bado yawezekana basi mwaka kesho tutaweza kuonwa kama wenzetu walivyosema au walivyoweza kutoa shukrani zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kutokana na hali hii, mimi ninarudi kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, natoa kwake maombi maalum ambayo hayataigharimu sana Serikali fedha, lakini yanachohitaji ni ridhaa yake kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali ambayo akinikubalia haya maombi yatasaidia katika kupunguza ukali wa maisha kwa wale wananchi wangu wa Musoma, lakini wananchi wa Mara kwa ujumla.

Tatizo kubwa tulilonalo sasa kule kwetu ni la mfumko wa bei, lakini hali kadhalika tuna tatizo kubwa la ajira. Kwa upande huu, ombi langu la kwanza, Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba utoe kibali kwa ile barabara ya Musoma – Mugumu - Mto wa Mbu – Arusha, kama utatukubalia kwa sababu ilishafanyiwa upembuzi yakinifu na ilishapimwa; na kwa taarifa yako Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kwamba, baadhi ya magari haya madogo madogo yanapita katika barabara ile.

Sasa kwa kuwa Serikali haina fedha na kwa mwaka huu haikutengewa fedha, tunachoomba pale ni kitu kidogo tu; ridhaa yako Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tumekuwa kila siku tunalipa fedha kupita *National Park*; gari moja linalipiwa zaidi ya shilingi laki moja. Tunaomba wale watu wa *National Park*, kwa kuwa ile barabara imeshapimwa, waweke huku vituo vya kukusanya yale mapato waliyokuwa wanayakusanya kule na watutengenezee ile barabara. Kwa kufanya hivyo, magari mengi yatapita na mizigo mingi itakwenda Mara na kupelekea mfumko wa bei unaoendelea kule uweze kushuka.

Kwa mfano, leo kutoka Mugumu kwenda Arusha ni kilomita 600 ukipita katika ile barabara, lakini bado kutokana na zile Mbuga za Serengeti na Ngorongoro, wanalazimika kuzunguka zaidi ya kilomita 1,200. Tafsiri yake, mfuko wa sementi badala ya kuuzwa kwa shilingi 6,000 tutaweza kuupeleka Musoma kwa shilingi 3,000. Kwa hiyo, tunadhani kwamba, kwa kufanya hivyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu utakuwa umetusaidia. Kwa hiyo, hilo nalisubiri ili uweze kutujibu na nipo tayari kutoa

ushirikiano wangu, kuonyesha ni kwa namna gani, barabara hiyo inaweza ikapitika tena hata kabla ya mwezi Desemba, 2008. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kuendelea kutusaidia ni wale ndugu zetu wachungaji, kwa maana ya wafugaji; sisi watu wa Mara wengi wetu tunafuga mifugo. Wafugaji wote wa Mara, lakini hali kadhalika wa Mwanza na Shinyanga ni wafugaji wachungaji; kwa sababu gani? Ili umfuge ng'ombe mpaka ukamuuza aweze kupata kilo 400; ng'ombe yule lazima umchunge kwa muda wa miaka tisa mpaka kumi na ndiyo maana tunasema hawa ni wafugaji wachungaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tunaweza kupunguza ule umri wa kuwachunga kutoka miaka tisa au kumi wakafikia miaka mitatu hadi mine, kwa utaratibu mdogo tu. Tunazo ranchi zetu nyingi kama Mpwapwa, Kongwa, Ruvu, lakini hali kadhalika na maeneo mengine ya Kagera na kule Mwanza Mwabuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Manyinyi, nafikiri hii nafasi ya kuwawakilisha wananchi, kwa kweli Waheshimiwa Wabunge mnaitumia sawa sawa na ndiyo maana kila mtu anashindwa kuona muda unakwendaje. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Nuru Bafadhili, halafu Mheshimiwa Mwanne Mchemba ajiandae.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha kuwa mzima na kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nitazungumzia kuhusu Halmashauri yetu ya Jiji la Tanga na nitajikita katika miundombinu. Hali ya miundombinu iliyoko Tanga kuna ubadhirifu wa hali ya juu. Ukienda katika sehemu za vijiji unakuta kunatengenezwa barabara, lakini wakati mvua inaponyesha barabara yote inakwenda na maji. Kwa hiyo, fedha za Serikali zinakwenda nyingi lakini barabara zinakuwa hazina hadhi ya kuwa zinalingana na fedha, yaani *value for money*.

Nikizungumzia kuhusu ujenzi mathalani wa madaraja, kuna Kata ya Duga, sehemu ya Magomeni, Kamati ya Fedha ilihamua ijenge daraja na nyumba zithaminiwe ili barabara ipite; nyumba zilithaminiwa na daraja likajengwa. Baada ya muda Mhandisi wa Jiji mwenyewe, kwa amri yake, akaamua baada ya kujenga daraja aipindishe ile barabara aipitishe sehemu nyingine. Kwa hiyo, hii inaonyesha kuwa kuna ubadhirifu wa hali fulani unaofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Idara ya Mipango Miji; ndiyo inayosikitisha zaidi na inajiamulia vile inavyotaka yenyewe. Kwa mfano, kuna kijiji kimoja kinaitwa Kata ya Mwanzange, palikuwa na eneo la mzalendo toka tumezaliwa. Eneo lile lilikuwa ni kiwanja cha michezo kwa ajili ya Shule ya Martin Shamba ya zamani, ambayo sasa hivi ni Mwanzange. Kiwanda kile kilichukuliwa tukaambiwa kwamba ni cha wenzetu wa madhehebu ya Ibadhi. Tukauliza nani ametoa amri hiyo; wakatuambia aliyetoa amri

hiyo ni Rais. Tukaomba kwenye Kamati ya Fedha, watupe hiyo nakala ya barua kutoka kwa Rais, barua hiyo hatukuonyeshwa. Hilo tukaliacha kwa sababu uwanja ule ulijengwa ukuta kwa ajili ya makaburi. Sasa hivi wananchi wa Kata hiyo hiyo, ambao wapo katika Mtaa wa Bukoba wananyanyasika, wanafukuzwa, kwa sababu wanaambiwa pia eneo lile ni la watu wa Ibadhi, wakati wananchi hao wengine wapo pale toka mwaka 1962 na wanalipia kodi. Wamepimiwa vile viwanja toka mwaka 1962 na ushahidi ni huu hapa.

Kwa hiyo, watu wale wanadhalilishwa; leo miaka 47 Mtanzania anadhalilishwa ndani ya nchi yake! Bahati mbaya ni kwamba, vyombo vyta habari haviwezi kuonyesha habari kama hizo labda kwa Dar es Salaam, wenzetu wana bahati habari kama hizo zinaonyeshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mzee ambaye alikuwa na kiwanja cha mwanawe ambaye amefariki, lakini alipata kile kiwanja toka mwaka 1990. Amesimamishwa asiendelee kukijenga kiwanja kile na amepewa Mhindi ili akijenge. Alipokwenda kwenye Idara ya Mipango Miji aliambiwa kwamba, hiyo ni ndoto kwa yeye kujenga pale, yaani kuna watu wana hadhi ya kujenga kwenye maeneo fulani na kuna wengine wana hadhi ya kupelekwa kwenye vichochoro, ambako hakuna hata huduma muhimu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mipango Miji hiyo bado naendelea nayo, wana matatizo. Mimi mume wangu alizikwa kijijini kwao Mwambani, kiwanja kile cha eneo la makaburi kikauzwa. Nikamfuata Afisa Mipango Miji akaniambia kuna mtu alijitokeza akajifanya ni ndugu, nikamwambia ndugu ni sisi, mimi pia ni ndugu wa marehemu. Akaniambia nilipe shilingi 309,000, kweli nililipa zile fedha ili kirudishwe kile kiwanja cha makaburi. Baada ya kufuutilia, matokeo yake alinijibu kuwa, kiwanja hiki kimetengwa maalum na barua ninayo ya ushahidi na fedha nilizolipishwa pia ninazo hizi hapa; mpaka leo sijarudishiwa fedha zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye Idara ya Utumishi, nayo ina matatizo. Mtu anapoomba ajira labda kuna nafasi fulani ya afisa, jina linaloletwa ni moja ambapo si taratibu; utachagua vipi kitu kimoja?

Kitu kimoja hakichaguliki, majina yanatakiwa yaje matatu, manne na kuendelea; leo linakuja jina moja ina maana huyo tayari ameshachaguliwa, anataka tu apewe idhini labda na Kamati ya Fedha apitishwe. Kwa hiyo, huu ni ubadirifu wa aina yake katika Halmashauri yetu ya Jiji.

Kuna walinzi ambao walikuwa wakidai malipo ya kufanya kazi baada ya saa za kazi, bahati mbaya mpaka leo wanapigwa danadana hawajalipwa. Hili ni jambo la kusikitisha sana; kuna wengine wamelipwa lakini wengine hawajalipwa mpaka leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mfanyakazi ambaye amethibitishwa kazini toka tarehe 1 Agosti, 2000 kwenye Halmashauri katika kikao kilichokaa tarehe 28 Agosti, 2003, lakini mtu huyo mpaka leo analipwa *payment voucher* hajaingia katika

*payroll.* Kwa hiyo, huu pia ni ubadhifuru wa aina yake, ina maana mtu yule mpaka leo bado hajapata ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu masuala ya wachimbaji wadogo wadogo; hawa wachimbaji wadogo wadogo wananyanyasika sana. Kuna wachimbaji wadogo wadogo katika Kitongoji cha Kigwasi, Kijiji cha Kalalani, Kata ya Mashewa, Wilaya ya Korogwe Vijijini. Hawa wachimbaji wadogo wadogo wanyanyasika sana. Kuna wachimbaji ambao wao wanajiita kuwa ndio wenye haki ya kumiliki lile eneo na hao wadogo wadogo nao wana sehemu zao wanazochimba, lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba, wale wachimbaji wadogo wadogo wanapata madhara makubwa sana. Wapo wanaopigwa, kuna wanaofanyiwa vitendo vya kiunyama na kuna wengine wanapigwa risasi, kiasi cha kuwa wanalazwa katika hospitali na ushahidi ninao huu hapa; huyu ni mchimbaji mdogo ambaye amepigwa risasi ambazo zilikuwa kwenye mapaja yake na hapa anaonyesha risasi ilikuwa imemwingia kwenye utumbo. Kwa hiyo, jamani Mtanzania bado anaendelea kunyanyasika katika nchi yake; tunakwenda wapi na je, tutafika kweli kwa hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia kuhusu viwanda. Tanga ilikuwa na viwanda; kulikuwa na Kiwanda cha Mbolea ambacho sasa hivi kimeuzwa kwa mwekezaji wa mafuta; na kulikuwa na Kiwanda cha Chuma. Viwanda hivi viliwasaidia sana wananchi wa Tanga katika kupata ajira. Walipata ajira viwandani mpaka vijana wetu walikuwa hawawezi kukaa vijiweni; leo viwanda vile havipo. Kiwanda cha Chuma kipo lakini hakifanyi kazi na hatuelewi ni sababu gani Kiwanda hicho hakifanyi kazi. Kwa hiyo, tunaomba Waziri atueleze kwa nini Kiwanda hicho hakifanyi kazi; je, kimeuzwa au vipi? Matokeo yake vijana wetu wanakamatwa usiku au mchana kwa uzembe na uzururaji; wakafanye kazi wapi wakati hakuna hata Kiwanda kimoja ambacho kinafanya kazi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri kunatolewa tenda mbalimbali, lakini tenda zile zinazunguka hapo hapo. Nuru Awadhi ameomba tenda asubuhi, Awadhi Bafadhili ameomba tenda asubuhi, Asha Awadhi ameomba tenda; inakuwa ni watu hao hao lakini kwa majina mbalimbali. Sasa inakuwa tenda zile wanazihodhi cha kuchekesha basi hata tenda ya kupika chai pia mtu wa Tanga hapewi. Mtu atoke huko mikoani mbali ndiyo apewe, watu wa Tanga hawawezi kupima chai. Mtu hapewi tenda hiyo ya kupika chai na inapofika wakati wa kuomba, hata akiwa amehama anadai apewe tenda ile afanye. Jamani lengo letu ni kuwapa watu ajira. Huyu aliye huku mikoa ya mbali akafanyie huko huko, huyu wa Tanga apewe ili aweze kuwatosheliza na watu wa Tanga nao wapate ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kunukuu; katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa 83, Ushirikiano wa Kimataifa inasema hivi: “Mheshimiwa Spika, Serikali yetu ilishiriki katika Kikao cha Wakuu wa Nchi na Serikali ya Umoja wa Afrika kilichofanyika Mjini Addis Ababa, Ethiopia, kuanzia tarehe 31 Januari hadi tarehe 2 Februari, 2008. Katika kikao hicho, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alichaguliwa kwa kauli moja,

kuwa Mwenyekiti wa Umoja huo kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hili ni tukio la heshima kubwa na ni kielelezo cha imani na upendo ambao Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika wanao kwa Uongozi wa nchi yetu. Heshima hiyo imeongeza wajibu wetu katika kushughulikia changamoto zinazolikabili Bara la Afrika katika nyanja za ushirikiano, kuimarisha uchumi, kuondoa umaskini, pamoja na kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa migogoro inayoendelea katika Bara la Afrika.”

Nimesema hivyo kwa sababu Mheshimiwa Rais alipoteuliwa na kusifiwa katika kuendeleza kuliandaa Bara la Afrika liwe na amani na utulivu; kwa hiyo, ninachomwomba Mheshimiwa Rais; najua ni msikivu, mnyenyekevu na mpole, tunaomba azidi kulitilia mkazo suala la mpasuko wa kisiasa wa Zanzibar, ili tufikie kwenye muafaka unaokubalika. Tusikubali, unapofagia unaanza kufagia miguuni kwako ndiyo unaenda mbele, hatufagii kuanzia mbele tukarudi nyuma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesahau pia kuhusu masuala ya uvuvi. Katika Wilaya ya Tanga, Pangani, Mkinga na Muheza katika kijiji cha Kigombe, kuna Bahari ya Hindi, ambayo inatoa samaki wengi sana. Samaki wale wakikusanywa, tunaweza kupata faida kubwa sana katika nchi hii. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali, kama pana uwezekano kwa vile Tanga hakuna viwanda, basi tujengewe Kiwanda cha Samaki na sisi tupate minofu ya maji ya chumvi, badala ya kula samaki wa maji baridi kutoka Ziwa Victoria. Tupate minofu ya maji ya chumvi na tuweze kutoa ajira katika viwanda vitakavyoweza kujengwa katika Wilaya yetu au Mkoa wetu wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Bafadhili, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwanne Mcemba na Mheshimiwa Rizik Omar Juma ajiandae.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi jioni hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote, nachukua nafasi hii ya pekee, kumpongeza yeze mwenyewe binafsi, kwa kazi nzuri na huruma yake aliyoiionyesha tangu alipoteuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa natumia muda mrefu, nachukua nafasi hii pia kumpongeza dada yangu, Mheshimiwa Celina Kombani kwa uteuzi wake, kwa kushika nafasi ambayo ndiyo ilikuwa inamhitaji aishike. Baraka hizo alizipata kutoka Mkoa wa Tabora, kwa sababu alikuwa ziarani na Wananchi wa Izimbili walimbashilia, hatimaye sasa imekuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ndugu yangu Mheshimiwa Mwanri, kwa kuteuliwa kushika nafasi hiyo na kushirikiana na Waziri Mkuu. Nampongeza pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ndugu yangu Mheshimiwa Phillip Marmo, kwa kazi nzuri wanazozifanya na wataalamu wote wa Wizara hii. Pongezi za pekee pia zimfikie Rais wetu, kwa kazi nzuri anayoifanya ya utekelezaji wa ahadi zake ambayo ameianza sasa. Kazi inaonekana kwa

baadhi, nyingine nimezisikia ingawa sijazona; za kuanza kukamilisha matengenezo ya Daraja la Mto Malagarasi. Kwa kweli nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuchangia moja kwa moja hali halisi ya miundombinu. Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Tabora, asubuhi walichangia vizuri sana kuhusu barabara ya kutoka Manyoni - Itigi - Tabora - Kigoma; nawapongeza nao pia kwa nafasi hiyo waliyoionyesha. Mwaka 2007 wakati tunachangia katika bajeti kuhusu hii barabara, bahati mbaya sikuweza kupata nafasi ya kuchukua *Hansard* zote ningezileta hapa, ukawa ushahidi tosha kwa kauli zilizokuwa zimetolewa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe, sisi kama Wabunge wa Tabora, tulikaa meza moja na Waziri Mkuu aliyejukwepo wakati ule, Mheshimiwa Edward Lowassa, pamoja na Waziri wa Miundombinu, ndugu yetu Mheshimiwa Andrew Chenge, tukakubaliana baadhi ya mambo ambayo tulitegemea kwamba, leo kwenye bajeti hii tungeyaona lakini hatukuyaona. Nikisema hivyo ni kwamba, kweli kuna utaratibu au kuna maandalizi ya kutafuta wafadhili wa kukamilisha ahadi hii ya barabara. Tulikuwa tumeiomba Serikali itengeneze barabara hii, angalau kwa kiwango cha changarawe ipitike wakati wote; haikufanyika hivyo inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa masika watu wa Tabora na Kigoma waliteseka sana. Tulikuwa na mambo mawili magumu; reli ilikuwa haifanyi kazi na barabara hazifanyi kazi. Kwa hiyo, tulikuwa na wakati mgumu sana Mkoa wa Tabora kwamba, Serikali ilitutenga, haikuthamini mchango ambao ultolewa kwa Mkoa wa Tabora, kwa ushirikiano ulioikiwezesha Chama cha Mapinduzi kufika hapa kwa kuititia Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna barabara ambayo inatoka Tabora kwenda Nzega ni kilomita 110 tu, Serikali ilisema ingetengeneza kwa kiwango cha lami. Matokeo yake, kwa mwaka huu hakuna hata shilingi moja. Nimwombe Waziri Mkuu, sababu za msingi za kutengeneza hizi barabara zipo; kwanza, zitapunguza mfumko wa bei Mkoani Tabora. Sasa hivi magari yote ambayo yanatoka kubeba mizigo Dar es Salaam kwenda Burundi na Congo, yanapitia Tabora kwa kuwa njia hii ni mkato kwao na haitumii muda mwingi. Inasikitisha kwamba, Serikali bado inasuasua kwa kuona kwamba, haitalipa gharama zile watakazokuwa wameziweka kwenye matengenezo hayo.

Barabara ya Tabora - Nzega kwa lami inaunganisha pia Mkoa wa Shinyanga na Mkoa wa Mwanza. Kwa hiyo, hata kama hii barabara itakuwa haijatengenezwa, bado Wananchi wa Tabora watakuwa na uwezo wa kutoka Tabora Mjini kwenda Nzega, Shinyanga, Mwanza na kupanda ndege kwenda Dar es Salaam au mahali pengine popote. Kwa hiyo, ndiyo maana nimeona nilitoe ufanuzi wa makini wa kuiomba hiyo barabara; kwa kweli tuna hali ngumu sana kiasi ambacho tumekata tamaa. Waziri wetu Mkuu, nina imani analijua hili maana anapita Tabora kwenda Mpanda, amejionea hali halisi. Nina imani, kwa upendo wa kaka yetu, sisemi kwamba ametoka upande wa Magharibi hapana; anaongoza Tanzania nzima, lakini kwa hili amelisikia angalau atalifanyia maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la reli ni tatizo. Kabla ya mbia kuingia, reli ilikuwa inakwenda vizuri sana, haikuwa na matatizo. Tulikuwa tunasusua hivyo hivyo, lakini kwa sasa ameingia mwekezaji ndiyo matatizo makubwa mno. Wakati ule kabla hajaingia mbia, sijui ni Mhindi au nani; kilichotokea ni kwamba, alifika na maamuzi yake, akapunguza ratiba za treni. Serikali haijasema lolote; kwa nini amepunguza ratiba za treni? Sisi tulizoea kuwa na ratiba tatu. Jumatatu, Jumatano na Jumamosi. Amefika ye ye amezikata; hivi Serikali inasema nini; je, hailioni hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea hapo hapo, injini ambazo zinatumika hivi sasa ni za kwetu; ye ye amepata hasara ipi ya uendeshaji kwa sababu bado hajaanza kukamilisha miundombinu? Kwa nini asituache sisi tuendelee na ratiba zetu zilizokuwepo, akileta ya kwake ajue jinsi ya kupanga, lakini kwa leo atufuate sisi? Hata suala zima la uwekezaji Tabora itakuwa ni ndoto; anakuja kuwekeza nini na anapita wapi? Kwa hiyo ni vitu ambavyo ningeishauri Serikali, Makatibu Wakuu wa Wizara hizi husika zote, waangalie jiografia ilivyo, waone sehemu ambazo wanaweza kufanya marekebisho kutokana na kero za wananchi wa sehemu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimechukua muda mrefu kwa sababu miundombinu inanikera. Sasa niende kwenye suala la tumbaku. Suala la tumbaku ni tatizo kwa wakulima wa Tabora, ndio zao pekee la biashara lakini pembejeo hakuna kabisa hawapati. Naiomba Serikali kama inatambua kwamba, Zao la Tumbaku ni Zao la Biashara ambalo linaitangaza Tanzania yetu ni vyema wakulima wa tumbaku wapate ruzuku, itasaidia sana na Tanzania tutapiga hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda unakaribia kwisha na maadam nimezungumza masuala ya msingi, ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameyasikia, basi huku niende haraka haraka. Kuna suala zima la ujenzi wa Ofisi au Makao Makuu ya Wilaya ya Uyui, fedha zilizotengwa ni kidogo sana. Majengo yapo pale yamekamilika, nyumba zilizoanza kujengwa ni ya *DAS* na *DC*, wafanyakazi wengine hakuna. Ningeishauri Serikali ikubali kuingia ubia na Shirika la Nyumba, wajenge nyumba pale kwa ajili ya wafanyakazi wa kawaida halafu wazipangishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kugawa Wilaya ya Urambo ni tatizo. Kijiografia, Wilaya ya Urambo ni kubwa sana; ina kilomita za mraba 26 na ina wakazi zaidi ya 600,000. Sisi kama Wabunge wa Viti Maalum, tunakwenda kwenye maeneo hayo na tunajionea hali halisi ilivyo. Serikali inapata kigugumizi gani, kwenye *RCC* tumeshapitisha, tumekubaliana na nampongeza sana Mkuu wangu wa Mkoa, kwa kazi nzuri anayoifanya; sasa kigugumizi tunakipata wapi cha kuwa na maamuzi, tumepitia taratibu zote na vigezo vyote vinakubalika?

Mheshimiwa Waziri Mkuu, Urambo ni jirani zako na ni ndugu zako, nakuomba lichukulie kwa uzito wa pekee suala hili ili ikiwezekana Urambo ziwe Wilaya mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika anatoka huko, naye pia angefurahi; Mheshimiwa Kapuya anatoka huko, naye pia angefurahi; kwa sababu *DC* wetu anafanya

kazi katika mazingira magumu; eneo ni kubwa mno. Bajeti ambayo anapewa *DC* wa Urambo ndiyo atakayopewa *DC* mwingine ambaye ana Wilaya ndogo. Kwa hiyo, nadhani hili nalo lingechangia kuona uwiano mkubwa uliopo ili hayo mambo yaweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie haraka haraka suala la elimu, nalo nitatizo kubwa. Sasa hivi kumekuwa na mfumko wa kila Waziri anapoingia pale anabadilisha mitaala. Mitaala inabadilishwa sana na hii pia inachangia kushuka kwa kiwango cha elimu. Kwa sababu mnapobadilisha mitaala, darasa la kwanza mpaka la nne labda wana masomo sita, anakuja mwingine anasema hapana yatakuwa masomo kumi. Kwa hiyo, nafikiri Serikali sasa ijipange, inapobadilisha mitaala basi ichukue muda mrefu ili wanafunzi waweze kujua nini ambacho wanafundishwa, lakini hii inakatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kusubiri matokeo ya mtihani; sasa hivi tuna masuala ya utandawazi na teknolojia imeshakua ni vyema wanapofanya mtihani darasa la saba, majibu yatoke mapema. Unatoa majibu Desemba, mtoto anakaa miezi mitatu nyumbani; kwa mtoto wa kike unaashiria nini kama baba au mama hajatamani kupokea mahari ili amuoze, kwa sababu yanachukua muda mrefu? Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali ijipange upya, matokeo ya mtihani yarekebishwe ili yaendane na wakati tuliokuwa nao sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu waliojifunza kipindi kile na wewe ukiwa Mwalimu, sio mitaala inayotumika hivi sasa. Walimu Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari, wapigwe msasa ili mtaala unapokuja wajue nini cha kufanya na wao watawapa semina walimu wenzao kwenye maeneo yao na vitabu viwahi kwa wakati. Mtaala unatangazwa leo, kesho mwalimu anaambiwa afundishe halafu vitabu vinakuja baada ya miezi miwili au mitatu! Tumefanya nini? Kwa hiyo, hivi vyote navyo vinaashiria kuwa kwa kiasi kikubwa sana elimu itashuka.

Uhamisho kwa wafanyakazi; kuna maeneo kwenye Halmashauri zetu na kwenye Serikali Kuu, wafanyakazi wamekaa muda mrefu, kiasi ambacho wamezoleka na kazi wanaiona kama ni sehemu ya maisha yao au ni sehemu ambayo haina nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima naunga mkono hoja ahsante. (*Makofit*)

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia katika hoja hii. (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kutoa pole kwa Wananchi wa Pemba, ambao jamaa zao walifariki kwa ajali ya mashua, iliyotokea wiki iliyopita. Ndugu zangu, jamaa zangu na jirani zangu, ambao wamehusika katika msiba huo, Mungu awape subira na azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa Hotuba yake nzuri ambayo ameiwasilisha mbele yetu, ingawa utendaji unakuwa ni hafifu, lakini nia na dhamira ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni njema kabisa tunaipongeza. Kwanza, naomba nianze kusema kwamba, kuna mchangiaji mmoja asubuhi ambaye alinigusa na lazima nimseme. Naomba uniruhusu niseme kwamba, *CUF* ni Chama cha Siasa, hakijaomba kujitenga hata siku moja na wala hakijawahi kuwa na nia wala dhamira hiyo. Kama kuna mawazo ya watu binafsi ambayo ameyapeleka kokote alikoyapeleka, sisi ni wawakilishi wa wananchi, tusubiri wananchi watuambie nendeni mkatusemee Bungeni kama tunataka jambo Fulani. Hawajatutuma, sisi kama Chama hatuhusiki, *CUF* ni Chama cha Siasa ambacho kinajua masharti ya usajiri wa Vyama vya Siasa ndani ya Jamhuri hii ya Tanzania. Hakiwezi kabisa kujihusisha na mambo hayo ya kipuuzi. Naomba radhi sana, hakuna mtu ambaye anaweza kuthibitsha hilo kwamba, Chama cha *CUF* kinaandaa ama kina haja ya kujitenga. Naomba radhi sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na ndugu zetu Polisi. Jeshi la Polisi ndio ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Popote pale raia alipo, anamtegema askari alinde usalama wake. Kwa maana hiyo basi, askari ni watu wa kuwatunza sana na kuwaweka vizuri, tuboreshe mishahara yao na maeneo wanayoishi ili waweze kufanya kazi zao kwa faraja njema kabisa kwa nia ya kuilinda vyema nchi hii. Naomba niseme kwamba, askari wanapostaa fu huchelewa sana kulipwa mafao yao, jambo ambalo linawapelekea kuwa wanyonge na kuendelea kudhalilika katika maisha, pamoja na familia zao. Mbali na hilo, askari hao huajiriwa kwa mkataba na hivi ninavyozungumza, kuna askari ambao wameajiriwa kwa mkataba na huu ni mwaka sasa, tangu Julai, 2007 hadi leo ninavyozungumza Juni, 2008 askari hawa hawajapewa mishahara. Tunatarajia nini? Askari hawa tunawapeleka kule ambako hatukutaki, ndipo wanapofikia mahali pa kuomba rushwa. Sisi tunapiga vita rushwa huku tunaikaribisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije upande wa elimu. Elimu ndio msingi wa maisha kwa mwanadamu ye yote. Binadamu anahitaji elimu iwe ya dini, iwe ya dunia, iwe ya Quran au ya dini yoyote ambayo anaiamini yeye mwenyewe, lakini elimu ni kitu muhimu. Tumekuwa tukiandaa hotuba nyingi za kuboresha elimu. Ni kweli na kama nilivyosema, Waziri Mkuu ana nia njema kabisa, lakini utekelezaji wa huduma za elimu ni mbovu kupindukia. Madarasa tumejenga mengi ya kutosha, walimu hawatoshi, mishahara yao haitoshi, makazi yao hayatoshi, hawana mazingira mazuri ya kuishi na kuweza kufanya kazi zao vizuri. Ili mwalimu na mtu ye yote aipende kazi yake, basi anahitaji kuwekwa vizuri ili aweze kufanya kazi zake vizuri.

Tunajenga madarasa, tunawaweka wanafunzi wanaofika 100 na kuendelea, mwalimu huyo unamtegema atafanyaje kazi yake ndani ya wanafunzi 100. Wanafunzi kwa mfano wa darasa la kwanza, la pili na kuendelea; hebu niambie mwalimu gani anaweza kuwafundisha wanafunzi hawa kama hatasema uongo. Hawezi kusahihisha madaftari yao, hawezi kukagua kazi zao na matokeo yake tunazalisha elimu duni. Hatuzalishi elimu bora, tunazalisha elimu duni kwa sababu mwalimu hana uwezo wa kulidhibiti darasa. Wanafunzi anayekaa dawati la mwisho kwenye darasa la wanafunzi 100 na una vipindi viwili vya somo lako, kweli utamfikia huyo?

Huwezi kumfikia; atacheza na atafanya anachokitaka, wewe unakuja kukusanya madaftari unampiga marongi, huangalii na huwezi kuangalia vizuri kazi zake. Tunahitaji kuboresha elimu, wingi wa madarasa sio kuboresha elimu. Tuweke walimu wa kutosha, wenyе uwezo na tuwajengee mazingira mazuri ili waweze kukaa katika maeneo wanayoishi na waweze kufundisha vizuri, tupate matunda mazuri kwa taifa letu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado sijamalizia kuhusu elimu; Chuo cha Elimu Kibaha kilikuwa ni kizuri sana na mpaka leo nadhani kinaendelea, lakini ni jambo la kusikitisha kwamba, pale palikuwa na maabara zinazofikia sita na leo ni maabara tatu tu ndizo zilizobaki na tatu ni mbovu hazifai. Tunategemea nini katika kuzalisha walimu wa sayansi, ni kitu muhimu katika ulimwengu wetu? Leo maabara zimekufa, tunajenga wingi wa mabanda, tuziboreshe maabara zile ili ziweze kuzalisha vizuri, hebu tuliboreshe lile eneo jamani. Mheshimiwa Waziri Mkuu, ananisikia na hilo naamini atalishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara za Dar es Salaam hazitoshi; ni mbaya, mbovu, magari yamekuwa mengi na miundombinu iliyopo haitoshi; hivyo, naishauri Serikali kama kuna uwezekano basi tuanze tena kuangalia hali ya barabara zile, tuanzishe barabara mpya angalau *flying overs* kama kuna uwezekano tujenge. Pia nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu au Ofisi yake, iwatahadharishe Wakazi wa Dar es Salaam wasiigeuze ile mitaro kuwa jalala la kutupia taka. Mitaro ile ya maji machafu imegeuzwa jalala, taka zinajaa, ikinyesha mvua inafurika inakuwa uchafu na kuharibu mazingira ya jiji, inaharibu mazingira ya wananchi wenyewe na kuhatarisha hali mbaya ya magonjwa ya hatari ya kuambukiza. Naomba sasa Ofisi ya Waziri Mkuu, iliangalie kwa umakini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye suala la Muungano. Leo ni miaka 44 kama sikosei, tunazungumzia Muungano una kero. Kila akisimama mtu na kila tunapokutana Bungeni, kuna masuala yanayohusu Muungano na kero za Muungano. Naiomba Ofisi ya Waziri Mkuu au Waziri Mkuu mwenyewe, ambaye ndiye Mtendaji Mkuu wa Serikali, ahakikishe kwamba, mwaka 2009 hatuji hapa tena kuzungumzia kero kila siku. Tukija hapa tunaambiwa vikao vinakutana, tunatekeleza hili lakini kero iliyoondoka ni ipi? Hakuna, haitajwi wala haijulikani; tunaendelea kulalamika kero za Muungano kwa pande zote za mbili, kero hazipo upande mmoja. Kwa maslahi ya Watanzania, naomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, tusigeuze hadithi; kila siku kikija kitabu kina Kero za Muungano. Umekuwa ni kama Wimbo wa Taifa, badala ya kuimba Wimbo wetu wa Taifa tunaimba kero kila siku. Naomba sana kero ziondoke, kwenye kitabu umegusia lakini mbali sana kwamba, tunafuatilia hatua kwa hatua, utekelezaji wa kutatua Kero za Muungano lakini hakuna kero zilizotatuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa fedha za JK, Mheshimiwa Rais wetu kwamba, Zanzibar zimekwenda shilingi milioni 500. Hizi fedha hatuzioni na hatujui kama kuna watu maalum wanaopaswa kupewa au vipi? Naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, anieleze kama watu wote wanahuksika au ni kwa watu maalum?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi kidogo kwenye suala la elimu; kuna mwananfunzi ambaye amenigusa na ameniumiza sana. Siku zote tunapiga kelele kuwasaidia watu wasiojiweza. Kuna mwanafunzi mmoja amefaulu kwenda Kidato cha Kwanza katika shule moja ya Tanzania, ambaye baba yake ni mzee sana na hajiwezi kabisa.

Mkitaka nitoe uthibitisho nitatoa. Bahati mbaya sana, ameshindwa kuripoti shulen iiasi cha kipindi kisichopungua miezi sita anapigwa danadana, mara asimamishwe darasa kwa muda mpaka baba yake atakapopata uwezo ataaleta fedha. Hakuna lililofanyika. Michango ambayo mzee huyo angeweza kuilipia, nadhani hana uwezo hata wa dakika moja. Anatakiwa aliye kwanza shilingi 20,000, halafu kuna fedha ya mwaka 10,000, kuna mchango wa sare sijui shilingi 24,000, mchango wa tahadari shilingi 5,000, mchango wa jembe na ndoo na vitu vingine. Shule ya kutwa Waheshimiwa Wabunge, kuna *ream* ya karatasi A4, fulana yenyenye jina la shule shilingi 4,000, kitambulisho shilingi 2,000, fedha ya picha shilingi 1,500, mlinzi shilingi 5,000, maji shilingi 3,000, nembo ya shule shilingi 1,500 na kuboresha majengo kwa kurabati shilingi 10,000. Mzee huyo anapompeleka tu mtoto aliye shilingi 25,000 za jengo. Tunawapeleka wapi watoto wa maskini, wanyonge, waliokuwa hawana uwezo wa kumiliki hata mlo wa siku moja, achilia mbali michango hii?

Namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliangalie kwa kina hili, jamani tutafute namna ya kuwawezesha watoto wetu kusoma kwa makini kwa maslahi ya Tanzania hii. Sisi tunaondoka, wao ndio warithi wa Tanzania hii, kama hatutawajengea mazingira mazuri, wakawenza kupata elimu kwa njia ambazo zitawasaidia, bila kuwa na woga wala ugumu, nadhani taifa hili tutalipeleka kubaya. Naomba sana hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye uboreshaji wa Daftari la Wapiga Kula. Nashukuru sana Daftari hili huboreshwa kila linapohitajika au zaidi ni wakati wa uchaguzi. Mambo yanayojitokeza wakati wa uchaguzi; tunasema Tume ni huru, lakini yale yanayojitokeza wakati wa uchaguzi hayaonekani kama Tume ni huru. Kama ipo huru, basi labda watendaji wanakiuka sheria na taratibu. Kama watendaji wanakiuka sheria na taratibu na Tume inakaa kimya; inaonekana dhahiri na hicho ni kiashiria tosha kwamba, Tume hiyo si huru na inaegemea upande mmoja wa Chama, kwa maana hiyo yale yanayotendeka Tume inayafumbia macho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyeikiti, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia leo. Pili, naishukuru kwa ujumla, Wizara iliyoleta makadirio yake hapa, kwa hotuba nzuri ambayo inaeleweka tena imechambua mambo kwa kina. Wengine tunaonzeza ongeza, lakini imechambua vyakutosha kabisa.

Tatu, nawapongeza walioiandaa Hotuba, nikianza na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri wake wote wawili, Naibu Mawaziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kubwa, kwa sababu inaingiza Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na

Uratibu wa Bunge. Mmefanya kazi nzuri sana, haya tunayoyasema ni kuongeza kusudi mwakani yawe mazuri zaidi ya leo. Kwa upande wangu, sina matatizo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu, naanza na elimu. Ukurasa wa 87 wa Hotuba unasema; naomba ninukuu: “Tuongeze juhudu kujenga miundombinu ya kutosha kwa ajili ya elimu kwa wote.” Narudia, kwa ajili ya elimu kwa wote kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na mimi naongeza chumvi na mafunzo ya ufundi. Nimependezwa na muishilio huu wa hotuba, kwa sababu nitaanza na elimu. Mimi kila nikisimama hapa, kwa kweli Jimbo langu mnalijua, Mkoa wangu mnaujua ni Mkoa na Jimbo la watu wenye ulemavu, pamoja na akina mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe pongezi kwa Serikali kwa upande wa elimu, kuna mengi mema yamefanyika. Wanafunzi wameongezeka, madarasa yamejengeka, jitihada za walimu na nyumba zinafanyika. Pongezi sana lakini pana upungufu kwa kundi langu. Pamoja na kwamba, hotuba hapa imefafanua kabisa miundombinu itakayofaa kwa elimu kwa wote, watoto wenye ulemavu kwa upande wa elimu bado nitaendelea kuishauri Serikali kwamba, nitaendelea kulia, ingawa silii machozi lakini wakati mwingine inauma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo ya shule zetu zote za sekondari na msingi, mwaka jana niliambiwa kuna ramani maalum zinazofuatwa au zilizotengenezwa kusudi majengo yawe rafiki kwa watoto wa aina zote za ulemavu. Nasikitika kusema kwamba, nimefanya ziara kama Kamati na kama mimi binfasi, nikiangalia hayo hayo niliyoahidiwa; hakuna linalofanyika kwa upande huu. Hivi hawa watoto wote wataweza na hata jinsi ya kufika darasani hawawezi. Kwa hiyo, naomba msaada hapo, zile ramani sasa sielewi kama zimetoka Wizara ya Elimu au zimekwama kwenye Halmashauri zetu? Niwalaumu Wakurugenzi na Wahandisi au nimlaumu nani? Hakuna kinachofanyika, kwa hiyo, kikwazo hicho bado kipo pale pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, lazima nishukuru kwa walemovu wasiosikia. Serikali imejitahidi sana kununua vifaa, nimethibitisha na kila shule yenye kitengo cha viziwi vifaa hivyo viro. Ninashukuru sana kwani vifaa ni aghari. Vifaa vingine vya wale wenzangu wenye matatizo ya akili viro, lakini kwa wengine hakuna. Wasioona hatujajitosheleza hata kidogo; na wa *wheel chair* hatujajitosheleza hata kidogo. Kwa hiyo, kwa upande huu, natarajia Wizara ya Elimu itakapoeleza mambo yake, kutakuwa na mengi mema kama ilivyofanyika kwa upande wa viziwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande huo huo wa elimu, walimu wanaohangaika na hao watoto wenye ulemavu wa aina zote, bado wanalamika na nadhani ni haki yao jamani. Wengine hatujaona tu wanavyohangaika na hao watoto, wanaomba sana sana kama kuna uwezekano, Serikali iwafikirie posho ya mazingira magumu ya kufundisha watoto hawa. Walimu wote wana matatizo lakini hawa sasa

wananyongeza ya matatizo. Wengine inabidi wawabebe watoto wale kutoka kwa wazazi wao kuwaleta shulen i kana kwamba, wale ndiyo wazazi wao.

Jamani chonde chonde na hawa si wengi. Nikiongezea hapo hapo, walimu hawa wenyenye taaluma hii ya kumudu watoto wenyenye ulemavu hapa nchini, bado ni wachache. Patandi kama Chuo kinachoandaa bado ni kidogo na wanatoka wachache kila mwaka na vitengo vipo vingi tu. Sasa hivi karibu kila Wilaya, kila shule ina vitengo kwa sababu watoto wenyenye ulemavu ni wengi na wa aina mbalimbali. Kwa hiyo, hilo nalo kwanza waongezeke kiidadi halafu waweze kuangaliwa katika hali zao za kuwapa moyo kuweza kuangalia kufanya kazi hii ya Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo katika elimu, nimeona katika idara ya elimu kuna idara zote. Walimu hawa wanaohudumia watoto wenyenye ulemavu, wamependekeza kwamba, basi pawe na afisa elimu maalum katika kila Wilaya, kwa sababu huyo ndiyo atakayesaidia kuratibu masuala ya watoto wenyenye ulemavu katika eneo lake. Mbona wapo wa vielelezo, wapo wa michezo, wapo wa mitaala; hawa ni muhimu lakini hawapo Mawilayani. Kwa hiyo, ninapendekeza kwamba, waanzie Wilayani au Mkoani pale, iwe kwenye Kamati ya Ushauri ya Mkoa awepo ili aweze kusaidia kuyaangalia masuala ya watoto wenyenye ulemavu hasa katika shule mbalimbali tulizonazo. Vinginevyo, kuna *tendency* ya kusahauilika au ya kuwekwa pembeni, lakini hawa nao ni wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo, naomba nizungumzie suala la ajira. Suala la ajira kwa wasomi wenyenye ulemavu kwa sasa ni gumu. Tunajua kuna sheria ambayo bado hata hajarekebishwa na sijui tutairekebisha vipi. Hata wale waliohitimu Vyuo Vikuu ajira rasmi ni matatizo. Wanaishia kujunga kwenye Taasisi Zisizo za Kiserikali kama mtu amebahatika, lakini hawa wamehitimu. Sasa hivi tunafanyaje? Mtu huyu amesoma kwa shida mpaka kufika hatua aliyofikia; ajira rasmi hakuna na ya kujiajiri ndiyo ngumu kabisa.

Katika Programu ya Uwezeshaji, pamoja na kwamba, kuna fedha za Mheshimiwa JK tunazilalamikia hapa, hata wale wenyenye uwezo hawazipati, sikwambii hawa wenzangu na mimi. Vilevile kuna mikopo katika Halmashauri zetu ambazo ni Mfuko wa Vijana na Akina Mama, lakini nachelea kusema kwamba, inakuwa vigumu kwa Watendaji kuweza kuwahamasisha watu wenyenye ulemavu waweze kupata mikopo ili wajiajiri wenye nayo hiyo ni tatizo. Kwa hiyo, hata kwenye sehemu ya uwezeshaji kwa hawa, bado walio wengi hawajafaidika na shughuli hizi. Sana sana kuna Halmashauri chache, kwa mfano, Shinyanga; niliwahi kusikia walikopeshwa. Wanafanya kazi vizuri, lakini ni Halmashauri chache, walio wengi hakuna. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba utakapokuwa na Watendaji sijui *DCs*, jamani na sisi tupo tunahitaji kujiajiri tuweze kujitegemea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *SACCOS*, katika huo huo uwezeshaji; hawa bado hawahamasishwi vya kutosha ili waweze kujunga hata kwenye vikundi ambavyo baadae vitaweza kukopesheka, inakuwa ni vigumu sana kwao. Suala lingine kuhusu watu wenyenye ulemavu, ambalo ningependa kulizungumzia ni la UKIMWI. Rasilimali nyingi sana zinapelekwa Wilayani kwenye Halmashauri zetu, kwa kupitia

taasisi ambazo si za Kiserikali na hata za Serikali yenyewe. Katika Programu nyingi zinazoendelea kuhusu UKIMWI, watu wenye ulemavu hawajafaidika nazo. Naupongeza mfano wa Halmashauri ya Morogoro, niliona waliwekwa kwenye Programu, wameshukuru kweli kweli. Mbozi walijumuishwa na kufundishwa, nao walifurahi kweli kweli. Hili ni suala muhimu, sote hapa tunajua na watu wenye ulemavu nao huwa wanafanya ngono zembe ili waishie wapi?

Huku ameletaa, huku UKIMWI, unyanyapaa na unyanyasaji unakuwa mkubwa zaidi. Kwa hiyo, naomba sana katika Programu hizo na wao wasisaha unlike. Katika Halmashauri walizosahau basi nawakumbusha, wale ambao wameanza wasonge mbele kwa sababu ni kwa manufaa ya wenzangu hawa walio wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi wa Vyuo Vikuu wana nafasi ya kukopa ili kuweza kujiendeleza katika masomo yao. Mimi ninaomba na wameniagiza si wengi wanaofika hatua ya Chuo Kikuu; jamani wanafunzi hawa wasomeshwe bure, hapatakuwa na hasara yoyote. Si wanafunzi wa vyuo vikuu tu, ningeomba katika ngazi zote za elimu watoto wenye ulemavu wasomeshwe bure vinginevyo, hawataweza kufikia hatua hii. Mtasema wazazi wao wachangie lakini wazazi wao wamepata shida kuwalea na kuhangaika nao, ndiyo mchango wao na kuwafikisha darasa la kwanza, *form four* mpaka *form six*; mtaendeleaje kuwa *punish* jamani? Kwa sababu hawa wazazi wamefanya kazi mpaka hawa watoto wamefikia hapo. Ninaomba sana Serikali isomeshe bure watoto wenye ulemavu ngazi zote, kwa sababu si wengi wanaoweza kwenda shule. Mbona mengine tunachangia kwa bidii zote? (*Makofit*)

Mheshimiwa Mwenyeketi, wakati mwengine huwa nachuma dhambi, mpaka nasema labda masuala ya watu wenye ulemavu yangewekwa kwenye Wizara ya Juu, ambayo itaweza kutoa maelekezo kwa Wizara nyingine, kwa sababu mambo hayaendi. Yanaandikwa, yanasmwa na tunayatetea lakini hayaendi. Labda kama yupo wa juu, akitoa amri hawa huku watasikia; je, tufikie hapo? Ninalopendekeza si kwamba masuala ya watu wenye ulemavu yaende kwenye Wizara ya juu ambayo ni aidha Ofisi ya Waziri Mkuu au Makamu wa Rais, hata kitengo ndani ya Ofisi ya Rais mwenyewe. Kama si hivyo, kila Wizara itenge rasilimali za kutosha kushughulikia sekta inayowahusu walemvu ndani ya eneo lao kuliko ilivyo sasa. Kwa sababu ukizungumzia hiki, unaambwiwa nenda Ustawi wa Jamii ambayo ni Idara ndani ya Wizara ya Afya, lakini si kila kitu ambacho kinaangaliwa na Ustawi wa Jamii.

Kwa hiyo, naomba sana Wizara karibu zote, kwa sababu naona ulemavu ni mtambuka, hauna jinsia, hauna umri, hauna rangi wala hauna roho. Kwa hiyo, ushughulikiwe na kila Wizara, labda ndiyo pataweza kuwa na kitu ambacho kinaonekana hivi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na haya kwa leo, ninajiandaa kuchangia kwenye Wizara husika ambayo ina kipengele hicho cha Ustawi wa Jamii. Huko kuna mambo mengi tu ambayo tunapaswa kuona yanakaa sawasawa, lakini kwa ujumla wake naomba yatekelezwe. Majengo yaye rafiki, vifaa mashulenii viongezeke, watoto hawa

wasomeshwe bure katika ngazi zote hata kwenye vyuo vya ufundi. Ahsante sana.  
*(Makofî)*

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana na mimi kupata nafasi hii adimu ya kuchangia hoja ya Waziri Mkuu jioni ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti na mimi nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba yake nzuri. Nawapongeza pia Mawaziri katika Ofisi yake; Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Celina Kombani na Naibu Waziri katika Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Aggrey Mwanri. Aidha, nawapongeza Makatibu Wakuu na Watendaji wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu.  
*(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba na mimi nichangie maeneo machache. Kwanza, nianze na suala la kugawa Wilaya. Wananchi wa Wilaya ya Kondoa, wamefarijika sana na kauli ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa anajibu swalî langu kuhusu suala la kuigawa Wilaya ya Kondoa. Serikali imekiri kwamba, Wilaya ya Kondoa ni kubwa na inahitaji kugawanywa katika Wilaya mbili na lengo hasa ni kusogea huduma karibu na wananchi. Kwa niaba ya wananchi hao, napenda nitoe shukrani za dhati kabisa kwa Serikali kutambua hilo. Ombi la wananchi ni kwamba, hili zoezi la kuigawa Wilaya liharakishwe ili wananchi waweze kunufaika kutokana na kusogezwa na huduma hizo za kiutawala karibu na wananchi. *(Makofî)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ambalo nataka kuchangia ni kuhusu elimu na nitajikita katika ngazi ya elimu ya sekondari. Napenda nami nitumie nafasi hii, kuipongeza Serikali kwa jitihada kubwa ambayo imefanyika, kwa kipindi kifupi kupanua elimu ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwapongeze Watanzania wote, hususan wapiga kura wa Jimbo la Kondoa Kusini, kwa kuchangia kwa hali na mali. Uboreshaji wa elimu ya sekondari hivi sasa hali inaridhisha kabisa, kila Kata ina sekondari yake na kwenye maeneo mengine, Kata moja ina zaidi ya sekondari moja; kwa hiyo, kazi kubwa imefanyika katika muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo changamoto kutokana na upanuzi huu, moja ni upungufu wa Walimu, wenzangu wamesema sana kuhusu jambo hili. Mwaka 2007 nilipokuwa nachangia ofisi hii nilisema; wanafunzi hawawezi kupata elimu ya sekondari kwa kuwepo katika mazingira ya shule bila kufundishwa na walimu na nikasema walimu ni msingi wa elimu katika shule yoyote hivyo, upungufu wa walimu ni lazima ufikiriwe na ufanyiwe kazi haraka iwezekanavyo.

Katika shule zetu za sekondari za Kata nyingi kwa kweli wanafunzi hawapati elimu kikamilifu, kwa sababu walimu hakuna ama ni wachache mno. Hizi Sekondari za Kata tumewahi kusikia kwamba, kuna sekondari ina walimu wawili kwa shule ambayo ina kidato cha 1 – 4. Hapo hatuwatendei haki watoto wetu, tunawaweka katika mazingira ya shule lakini hawapati elimu yoyote. Kwa hiyo, naomba Serikali itafute kila

linalowezekana, kuweza kuharakisha kupata walimu wa kutosha na kuwapanga katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ambayo nilitaka kuizungumzia ni ukosefu wa maabara. Wabunge waliotangulia kuchangia hoja ya Waziri Mkuu wamezungumzia suala hili, lakini nataka kusisitiza hapa kwamba, hivi sasa dunia hii ni ya sayansi na teknolojia, lakini sisi hatufundishi sayansi katika shule za sekondari, kwa sababu hatuna walimu na hakuna maabara. Kwa hiyo, hata kama walimu wapo lakini kinachofundishwa ni nadharia tu, vitendo havifanyiki katika shule zetu. Naomba Serikali iangarie namna ya kuweza kujenga maabara katika shule zetu zote za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba, Watanzania ama wananchi katika Kata zetu, wametumia rasilimali zao nyingi katika kujenga majengo, lakini hawawezi kujenga kila kitu ni lazima Serikali iweke mkono wake hasa katika suala la maabara. Kwa hiyo, naomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu, itenye pesa za kutosha kujenga maabara katika shule zetu zote, vinginevyo, hakuna elimu ya sayansi inayotolewa katika shule zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika changamoto nyingine ni ukosefu wa vifaa vya kutolea elimu kama vile vitabu, shule zetu nyingi hazina vitabu kabisa; sasa unatengemea watoto watapata elimu namna gani kama hakuna vitabu? Wizara au Serikali kwa ujumla, iweke mkakati wa kununua vitabu na kupeleka katika shule zetu zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa Mwalimu na pia nilikuwa Mkuu wa Shule. Shule mpya ikifunguliwa, kwa kawaida Wizara husika ama Wizara ya Elimu, ilikuwa inahakikisha kwamba, inanunua vifaa vya kutosha na kupeleka kwenye shule mpya inayofunguliwa. Hivi sasa shule zinafunguliwa lakini vifaa havipelekwi, kwa hiyo ni jikumu la mzazi sasa kununua vifaa vya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vitabu tunaweza kununua, lakini vifaa vingine hatuwezi kununua. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali katika hili iwekee mkazo ama iangalie kwa macho mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la umeme mashulen, huduma ya umeme kwa kweli ni hitaji muhimu katika shule zetu za sekondari. Shule zetu nyingi tulizojenga zipo gizani, hata kama kungekuwa na hosteli watoto wasingeweza kusoma kwa sababu hakuna umeme. Napendekeza kwamba, kuna baadhi ya shule zipo karibu sana na umeme wa Gridi ya Taifa, kwa mfano, katika Jimbo langu kuna shule kama Mondo, Goima, Songolo, Chandama, Soya, Mwailanje na Mrijo, zimepitiwa na Umeme huo lakini kwa kuwa hatuna mpango wa kuzipatia umeme, shule hizi zipo gizani. Pamoja na kwamba, wananchi wengine wote wanapatiwa umeme kwa sababu wana uwezo wa kulipia, lakini shule tulizojenga hazina uwezo wa kulipia. Serikali iweke Mpango Maalum wa kuweza kuzipatia umeme shule hizi ambazo zipo karibu na Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa shule zile ambazo zipo mbali na umeme, tuna vyanzo vingi vya umeme siku hizi; kuna *solar* ama umeme wa juu, basi tuweke

utaratibu wa kuweza kuzipatia shule hizi umeme wa jua, angalau waweze kuwa kwenye mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine katika ujenzi wa Sekondari ni ukosefu wa hosteli. Naamini kabisa kwamba, kwa mazingira ya Tanzania, shule za sekondari za kutwa vijiji haziwezi kufanya kazi kwa sababu ya mtawanyiko wa vijiji; utakuta Makao Makuu ya Kata ambako ndiko shule inajengwa ipo kilomita 20, mahali pengine kilomita 15 au 30. Shule za kutwa zinajengwa, kwa hiyo, watoto wanategemewa kwenda kusoma na kurudi nyumbani, hawataweza kumudu umbali huo; ni muhimu kuwa na hosteli kwa shule zetu zote za vijiji na hasa katika Jimbo langu la Kondoa Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika Hotuba ya Waziriri Mkuu, suala la hosteli anasema mwaka 2007 alijenga hosteli 12 kwa ajili ya wasichana kutoka katika mikoa ya wafugaji. Sasa mikoa ya wafugaji sijui ni ipi, kwa sababu wengi hatujapata? Napenda kusisitiza kwamba, idadi hiyo ni ndogo mno na mahitaji ni makubwa mno, kwa hiyo ni lazima tujenge hosteli nyingi zaidi; kama Serikali haina uwezo, tutafute wafadhili waweze kutusaidia jambo hili na si kwa ajili ya wasichana tu pamoja na wavulana pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa nyumba za walimu, Serikali ni lazima iweke mkono wake pale. Wananchi wamechangia lakini Serikali naona mchango wake ni mdogo sana katika kuboresha majengo ya shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia elimu, naomba nипитie haraka haraka maeneo mengine kama maji. Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi katika ukurasa wa 82 - 83 inasema hivi: "Kuwawezesha wananchi mijini na vijiji kupata maji safi na salama na ya kutosha, kwa matumizi yao ya kawaide karibu na sehemu wanakoishi na kwa mahitaji ya kiuchumi. Lengo ni kuwafikishia huduma hiyo asilimia 90 ya wakazi wa mijini na asilimia 65 ya wakazi wa vijiji ifikapo mwaka 2010."

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina uhakika kama lengo hili litafikiwa kwa sababu tatu; kwanza, hakuna miradi mipy ya maji ambayo inatekelezwa hivi sasa. Jimboni kwangu hakuna hata mradi mmoja tangu mwaka 2005, sasa utafikia namna gani hiyo asilimia 90 na 65? Pili, miradi ambayo ilianza kabla ya mwaka 1995 nayo imesimama, kwa hiyo, hakuna kinachoendelea na kwa hiyo hakuna huduma inayoendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mifano mingi sana kwa hilo, lakini kwa sababu ya muda sitawenza kuitaja, lakini vijiji 13 vyenye miradi ambayo imesimama tangu mwaka 2005 mpaka leo, kama hatutaweza kuikamilisha, huduma haitawenza kuboreka. Kwa hiyo, siamini hiyo asilimia tunayoitaja katika Ilani kama itafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi ni kwamba, hata miradi ambayo ilikuwa inafanya kazi tumeiachia, kwa mfano, leo nilikuwa nimeuliza swali la Ntomoko ni mradi mkubwa ambao ulikuwa unatoa huduma ya maji kwa watu 60,000 hivi sasa haufanyi

kazi. Asilimia ya upatikanaji wa maji katika Jimbo langu la Kondoa Kusini imeshuka, labda ipo kwenye asilimia 20. Kwa hiyo, siamini kama hilo lengo tutalifikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jitihada zifanyike ili miradi mipyä ianze, tukarabati miradi iliyopo na tumalizie iliyokwisha anza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme kidogo kwamba, kuna mchezo sasa hivi amba Serikali inafanya wa kupunguza bajeti ya maji. Huo mchezo ni mbaya, naomba bajeti ya maji iendelee kuboreshwa, hitaji la maji si kwa Shinyanga na Kahama peke yake, ni kwa nchi nzima. Kwa hiyo, tunaomba mwakani turejeshe pesa hizo kwenye bajeti ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu afya ni matatizo makubwa, labda niseme kwamba, naipongeza Serikali kwa kauli yake ya kujenga Zahanati katika kila kijiji na Kituo cha Afya katika kila Kata. Ushauri wangu ni kwamba, kabla hatujaanza kujenga, tutafute watumishi wa kutosha na dawa za kutosha katika zahanati na Vituo vya Afya vilivypopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la barabara. Wenzangu wamezungumzia sana barabara zao na mimi naomba nitaje barabara moja ya Iringa - Dodoma – Babati. Nimekwisha elezea umuhimu wake, sitaki kurudia lakini hapa kazi ya upembuzi yakinifu imechukua miaka 10. Sasa hivi kuna usanifu, una miaka sita sijui utakwisha lini na ujenzi utaanza lini? Naomba usanifu uishe mapema ili barabara hiyo ianze kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kuhamia Dodoma; nimeshangaa sana niliposoma Hotuba ya Waziri Mkuu ukurasa wa 74, aya ya 110 anasema; kutakuwa na mjadala wa Kitaifa kuhusu kuhamia Makao Makuu Dodoma! Mimi nimeshangaa sana, nafikiri mjadala ulikwishafanyika na uamuzi ulikwishafanyika, suala lililobaki ni kutunga Sheria ya kuhamia Mji Mkuu wa Dodoma.

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Degera, hiyo ni kengele ya pili, muda wako umeisha

**MHE. PASCHAL C. DEREGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naunga mkono Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Degera, kwa kweli kasi ni kubwa mno, kila anayesimama anasahau kabisa muda unakwendaje. Hongera sana Mheshimiwa Degera, nafikiri hata wapiga kura wamekusikia na wataendelea kuwa na imani na wewe. Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Shoka na Mheshimiwa N'hunga ajiandae. (*Makofi*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti. Nashukuru kwa kupata nafasi jioni hii na mimi niweze kutoa maoni yangu japo kidogo. Awali ya yote, nachukua fursa hii kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia afya njema. Baada ya hapo, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuchaguliwa kuwa Waziri Mkuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, nataka nizungumzie kuhusu suala la Ofisi za Wabunge. Napenda nishukuru utaratibu uliotumika safari hii wa kugawa Ofisi za Wabunge, kwa sababu ofisi hizi 40 zilitolewa pesa kwa ajili ya kujengwa. Sisi tulioko mbali tunashukuru tumebahatika kupata hizo ofisi.

Kwa hiyo, napendekeza hizi ofisi nyingine kumi zilinzojengwa mwaka huu, nazo vilevile ziangaliwe kama mgawo wa mara ya kwanza. Zaidi naomba hii ramani ambayo huwa tunaisubiri, ishughulikiwe haraka ili ipatikane na suala hili lianze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ninalotaka kulizungumzia ni kuhusiana na maslahi ya Madiwani. Tunashukuru safari hii maslahi ya Madiwani yameongezwa. Kuongezwa ni vizuri lakini mimi binafsi sikufurahi, hizi shilingi bilioni 4.8 walizotengewa zingekuwa mshahara mimi ningefurahi zaidi, kwa sababu posho ni posho, yaweza kubadilika. Ingekuwa ni mshahara kusingekuwa na mabadiliko tena. Wenzetu wangekuwa wanasonga mbele moja kwa moja. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, naona ametoka kidogo lakini wasaidizi wake wapo; hili suala liangaliwe; kwa nini hawa Madiwani hatuwalipi mshahara, kuna kigugumizi gani kulipwa mshahara?

Watu wengine wanalipwa mshahara, mpaka Watendaji wa Vijiji huko wanalipwa mshahara, lakini Madiwani ni watu wa posho tu. Hapa ndani kila wakikaa wanasifia tu kwamba, Madiwani ni watekelezaji wetu wazuri, wanasimamia Halmashauri lakini hatusemi nao tuwape mshahara, tunataka wapewe posho. Kwa hiyo, Madiwani ni wenzetu, baada ya sisi ni wao ndiyo waliopo chini yetu, kwa hiyo, naomba nao walipwe mshahara wasiendelee kulipwa posho kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile napenda kuchukua nafasi hii, kuwaombea Wenyeviti wa Mitaa na Wenyeviti wa Vijiji nao walipwe posho. Wao wasipewe mshahara, lakini angalau wapewe posho, kwa sababu nao wamechaguliwa. Mtu akichaguliwa naye anategemea kupata chochote, asichaguliwe halafu anakuwa jina tu, tena amechaguliwa kwenye *post* ya kuongoza watu Kiserikali. Naomba na hawa nao waangaliwe, wapatiwe japo posho kidogo kwa ajili ya sabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la wavuvi wa Bahari ya Hindi. Wavuvi hawa wamepata mtihani; wameletewa barua kutoka kwa Mkurugenzi kuwa uvuvi wa kutumia *ring net* hauruhusiwi tena. Mkurugenzi kaenda mbele zaidi, anazuia watu wasizame baharini kwa miwani, wasiogelee kwa viatu na wasizame kwa gesi; sasa sijui Mkurugenzi huyu ni mtaalam gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema ni mtalaam feki; haiwezekani mtu azame bila ya miwani na miwani ile kazi yake ni kukusaidia kuona mbele unachokitafuta. Unamzuia mtu asitumie miwani; sasa atumie nini? Halafu anazuia watu wasiogelee kwa viatu, vile viatu kazi yake ni kumwezesha yule anayeogelea aweze kuwa na *speed* zaidi, haina madhara yoyote na mazingira wala samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia anazuia watu wasizame kwa gesi, eti gesi ya *oxygen* nayo inaharibu mazingira; sijui ni mazingira gani hayo yanayoharibiwa na *oxygen*, maana hapa tulipo pana *oxygen* wala hatujaharibikiwa na jambo lolote? Kwa hiyo, sote tulipo hapa, naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, atakapotoa majumuisho, atueleze sababu za hawa wavuvi wetu kuzuiliwa kuvua, kuzamia kwa miwani, kuzama kwa kutumia gesi na kuogelea kwa viatu na je, watumie zana gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu unapowazuia kuzama, siku hizi baharini watu wameendelea; msifikirie mnaoendelea ni ninyi mnaofanya kazi za juu tu na walio baharini nao wanaendelea hivyo hivyo. Mheshimiwa Jumanne Magembe, analijua hili, nao wanaendelea kama tunavyoendelea sisi. Kwa hiyo, hawa nao wanapotaka kuingiza nyavu zao baharini, hawaendi tu wakatia nyavu; kwanza, unazama na miwani unaangalia kama samaki wapo unatia nyavu. Huwezi kwenda kuteremsha nyavu bila kujua kama pana samaki au hakuna. Kwa hiyo, suala hili liangaliwe, linawa-*affect* watu wengi sana, kwa sababu huyu Mkurugenzi kaandika barua kwa Wakurugenzi wa Majiji, Manispaa, Wilaya na Miji kuwa wote wawazuie watu wasivue na zana hizi zisitumike. Anasema zisionekane hata kule baharini, mitumbwi na hata kwenye mialo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia kwako, nasema suala hili liangaliwe upya. Alikaa akaandika barua na hata wavuvi hakuwashirikisha, anasema kuwa amewashirikisha lakini nina uhakika hakuwashirikisha. Hakuwaita Wavuvi wa Tanga, Mtwara na hata wa Lindi, amekaa pale ofisini Dar es Salaam ameandika tu, mimi nina uhakika na hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amewastopisha hata wavuvi wanaovua kwenye Maziwa. Kwenye Maziwa sina uhakika nako, lakini kwenye Bahari haiwezekani kumzuia mvuvi asizamie na miwani. Kwa hiyo, suala hili naomba Waziri Mkuu utakapo-*rewind* utupe *facts*; utuambie kama wavuvi hawa wamezuiliwa wasivue kwa kutumia *ring net*; watumie nini sasa?

Tunaomba tuambiewe kwamba, hawa watu tumewazuia kutumia nyavu hizi sasa watumie uvuvi huu. Wasizuiliwe kutumia uvuvi ule wakaachwa tu, tutazalisha watu wabaya wa aina nyingi sana, kwa sababu wanaofanya kazi hii ni wengi katika nchi hii, kwa hiyo, watakuwa hawana kazi za kufanya. Naomba wapewe kazi nyingine mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri atakapo-*wind up* atupe pa kushika na akisahau sisi tutamkumbusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie kuhusiana na suala la Mahakama ya Kadhi Mkuu. Suala hili kila siku tunalisema hapa Bungeni, Wabunge wengi

tumelizingumza na mwaka jana mimi nililizingumza vya kutosha. Kila siku tunazungumza lakini halifiki mwisho; kila siku tunaambiwa kuwa linaendelea, mara tunaambiwa linakwenda kwenye mjadala, mara kwenye kura ya maoni; ina maana nchi yetu sisi suala likitaka kuamshwa linapelekwa kwenye kura ya maoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la Kadhi tuliambiwa mwaka jana kwamba, linapelekwa kwenda kusikiliza maoni ya wananchi; sasa maoni yao hayaishi tu mpaka leo? Tunataka tupate jawabu kwamba, suala hili pamoja na kuwa limo kwenye Ilani yenu ya Chama cha Mapinduzi, tunataka tujue kama hili lipo au halipo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo asubuhi kuna Mbunge mwenzetu kutoka Zanzibar alichangia na akasema kuwa sisi *CUF* hatujulikani tunataka nini; tunataka Muafaka, Serikali ya Pamoja au tunataka kujitenga?

Hatujulikani tunachotaka watu wa *CUF* na ninawaomba muwe wastahimilivu kwa sababu tunapozungumza masuala haya, wengine huwa wanaumia kwenye roho hawawezi kuyasikiliza. Mimi naomba, asiyeweza kusikiliza bora atoke lakini ni lazima nizungumze, kwa sababu ni Mbunge, nimechaguliwa na watu na nawawakilisha watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi watu wa *CUF* tunataka tufikie Muafaka baina ya *CCM* na *CUF* na baadaye tuunde Serikali ya Pamoja ya Zanzibar, ambayo kweli itawashirikisha Wazanzibari wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliyopo siyo ya Zanzibar ni ya Unguja. Nasema wazi, ile ni Serikali ya Unguja; ninayo sababu na nitaitoa hapa, naomba uniruhusu nisome hapa kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shoka, naomba hicho unachotaka kukisoma lazima uwasiliame na Mwenyekiti. Unasoma nini; unanukuu hotuba ama unanukuu kitu chochote ambacho unataka ukisome hapa, kwa sababu Kanuni hazimruhusu Mbunge ye yeyote anapochangia asome? Sasa ningependa kujuu kitu hicho unachotaka kukisoma kabla sijakuruhusu.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kunukuu notisi zangu lakini, sikilizeni, mimi kichwa changu nakiamini; sina kichwa kibovu na nitakayoyazungumza yote yatakuwemo kwenye karatasi yangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shoka, naomba ukae. Ninakuruhusu uendelee kuchangia na si kunukuu kwenye karatasi ambalo unalo. Kanuni haziruhusu mtu anapochangia anukuu anayotaka kuyasema kwa kusoma kile alichokiandaa kwa kukiandika.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwambia hivi; mimi ninayotaka kuzungumza nitayatoa kwenye kichwa changu, sisomi tena, ninayo kichwani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ya Zanzibar au ya Unguja, imeundwa naanza kwa Mawaziri; Mawaziri wote ni 15, katika Mawaziri 15 aliyetoka Pemba ni Waziri mmoja; je, hiyo ni haki kweli jamani?

Nazungumzia Naibu Mawazi ni watano, aliyetoka Pemba ni mmoja. Naendelea, aliyekuwa anasema si kweli aje athibitishe haya ninayosema kama siyo kweli. Wakuu wa Mikoa ni watano kati ya hao Mpemba ni mmoja. Wakuu wa Wilaya ni kumi kati ya hao Wapemba ni Watatu. Makatibu Wakuu ni 15 kati ya hao Wapemba ni wawili. Naibu Makatibu Wakuu ni 12 kati ya hao Pemba *zero*; hakuna mtu. Tunatoka hapo tunakwenda kwenye Wakuu wa Polisi, Makamishna pamoja na Makamanda wapo 18, lakini pemba hakuna hata mmoja ni *zero*. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vikosi vya SMZ viro vitano, kati ya vikosi hivyo ni *zero*. Wakuu wa Idara, wapo 100 kati ya hao kuna watu 17; wao wana 83. Jamani hiyo kweli ni haki na ninyi msimame na haki siyo mwitikie tu hapana, semenjambo kwa haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tuliambiwa kuwa, Rais aliyepo madarakani hakuchaguliwa Pemba, ndiyo maana hakuchagua Mawaziri Pemba. Makatibu Wakuu, pamoja na Watendaji wengine, huwa ni lazima uchaguliwe. Suala hili lishughulikiwe, kama halishughulikiwi litatutia aibu kila siku, maana sisi wengine kila siku tutalisema humu. Mkilirekebisha na likakaa sawa, hatutalitaja tena, lakini likiendelea na sisi tutaendelea kulisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la kuhamia Dodoma.

(*Hapa Wabunge fulani walipiga kelele*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wakizungumza wao sisi tunanyamaza kimya, lakini sisi wengine tukizungumza wanatutilia maneno. Ngojea Mheshimiwa Khalifa hili ni Bunge.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shoka, wewe unaongea na Mwenyekiti, endelea

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hivyo, lakini sipendi nizungumze na watu wengine wanaongea nyuma, si heshima hiyo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia suala la kuhamia Dodoma, naona bado Serikali haijawa *serious* na kuhamia Dodoma, kwa sababu kila siku inatenga fedha kidogo kwa ajili hiyo. Mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni 2.3; hizi ni kidogo sana kwa ajili ya kuhamia Dodoma. Kama tuna nia hasa ya kuhamia Dodoma, tupangeni fedha za kutosha kujenga majengo kwa ajili ya kuhamia Dodoma. Kila siku kupeleka fedha kwa ajili ya kumalizia *Nyerere Square*, kuzibua mitaro, kujenga mnara wa kumbukumbu, sijui kujenga barabara moja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu toeni fedha hasa kwa ajili ya kujenga Dodoma na baadaye tuweze kuhamia Dodoma na si kutoa kidogo kidogo kama tunavyofanya. Sasa juzi tuliambiwa tuna miaka 35 ya kuhamia Dodoma, naona itakwenda mpaka 60 bado hatujahamia Dodoma. Kwanza, kuna sababu nyingine ya msingi; Mheshimiwa Waziri Mkuu, naona ofisi yako inajengwa Dar es Salaam, ile ilikuwa ijengwe Dodoma kama kuna nia nzuri ya kuhamia Dodoma. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nafikiri *message sent*, nashukuru sana. (*Makofi*)

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii. Naomba sijui nianzie wapi, lakini nianzie hapo hapo alipoanza Bwana Shoka. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu alisema mkianza kupanda mbegu ya ubaguzi haitakwisha. Tunazungumza suala la Upemba na Uunguja, tumesahau kwamba, Tanzania ina makabila 125. Mkianza kuzungumza hivyo, mimi Maganga Zanzibar nitakaa kisiwa kipi? Nadhani waliochaguliwa na Rais wa Zanzibar, wamechaguliwa kwa sababu ya sifa za kufanya kazi na si kwa sababu mtu anatoka kisiwa hiki au kile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee kuuimarisha umoja wetu. Tuna Makamu wa Rais anatoka kule, hiki ni cheo kizito sana katika Taifa letu. Niishie hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba, kila Mbunge anayetoka Zanzibar ukiachia jimbo lake, lakini ile Zanzibar nzima, ndio jimbo lake anapoingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Nimekuwa nasema hili kwamba, tumeishi vizuri toka mwaka 1964 mpaka leo hii. Hivi sasa Zanzibar hali yake ya uchumi siyo nzuri, lazima Jamhuri ya Muungano ichukue jitihada za makusudi za kukuza uchumi wa Zanzibar. Bajeti ya Jamhuri ya Muungano nimeambiwa ipo shilingi trilioni 7.2, Bajeti ya Zanzibar ipo kwenye shilingi bilioni 360; hawajafika hata trilioni moja. Hali ya uchumi wa Zanzibar ni mbaya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba ikiwa na njaa, watu hawaelewani; haya maneno yote sijui Upemba, Uinguja ni njaa tu. Kama mambo yatakuwa mazuri, hakuna njaa, hakuna maneno na wala watu hawatauliza makabila yao. Mahali ambapo watu wanashirikiana kwa ukamilifu, hakuna mambo ya Unguja na Pemba. Hivi atokee Muunguja gani atakayeniambia hana uhusiano na Pemba, hasa wakubwa wakubwa. Mtu ametoka Unguja anakwenda kuoa Pemba, ametoka Pemba amekuja kuoa Unguja; huu ndiyo ushirikiano. Nilimwona hapa mzee mmoja alikuwa Mbunge, Mzee Aida, alikuja kuoa Unguja, kazi kubwa ilikuwa kuwatoa ng'ombe huko Mara kuwapeleka Unguja. Hii yote ni katika mshikamano, nadhani sisi wanasiwa tusijielekeze huko, tukae tujenge uchumi wa nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali ya awamu hii, inajitahidi sana kuhakikisha kwamba, uchumi wa nchi unakua na uchumi wa Zanzibar ukue uende sambamba. Nilikuwa nampa pole Mheshimiwa Waziri Mkuu, mimi sikumpongeza siku alipochaguliwa, kwa sababu sasa yupo kizuijini, akiingia anaingia watu wanamlinda, akitoka hivyo hivyo, ukitaka kusema naye mpaka uombe ruhusa. Hee! Pole mwenzangu. Mimi hata sijaja kuomba kuongea na wewe, maana naona nikisogea pale kuna vijana wengi pale. Wengine wanaona fahari ukiwa Waziri Mkuu, lakini ukitazama wengine hao waliokaa nyuma yako wanakuwa hawapo unabakia peke yako katika hii hoja, ndiyo mfano huu. Wazee ni mambo ya kuangalia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wa *CUF* wana mtindo wa kuchupia hoja, maana hapa wamechupia hoja ya Chifu Kadhi. Hii hoja imo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na ni hoja ya Chama cha Mapinduzi. Kwa umoja wetu na mshikamo wetu, tutahakikisha kwamba, hoja hii inatekelezwa kwa nguvu zetu zote. Hapa ipo, mimi nimesoma Ilani ya *CUF* lakini sikuona wamelizungumzia mahali popote. Tunazungumza katika Chama. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Naomba kwa heshima na taadhima, niinukuu ilivyozungumzwa. Ipo kwenye ukurasa wa 132(b), kulipatia ufumbuzi suala la kuanzishwa kwa Mahakama ya Kadhi Tanzania Bara. Haya niambieni sasa kuna Ilani gani iliyozungumza habari hii kama siyo Chama cha Mapinduzi? Ilani hii tumeinadi sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la muda mrefu na ndiyo maana hawa rafiki zangu akina Shoka wanalichupia sasa. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa N'hunga ongea na Mwenyekiti.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Nakushukuru sana Mwenyekiti. Wenzetu watu wa Kenya, jambo hilo kwoo limo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Kenya. Ninayo Katiba hapa ya Kenya hii hapa, suala la Chifu Kadhi lipo kwenye ukurasa wa 63.

Sasa naiomba sana Serikali yangu Tukufu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nasikia kwamba, kuna mkakati wa kukusanya maoni; hivi ninyi watu wa Serikali hizi fedha mnazozitumia mara mbili mbili hamwoni uchungu wake?

Jambo hili limeanza na Kamati ya Bunge, tukazunguka nchi nzima ili kupata maoni, tukaandaa tena miaka mitano ilipita tukaandaa Kamati nyingine ya Bunge na taarifa tukatoa, tukazunguka tukatoa maoni, tumezunguka ndani ya nchi, tumekwenda nje ya nchi, wengine wamekwenda Afrika Kusini, wengine Uganda na nchi nyingine; bado mnataka mawazo gani?

Mimi ninavyoolewa, maana siku hizi Serikali huwa inapora madaraka ya Bunge na ndiyo maana Bunge tunaambiwa haliagizi linaomba katika Serikali. Bunge linaagiza, Serikali kazi yake kutekeleza yanayokubaliwa Bungeni. Tulishazungumza suala la Kadhi

tumelimaliza, tukaiachia Serikali mpaka leo, tunazungumza kutafuta maoni ya kitu gani? (*Makofi*)

Naomba sana jambo hili, Bunge hili sasa tusilizungumze tena, tupate utekelezaji wake. Mnatuchonganisha na wenzetu walioko nje, tunakuwa hatuelewani, baadaye zinakuja juhudzi za kuzima moto. Mrema kaleta sheria hapa haipo kwenye Bunge. Shehe Ramia Mbunge wa Bagamoyo aliileta hoja hiyo, hayupo tena Bungeni, mpaka amefariki bado tunazungumzia suala hili; hivi kuna kigugumizi gani? Naomba niachie hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo linaniuma NI suala la Makao Makuu. Sasa ni miaka 35 tunazungumzia Makao Makuu yawe Dodoma. Bunge limekuwa mfano wa kufanya vikao vyake vyote Dodoma, Serikali mnatuzungusha. Leo tunatafuta maoni, tunatafuta taratibu, hili jambo lilizungumzwa na *TANU* na tukakubaliana kwamba, tuyatekeleze mema yote ya *TANU* na *Afro-shiraz*. Wenzetu watu wa Serikali mnakuja tena na maoni mengine, tunataka tutafute maoni twende na kila kitu, ndani ya Ilani lipo linalosema ni kutunga Sheria ya kuwepo Makao Makuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu, hebu nyooresheni mikono msiotaka kuja Dodoma hapa Makao Makuu tujue Mawaziri wangapi hawataki.

Mimi nilitegemea sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, ulipochaguliwa siku ya pili yake ungesema unahamia Dodoma. Hapa Dodoma alihamia Mzee Kawawa, akapokewa na ngoma za watani wangu Wagogo. Mimi ni shahidi nilikuwepo, tulikuja kucheza ngoma za Kigogo. Leo hii wale waliosema wana ofisi Dodoma; ofisi moja ipo Dodoma na nyingine ipo Dar es Salaam. Maofisa wao hujui wanalipwa posho wapi, maana akifika Dar es Salaam anakuwa mgeni, akija Dodoma mgeni pia. Tunataka suala la kuhamia Dodoma liwe *serious*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Nigeria waliamua kuhama Lagos kwenda Abuja. Walituma timu yao ya watu 24 wakaja hapa *CDA* Dodoma, wakapewa mkakati wa *CDA* wakaenda nao kule na ndio wakajenga ile Abuja. Ukifika Abuja hoja ya kwanza unaulizwa Dodoma ikoje, tunasema Dodoma ipo hoi, lipo jengo la Bunge tu. Mheshimiwa Waziri mmoja ananiangalia pale anajua naelewa tunaelewana hapa. *CDA* ilikuwa na Waziri wa Ustawishaji Makao Makuu Dodoma, mwisho ikabakia yenyewe *CDA* na kila kitu ikawa hoi.

Leo tunazungumza nini sisi tunataka utekelezaji wa Programu ya Kuhamia Makao Makuu. Bunge limeonyesha mfano tu, sasa siku hizi kila kitu Bunge limehamia Makao Makuu, tunataka Wizara zote zihamie Makao Makuu.

Tengenezeni miuondombinu, shule za sekondari na kila kitu, maana kuna wakubwa wanalala Dar es Salaam tu, tunataka Dar es Salaam uwe mji wa biashara. Mwalimu alisema Dodoma ni Makao Makuu, katikati ya nchi na hasa Makao Makuu ilikuwa yawe Manyoni lakini tukasema tuvute kidogo tuweke Dodoma. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali yako na wenzako, haya sitakuuliza mimi atakuuliza Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia nizungumzie suala la Ofisi za Wabunge. Wabunge wa Tanzania, wanafanya kazi katika hali ngumu sana. Hakuna Mbunge hata mmoja mwenye Ofisi, wana chumba ndani ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, ofisi nyingine haziingiliki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipata nafasi ya kutembelea Mikoa kumi, kuangalia Ofisi za Wabunge. Nianze na ofisi ya Mheshimiwa John Malecela, katika ofisi iliyokuwa dhaifu hakuna kama hiyo.

Nataka niseme ukweli, Ofisi za Dar es Salaam pale wamepewa lakini hakuna chochote, hujui kama unakwenda kwa Mkuu wa Mkoa au unakwenda kwenye Ofisi ya Mbunge. Wabunge wa Viti Maalum hao ndiyo kabisa wapo hoi, wengine hawajui wafanyie wapi kazi. Hawajui hata wakutane wapi na wapiga kura. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ambayo ina uhuru zaidi ya miaka 40; Mbunge wake hajui akafanyie kazi wapi! Wabunge hawa hawana wasaidizi ambao ni *competent*; wana waratibu katika ofisi zao, anaambiwa ni msaidizi, lakini yeye anauliza unafanya ziara mzee ndiyo, kesho ndiyo, imeletwa barua, anasema barua yako hii hapa.

Hakuna msaidizi wa kumshauri Mbunge mambo ya kiuchumi, mambo ya kisheria na mambo mengine. Wabunge wengine ofisi zao zipo ndani ya magari.

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tungeomba sana, jambo hili lisimamiwe na Serikali kwa nguvu zake zote. Nimeona Wabunge wengine wana uhusiano na Wabunge wa Ulaya; sijui wanapokuja wale Wabunge wa Ulaya katika Majimbo yao wanawapeleka wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifika katika Ofisi ya Mwenyekiti mmoja, Mheshimiwa William Shellukindo, ukiiona unaanza kujiuliza hii ofisi iliyopo Bumbuli kweli ni ya Mheshimiwa William Shellukindo? Maana ni ndogo, sijui imekaa namna gani, hawezi hata kupumua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la kujenga Ofisi za Wabunge lilikuwepo kwa muda mrefu sana. Niliona ofisi ambayo ilijengwa mwaka 1960 ya Saruhati, ambayo Mheshimiwa Philip Marmo ndiyo yupo kule, nayo imepasuka pasuka, haingii hata kwenye ile ofisi maana yake hali yake ni mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naiomba sana Serikali yangu, kwa heshima na taadhima kuhakikishe kwamba ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge ni kengele ya pili.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Ya pili?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma N'hunga nakushukuru sana. Nimepokea viji-memo hapa Waheshimiwa Wabunge, wameniomba nimwambie Mheshimiwa Shoka, amsaidie Mheshimiwa Kombani kuelewa maana ya ku-rewind ili atakapokuwa anajibu hoja, aweze kufanya kazi hiyo sawasawa. Kwa hiyo, nitakuomba Mheshimiwa Shoka, kesho umtafute Mheshimiwa Kombani. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Naomba tuonane naye Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge, utaonana naye kwa wakati wako ili umsaidie kuweka sawa hilo ili aweze kufanya kazi yake vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, shughuli zilizopangwa kwa jioni hii ya leo zimekamilika na orodha ambayo nilikuwa nayo hapa mezani, naona tumefika hapo.

Naomba niseme tu wachangiaji watakaoanza kesho asubuhi, baada ya kipindi cha maswali na majibu; ataanza Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwape taarifa tu kwamba, utaratibu tunaoutumia wa kuwaita, tunafuata orodha kadiri ilivyo lakini pia tunazingatia jinsia; pande za Muungano na pia Kambi zote mbili katika kuchangia hoja hii iliyopo hapa mbele yetu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, niseme tangazo la mwisho; nimemwomba na Mheshimiwa William Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, niwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, Ndege za ATC sasa zitaanza kufanya kazi ya kutoka Dar es Salaam - Dodoma, Dodoma - Dar es Salaam. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tu niwape taarifa kwamba, ratiba itakuwa ni kila Siku ya Jumatatu na Jumamosi; saa 12.00 alfajiri itaondoka Dar es Salaam na kufika Dodoma saa 1.15 asubuhi na itaondoka saa 1.15 asubuhi kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam kila Siku ya Jumamosi na Jumatatu. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, usafiri huo wa ATC utaanza tarehe 30 Juni, 2008; kuhusu nauli tutapewa matangazo hayo baadaye.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya tangazo hilo, ninaomba niwashukuru sana kwa michango yenu na kwa muda tulionao sasa, naomba niahirishwa Shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.45 usiku Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 26 Juni, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*